



TAFUTA UKWELI

"Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru"
- Yohana 8:32

JOHN MOORE

Kimetafsiriwa kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili Na Charles Heberth

TAFUTA UKWELI

“Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru”

-Yohana 8: 32

Mwongozo wa Kujifunzia

John Moore

Kimetafsiriwa kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili

Na Charles Heberth Mwanga

World Video Bible School ®

www.wvbs.org

Tafuta Ukweli
(Mwongozo wa kujifunzia)

Kimetengenezwa na kuchapishwa na:
World Video Bible School.
25 Lantana Lane
Maxwell, TX 78656-4231
USA

Hakimiliki © 2012 na World Video Bible School®

ISBN: 978-0-9827455-3-3

World Video Bible School® ni chanzo chako cha elimu bora, kinadumu katika maandiko, si ya kimadhehebu. Kina mafundisho ya Biblia kwa njia ya DVD, MP3, CD-ROM na kurasa zilizochapishwa. WVBS ina masomo ya vitabu vyote vya Biblia kuyatumia ili liweze kuwa imara katika Bwana. WVBS ina jitahidi kulipatia kanisa nyenzo bora za kufundishia kadri iwezekanavyo.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kurudufu sehemu yeyote ya kitabu hiki kwa ajili ya kuuza bila ruhusa kutoka kwa mchapishaji. Hata hivyo, kutoa nakala kwa kiwango chochote ni ruhusa kwa ajili ya kufundishia darasani, kujifunza kwa mtu binafsi, jitihada za kiinjilist n.k. Kama una swali lolote kuhusiana na suala la hakimiliki inayohusisha upigaji wa chapa au uwezekano wowote wa kuitumia nyenzo hii, tafadhali wasiliana na ofisi za World Video Bible School®.

Vifungu vya Biblia vilivyotumika vimetoka katika The Union Version in Kiswahili

Kimechapishwa China.

Toleo la kwanza 2012, nakala 5,000

DIBAJI

Tafuta kama unaweza, lakini hutaweza kamwe kupata kitabu ambacho ni kikuu kuliko Biblia. Vitabu vyake sitini na sita vyenye ukweli wa milele, vilivyotungwa na Mungu mkamilifu anayejua yote, ni habari ya mbinguni kuhusu matukio makuu ya historia ya mwanadamu, yaliyoambatana na ujumbe wa ukombozi, msamaha na tumaini. Ujumbe wake kuhusu Kristo na msalaba ni wa ajabu, na hadithi yake ya upendo haitamkiki. Ufunuo wake wa neema ya Bwana na masharti ya utakaso ni nguvu dhahiri ya Mungu ambayo huwaongoza wenye dhambi wokovoni (Warumi 1:16). Watu wa kawaida kamwe hawawezi kuboresha hekima itoayo au mafundisho ifundishayo. Hivyo nyezo pekee ya kuboresha ni lazima iwe katika maeneo ya ni jinsi gani tuna maarifa ya kutumia upanga wa haki, uwezo wetu wa kutumia njia za kufundishia zilizoruhusiwa katika Biblia (kwa mfano, mifano iliyotumiwa na Yesu), na juhudi zetu za kuufikia ulimwengu wote tukiwa na ukweli wake.

Kipindi chetu kilichopiga hatua kiteknolojia, tumebarikiwa kuwa na njia mbalimbali za kueneza ujumbe wa Mungu wa matumaini na kweli. Haya maendeleo, ijapokuwa hutumika kama chombo muhimu katika kueneza injili, kamwe hayawezi na hayataweza kuchukua nafasi ya ujumbe wa kushangaza wa Kristo. Haijalishi uvumbuzi au mitindo ya ubunifu wa kuwasilisha, kamwe haiwezi kuwa mbadala wa ukweli wa Biblia. Hata hivyo tatizo ni kwamba katika kuziongoa roho kwa Yesu, maadili ya uthabiti wa Ukristo hayajawa ni ujumbe, badala yake tatizo mara kwa mara limekuwa katika kutafuta njia ya kumtia mtu moyo aweze kuguswa na maandiko matakafu. Kama kanisa la leo litatumia njia zenye ufanisi zaidi katika kuzifikia roho zilizopotea likiwa na ukweli wa Mungu (kama mitume walivyofanya walipokuwa wakisafiri na majahazi au katika kumtumia mjumbe), ndipo idadi kubwa ya watu wataokolewa. Hii ni kweli, si kwa sababu ya njia za kuenezea, bali kwa sababu injili itakuwa na fursa kubwa ya kuangaza miongoni mwa idadi kubwa ya watu. Katika kipupwe cha 2004, utengenezaji wa video ya Tafuta Ukweli ulianza kukiwa na wazo hili akilini – kuzalisha chombo ambacho kupitia kwacho injili itajulikana kwa watu wengi (sehemu kubwa ambayo kwa hakika hawako tayari kujitoa kujifunza darasa la Biblia la mtu na mtu).

Kama vile DVD ya Tafuta Ukweli inavyoanza kusambazwa mbali zaidi, maombi mbalimbali yalitolewa kwamba namna ya maandishi ya Tafuta Ukweli yapatikane ili kuwa msaada kwa watazamaji katika kuelewa, kushika na kufahamu masomo yanayotolewa kwenye video. Pia ilisemekana kwamba masomo kwa njia ya maandishi yanapaswa kujumuisha maswali ya kujifunzia na dondoo za ziada kuhusiana na mambo mbalimbali ya kimafundisho. Ni dhahiri pia kwamba kuna mahali walipo watu wanaohitaji kufahamu yaliyomo katika mpango huu (kitabu) lakini hawawezi kutumia video (kama vile wafungwa, magereza, nchi fulani za kigeni, n.k) Hii ililazimisha hitaji la kitabu ambacho siyo tu kinahusisha mambo ya msingi yaliyomo kwenye mpango huu

lakini pia ambacho kinamruhusu mtu – kupitia matumizi ya maandishi-ili kiwe mwalimu wake mwenyewe. Kwa kifupi, mwongozo wa kujifunzia ulihitajika ambao ungeweza kutumika kwa njia mbalimbali na ungetumika sambamba na video na kuwa kama kitabu cha “kujitegemea” kwa ajili ya matumizi ya uinjilisti na uelimishaji.

Kitabu ambacho sasa umekishika mikononi mwako ni matokeo ya mahitaji hayo. Ili hali hakiendani neno kwa neno na kile kilichopo katika video, lakini kinakaribiana sana. Hii inamaanisha kwamba watu ambao wanadvd ya Tafuta Ukweli na ambao wanataka kutumia mara kwa mara Mwongozo huu wa kujifunzia wanaweza wakafanya hivyo kwa urahisi sana huku wakifuatilia kwa urahisi yaliyomo katika video. Lakini pia inamaanisha kwamba, katika baadhi ya maeneo kitabu hakiko kama vile mimi mwandishi ningelitaka kiwe. Kuwasiliana ana kwa ana mara kwa mara huwasiliana katika aina tofauti kuliko insha zilizoandikwa, na kwa hiyo katika maeneo mbalimbali unaweza ukakuta masomo yanakosa muundo sahihi na neema halisi. Kwa ajili ya hili ninaomba msamaha. Mpango wa awali wa maandishi ulikuwa ni kutumika kama mswaada wakati wa utengenezaji wa filamu. Sala zangu ni kwamba utaangalia mbali zaidi ya ukomo huu na upungufu wangu kama muwasilishaji, na kuangalia Ukweli thabiti wa Ukristo na ujumbe wa Mungu wa wokovu kama ulivyowasilishwa katika kitabu hiki.

Kama ilivyotajwa mwanzoni, moja kati ya malengo yetu katika kutengeneza Tafuta Ukweli ni kuupeleka ukweli wa neno la Mungu kwa watu wengi kadri iwezekanavyo, ili kwamba kila mahali roho zipate nafasi ya kuishi milele pamoja na Mungu. Pamoja na utengenezaji wa Tafuta Ukweli, kwa sasa tunaweza kuwa na ufanisi zaidi wa kulitimiza lengo hilo. (pia ninaweza nikaelezea katika shukrani hizi kwamba kitabu cha Tafuta Ukweli, kwa sasa kimetafsiriwa katika lugha mbalimbali za kigeni ili kwamba watu ambao hawazungumzi wala kusoma Kiingereza nao pia wapate fursa ya kuyajua masomo haya. Zaidi sana, wakati hiki kitabu kilipokuwa kikipangiliwa na kubuniwa, mswaada wa neno kwa neno wa mpango wa Tafuta Ukweli ulikuwa umekamilika, na unatumika kuandaa toleo la Kiingereza ambalo linavipengele vidogo vidogo. (kwa wale ambao hawana uwezo wa kusikia) pamoja na matoleo mbalimbali ya DVD za lugha za kigeni.)

Kama mtu ninayewiwa na Kristo, ningependa kuyapendekeza kwako masomo ambayo yanatolewa katika kitabu hiki – katika tumaini kwamba si tu kwamba yatakusaidia katika kujifunza kwako neno la Mungu, bali pia yatakusaidia wewe katika kuwasaidia wengine “kuifahamu kweli” (Yohana 8:32) – ukweli ambao unatuweka huru.

John Moore
December 2006

Yaliyomo



Sura ya 1 - *Kuhusu Ukweli*

5



Sura ya 2 - *Kuhusu Muumbaji*

10



Sura ya 3 - *Kuhusu Mamlaka kwenye Dini*

24



Sura ya 4 - *Kuhusu Kanisa*

44



Sura ya 5 - *Kuhusu Nyumba ya Mungu.*

66



Sura ya 6 - *Kuhusu Ubatizo*

90



Majawabu

116



Tafuta Ukweli

KUHUSU UKWELI



Kuhusu Ukweli

KUHUSU UKWELI

Kwa miaka mingi, nimeongoza mazishi mengi na nimekuwa kwenye maeneo mengi ya makaburi. Na kila wakati ninapoendesha ibada ya mazishi au kutembelea makaburi, Ninakumbushwa *kwamba* kifo ni hakika na hakiepukiki. Je, unafahamu kwamba wastani wa watu 107 hufa kila dakika? Hao ni watu 153,000 kwa siku, hiyo ni idadi ya kushangaza. Ni vigumu kufikiri kwamba watu wengi hufa kila siku. Lakini hutokea. Kifo huja kwa walio wazee sana, wadogo sana na kila mtu katikati ya umri huo. Kadiri *tunavyopenda* kuendelea kuishi sisi sote *tutakabiliana* na kifo.

Lakini ni nini kitatutokea baada ya kufa? Je, kuna maisha baada ya kufa? Kama ndivyo, Je, ni maisha ya *aina* gani? Je, Mbingu ipo? Je, Jehanamu ipo? Na kama ndivyo, Je ni kitu gani *kitakutokea* wakati utakapokufa? La muhimu zaidi, Je kile unachiamini kitajalisha au jinsi ulivyoishi katika maisha haya? Na je, jibu la maswali hayo litaathiri hatima yako ya umilele?

Watu wengi wanaamini kwamba wengi kati ya wale ambao wanakufa wataishia kuingia mbinguni. Lakini sikiliza kile Yesu alichokisema katika Mathayo 7: 13-14

Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba, maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache. (Mathayo 7:13-14)

Je, umekielewa kile Yesu alichokisema? Kuna *wachache* ambao watauona uzima, na *wengi* ambao watachagua njia iendayo upotevuni. Je wewe ni miongoni mwa *wachache* au miongoni mwa *wengi*? Je, *unauhakika* kuhusiana na ni wapi utakapo kuwa milele?

Kile ambacho ni cha busara zaidi ni ambacho Yesu alisema kuhusu wale ambao watamwamini yeye kama Mwokozi

Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wata-niambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe, ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu” (Mathayo 7:21-23)

Kulingana na kile Yesu alichokisema, kutakuwako na watu wengi wa *kidini* ambao hawataingia mbinguni. Kwa *kuliita* tu jina la Yesu kama Mwokozi wetu ni wazi kabisa kwamba haitoshi kuziandaa roho zetu kwa ajili ya mbingu. Kulingana na Mathayo 7:21, tunapaswa *kuyafanya* mapenzi ya Baba ili tuweze kwenda mbinguni.

Hebu sasa nikuulize baadhi ya maswali. Je, *wewe* umeya-

fanya mapenzi ya Baba? Kama ungelikufa leo na kusimama mbele ya Yesu, Je, Yeye angelikuambia nini? Je, angelisema, “Ondoka kwangu, sikukujua kamwe?” Au angeliku-karibisha mbinguni? Je, wewe una uhakika *thabiti* kuhusu hili? Je, umeshawahi kujiuliza iwapo *umeokolewa kweli* au la? Je, una mashaka, hofu au maswali?

Kama umeshawahi kuwa na maswali kuhusu maisha baada ya kifo, ndipo labda ukawa unastaajabu kuhusu azma ya wewe kuwepo hapa duniani. Umejiuliza maswali kama, “Je, ni kwa nini mimi niko hapa?” na “Je, Mungu anamakusudi na mimi?” Tangu mwanzo wa wakati, wanadamu wamekuwa wakijiuliza haya maswali. Wanafilosofia, Wanatheologia, Wakemia, akina mama na akina baba, seremala, wanasheria, hawa wote wamejiuliza maswali haya.

Kwa bahati mbaya, majibu mengi ya uongo yametolewa kwa ajili ya maswali hayo. Baadhi ya hayo majibu yanayapinga mengine. Inaweza kuchanganya na kuchosha, haswa pale inapoonekana kuwa na majibu mengi tofauti yanayotolewa.

Sasa, Je, majibu ya *kweli* kwa maswali haya ni yapi? Je ni majibu gani yaliyo *sahihi*? Je inajalisha *kile tunachoamini* na *jinsi tunavyoishi* hapa duniani? Je ungelipenda kuwa na uhakika thabiti? Je hungelipenda kuufahamu *ukweli*?

Ninataka ujue kwamba hakuna hata mmoja wetu ambaye anapaswa kupitia maisha huku akitangatanga. Mtu mkuu kuliko wote ambaye aliwahi kutembea katika uso wa nchi alituletea majibu ya maswali hayo – majibu ambayo yatatuweka huru kutoka katika mashaka, hofu na woga wetu. Hayo majibu yanaweza yakapatikana katika Biblia, kwa sababu katika kitabu hicho kikuu Yesu anatuambia kuhusu ukweli, na ni jinsi gani kweli itatuweka huru.

...Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli. Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru. (Yohana 8:31-32).

Hayo ni maneno yenye nguvu sana. Kwa kadiri tunavyoendelea kutafakari maana ya kifungu hiki, hebu tuangalie vitu vitatu kuhusiana na ukweli

Kwanza, Yesu alifundisha kwamba *tunaweza tukaitifahamu kweli*. Ukweli upo. Ni hakika. Siyo tu chochote unachoamini au kile mtu mwingine anachoamini kuwa ndiyo ukweli. Ukweli ni halisi! Kuna kipimo/ kiwango cha kugundua kipi ni sahihi na kipi si sahihi, na kwa kile ambacho ni chema na kiovu.

Haupaswi kuhangaika ili kujua kama ninasema ukweli au la, ama mtu mwingine ana kuambia ukweli. Ukweli kwa hakika upo. *Tunaweza* tukajua kile tunachohitajika kufanya ili twende mbinguni.

Sura ya 1

Pili, siyo tu kwamba tunaweza *tukajua* kwamba ukweli ni nini, lakini pia *kweli itatuweka huru*. Unaweza kutuweka huru kutoka katika vifungo vya dhambi. Yesu alisema, “Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi.” (Yohana 8:34). Hebu nikuulize – Je, unapambana na dhambi? Je ni mzigo mzito? Je, wewe umekuwa ni mtumwa wa pesa, pombe au madawa ya kulevya, picha za ngono, n.k? Vipi kuhusu uhusiano wako na mwenzi wako? Je, unashindwa katika majukumu yako kama mzazi? Je, maisha yako yamejaa visasi, wivu, chuki au ubaguzi wa rangi? Hivi vitu vinaweza kutulemea sana. Vinaweza kuwa mizigo mizito kwetu. Lakini nataka wewe ujue kwamba kuna tumaini, kwa sababu kweli itatuweka huru kutoka katika hii mizigo.

Siyo tu kwamba kweli itatuweka huru kutoka katika tabia zisizo za haki, bali pia itatuweka huru kutoka katika kutenda matendo ya uongo ya kidini na mapokeo ya wanadamu. Kama vile baadhi katika karne ya kwanza waliokuwa watumwa kupitia dini zilizoundwa na wanadamu za mapokeo ya Mafarisayo zilizotajwa kweye Mathayo 23:1-33 na Marko 7: 1-13, kuna watu wengi leo ambao wanalemewa na matendo mbalimbali ya kidini, kanuni na sherehe ambazo hazijatajwa mahali popote kwenye Biblia, na kwamba hazijaamriwa na Mungu. Haya mafundisho na mapokeo ya wanadamu yanaweza yakatuchosha na kutulemea. Lakini baya zaidi, yanasababisha ibada yetu iwe ya bure. Katika Mathayo 15:9, Yesu, katika kuzungumzia mapokeo ya Mafarisayo kwamba hayajaamriwa na Mungu, alisema,

“Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu”.

Sasa vipi kuhusu *wewe*? Je, uko katika kifungo cha mapokeo ya kidini na mafundisho ya wanadamu? Je, umeshawahi kufungwa na mafundisho na amri za wanadamu? Je, umeshawahi kuombwa ufanye vitu ambavyo Mungu hajawahi kamwe kukutaka uvifanye? Kama ndivyo, Ninataka wewe ujue kwamba, *kunatumaini* tena, kwa sababu ukweli unaweza kutuweka huru kutoka katika aina hii ya utumwa.

Tukiwa na maarifa ya kweli, hatupaswi tena kushikwa mateka na vitu visivyo hakika, mashaka, hofu au kukata tamaa. Ikiwa inakuja katika njia ya wazi ya tabia ya dhambi, au katika hali ya matendo ya dini za uongo, dhambi kwa hakika inatutumikisha na kutufunga. Lakini bado Yesu na neno lake *anaweza* kutuweka huru. Shetani, baba wa uongo na matendo yote maovu (Yohana 8:44) hapaswi *kuwa* bwana wetu. Tukiwa na ukweli katika upande wetu, Yesu, Mtawala mwenye nguvu wa Ulimwengu, anaweza kuwa Kiongozi na Bwana wetu.

Tatu, siyo tu kwamba tunaweza kuijua kweli, na siyo tu kwamba kweli itatuweka huru, bali kila mtu anahitajika kufahamu kwamba *kweli inapatikana ndani ya Yesu*. Akiwa hapa duniani, Yesu alisema kwamba Yeye na ni Yeye pekee ndiye kweli.

...Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima, mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi. (Yohana 14:6)



Kuhusu Ukweli

Kama tunautafuta ukweli, na kama Yesu ni kweli pekee, ndipo tunapopaswa kwenda kwa Yesu kuitafuta kweli.

Biblia inafundisha wazi kwamba kweli inapatikana kwa Yesu binafsi na maneno yake. Angalia tena kile Yesu alichokisema kuhusu kweli:

...Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli, tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru. (Yohana 8:31-32)

Ni maneno ya Yesu ndiyo yatatuweka huru. Kweli, hata hivyo, ni bidhaa ya thamani na kwa maneno ya mwandishi wa Agano la Kale, tunaweza kusema, “Inunue kweli, wala usiiuze” (Mithali 23:23). Ukweli, kama ulivyofunuliwa katika Biblia, ni wa muhimu sana. Kwa kusoma 1 Petro 1:22, tunajifunza kwamba kweli hutakasa nafsi (roho) zetu. Kwa kusoma 2 Wathesalonike 1:7-9, tunajifunza kwamba tunapaswa kuitii kweli kama tunataka kuiepuka adhabu ya milele.

Maisha hayana uhakika kabisa. Miili ya walio wadogo sana, wazee sana na rika lolote katikati yao iko katika makaburi ulimwengu mzima. Baadhi yao wamekufa ghafla bila hata kuonywa. Ninastaajabu ni wangapi miongoni mwao wamekufa bila kuijua kweli. Hakuna hata mmoja wetu mwenye ahadi ya kuishi sekunde ijayo katika dunia hii. Ingawa wengine wanaweza wakaishi kwa miaka 70, 80, 90, au hata 100,

kitu kimoja ni hakika, kwa kadiri dunia inavyozunguka, watu watakuwa. Kipi kifuata? Biblia inasema tutahukumiwa kulingana na kile tulichokifanya hapa duniani. Kulingana na Warumi 2:2 na Warumi 2:16, kipimo cha hukumu kitakuwa ni Injili – kwa njia nyingine inafahamika kama Kweli. Wote tutahukumiwa kulingana na Kweli.

Unaweza ukawa unafikiria, “Lakini mimi tayari nimeshaokoka. Ni mnyofu kwa kile ninachokiamini, na hisia zangu zinambia kwamba tayari nilishaugundua ukweli” Ninatumaini uko sahihi. Ninatumaini umeshaugundua ukweli. Lakini tambua jambo moja: imani peke yake haitoshi kukuokoa!

Kabla ya kuitii injili, mtume Paulo yeye mwenyewe alikuwa mtu wa dini na mnyofu sana kuhusiana na imani yake. Bado alikuja kutambua kwamba yeye ni mkuu wa wenye dhambi (1 Timotheo 1:15). Katika Mdo 22, tunasoma kuhusu mtume Paulo akitufunulia kwamba alikuwa na shauku kwa Mungu, hata alipokuwa anawauwa Wakristo. Paulo alikuwa mwaminifu, lakini alikuwa mwaminifu kimakosa.

Sasa vipi kuhusu wewe? Labda unashauku kiasi kikubwa, lakini kamwe hujawahi kuyachunguza maandiko ili kuona kama mambo unayoyaamini yanaendana na Biblia. Je, unaifahamu kweli? Na Je, unauhakika kuhusu hayo? Kama sivyo, basi ungana nami katika safari hii ya Kutafuta Ukweli.

SEHEMU YA MARUDIO: KUHUSU UKWELI

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kwa wastani, ni watu wangapi hufa kila siku? _____
2. Kulingana na Mathayo 7:13-14, Je, kutakuwa na “wengi” au “wachache” ambao wataingia kupitia mlango mpana kwenda kwenye maandamizi? WENGI / WACHACHE
3. Kulingana na Mathayo 7:21-23
 - a. Je, Yesu atawaokoa wote waliitiao jina lake? NDIYO / HAPANA
 - b. Je, watu wengi wa kidini watapotea? NDIYO / HAPANA.
 - c. Je, mtu anapaswa kufanya nini ili aweze kwenda mbinguni? _____
4. Kulingana na mstari hapo chini, Je, inawezekana kumwabudu Mungu bure? NDIYO / HAPANA.

Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu. (Mathayo 15:9)

Sura ya 1

5. Kulingana na Yohana 8:31-32, Yesu alisema _____ itakuweka huru.
6. Kweli inaweza kumweka mtu huru kutoka katika _____, _____, _____ na _____ ya wanadamu.
7. Kulingana na Yohana 14:6
 - a. Kweli inapatikana katika _____
 - b. Je, mtu anaweza kwenda kwa Baba bila kupitia kwa Yesu? NDIYO / HAPANA.
8. Kulingana na mstari hapo chini, kwa kuitii kweli, Je, mtu anaweza akaitakasa roho/nafsi yake? NDIYO / HAPANA.

Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo (1 Petro 1:22)
9. Kulingana na mstari hapo chini, Je, wale ambao hawataitii kweli wataadhibiwa milele? NDIYO / HAPANA

Na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi, wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake, katika mwali wa moto, huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasio itii injili ya Bwana wetu Yesu, watakoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake (2 Wathesalonike 1:7-9)
10. Kulingana na mstari hapo chini, siku ya hukumu, kila nafsi/ roho itahukumiwa kulingana na _____ (Injili).

Nasi twajua ya kuwa hukumu ya Mungu ni ya kweli juu yao wafanyao hayo (Warumi 2:2)

Katika siku ile Mungu atakapozihukumu siri za mwanadamu, sawasawa na injili yangu, kwa Kristo Yesu. (Warumi 2:16)
11. Kabla mtume Paulo hajafanyika kuwa Mkristo, alikuwa mnyofu katika imani ya dini yake, likini alikuwa mnyofu _____.
12. Je, unyofu peke unaweza kuiokoa roho kutoka Jehanamu? NDIYO / HAPANA.

MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Ikiwa katika hatua fulani ya kujifunza kwako *Tafuta Ukweli* ukagundua kwamba kile ulichokuwa ukiamini kwa unyofu au kukifanya ni kinyume na mafundisho ya Biblia, Je, utabadilika ili uwez ekufuata mapenzi ya Mungu? NDIYO / HAPANA
- B. Kulingana na Mathayo 7:21-23, Je, umeshayafanya mapenzi ya Baba? NDIYO / HAPANA



Tafuta Ukweli

KUHUSU MUUMBAJI



Sura ya 2

Kama tunavyoangalia ulimwengu, dunia, na mwili wa ajabu wa mwanadamu, ni rahisi kuhitimisha kwamba hivi vitu havikutokea kwa bahati mbaya. Kwa hakika ni matokeo ya Muumbaji mwenye akili. Lakini ni Muumbaji wa aina gani? Je, ni kitu gani kwa kweli tunachokifahamu kuhusiana naye? Je, kwa hakika hujali uumbaji wake? Je, tunaweza kumfahamu? Na je, ni wapi tunaweza kwenda kuyapata majibu ya maswali hayo?

UTANGULIZI

Maisha ni uchunguzi wa majibu. Majibu ya *kweli* yanayoonesha hatima yetu ya milele ndiyo ambayo tunayathamini zaidi. Katika kuyatafuta haya majibu, inaonekana kwamba labda sehemu muhimu ya kuanzia safari kama hiyo itakuwa ni kuchunguza nyumba yetu – sayari dunia – ambapo uumbaji wa Mungu unaonekana bayana. Huwa ninafurahia kutembea katika misitu au kusafiri katika nchi – mbali na barabara zisizo na msongamano na maeneo ya masokoni. Kuwa pale hunikumbusha kuhusu mkono wa Mungu wenye nguvu. Lakini, Je, hapa ndipo pale tunapokutana na Mungu? Je, kwenye asili ndipo tunapompata Mungu? Katika kuutafuta kwetu ukweli, Hebu na tujiulize maswali matatu ya muhimu.

1. Je, asili inatueleza nini kuhusu Mungu?
2. Je, tunaweza kuifahamu nia ya Mungu?
3. Je, Biblia inatueleza nini kuhusu Mungu?

Hebu tuchunguze kila moja ya maswali haya.

JE, ASILI INATUELEZA NINI KUHUSU MUNGU?

Kwa karne nyingi, wanafalsafa wengi, wanasayansi na wananatheologia wameutambua uwepo wa Mungu. Utambuzi wao, kwa sehemu, ulikuwa unategemea ushahidi wa Mungu katika asili. William Paley, mwanatheologia wa karne ya kumi na nane, alifahamika sana kwa ajili ya kubisha kwake kuhusu uwepo wa Mungu kwa kutegemea asili.



Kazi za asili zinahitajika kutafakariwa tu. Wakati inapotafakariwa, zina vitu ndani yake ambavyo vinaweza kushangaza sana kwa ukuu wake kwa ajili ya ukubwa wa eneo letu la kugawanya, ambalo kupitia uchunguzi wetu unapotupeleka, tunaona nguvu ya ajabu. Kila kitu chochote kilichopangiliwa,

katika kiasi cha vitu vinavyotolewa na vinavyoendelea kutolewa, vinashuhudia kujali kwa upande wa Muumbaji. Tumezungukwa pande zote na vitu hivyo, vikichunguzwa katika sehemu zao, udadisi wa ajabu, vikilinganishwa kimoja na kingine, hakuna tofauti ya ajabu. Hakuna somo

ambalo, katika ukamilifu wake, upana wake ni mkubwa sana, Kama ile ya historia ya asili inavyotumika katika kumthibitisha Muumbaji mwenye akili. (*Theologi Asili*).

Ni kweli: Mungu amejidhihirisha nafsi yake katika asili – ukweli ambao Biblia pia inathibitisha kwa uwazi kabisa. Soma kile ambacho mtume Paulo alikiandika alipokuwa akiutambua ushahidi wa uwepo wa Mungu katika asili.

Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake, yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake, hata wasiwe na udhuru (Warumi 1:20)

Kutoka katika mstari huu, tunajifunza kwamba mwanadamu hana udhuru kwa *kutokumwamini* Mungu Mungu amejidhihirisha waziwazi duniani. Kama tunavyoichunguza dunia, ulimwengu na hata miili yetu wenyewe, tutakuja kuona kwamba hivi vyote ni ushahidi wa Muumbaji. Lakini hebu tuangalie mwanasayansi anasemaje kuhusu hili:

Huwezi kuwa na shairi bila kuwa na mshairi, au nyumba bila mjenzi. Huwezi kuwa na ubunifu bila kuwa na Mbunifu mwenye akili, Utata wa chembe, utata wa hali ya hewa ya dunia, umbali kati ya sayari – kila kitu kiliwekwa hapa kwa makusudi. Kama tukiangalia mfumo ufahamu wa mwanadamu, kwa mfano, tunaona kwamba unaundwa na mabilioni ya chembe, na umeandaliwa kwa makusudi kuwa na uwezo wa kusafirisha Hisia kutoka sehemu moja ya mwili



Kuhusu Muumbaji

kwenda sehemu nyingine. Katika hatua ya darubini, tunaona kwamba chembe moja ina mlango wa mifereji ya ioni, milango ya mifereji ya volti na utando wenye nguvu zisizodhihirika. Ulibuniwa mahsusi kufanya kitu kimoja – kubeba msukumo wa hisia kutoka kwenye chembe moja kwenda kwa nyingine. Unapoangalia kwa undani, ndani ya chembe, utapata DNA – kanuni za kibaiologia za uzima ambazo huruhusu chembe kujiendeleza yenyewe. Ndani ya chembe, kunamchanganyiko wa ajabu wa kanuni za kibaiologia, na bado tunatarajia kuamini kwamba “Ilitokea tu, kwa nasibu”? Tena na tena, kwa kadiri unavyoangalia katika asili yote, unaona kile ambacho ni kama “mshale wa neon” unaoelekea kwa Muumbaji, Mbunifu mwenye akili. Huyu mbunifu ni Mungu.

Brad Harrub, PhD.
Mtaalamu wa nyurolojia.

Mungu, ingelionekana, anatupigia kelele kwa vitendo kupitia ulimwengu unaotuzunguka, kwa kusema, “*Niko hapa, Mimi*

niko” Lakini ulimwengu unaotuzunguka unatufunulia nini kumhusu yeye? Unatueleza kwamba yeye anaakili, mhandisi mkuu ambaye anauwezo wa kuumba na kuutimizia huu ulimwengu usioelezeka kirahisi. Unatueleza kwamba yeye ndiye Muumbaji wa viumbe vya kushangaza na ubunifu wa mfumo wa kutatanisha. Unatueleza kwamba yeye ni mkuu zaidi na ananguvu zaidi kuliko nguvu yoyote tunayoweza kuifikiri.

Hata hivyo, kama tunavyoweza kuwa tumeshangazwa kwa huu uumbaji wa ajabu, hatuwezi kuifahamu nia ya Mungu kwa kuutazama mti – au asili katika njia yoyote. Si wezi kujua kama Mungu ananipenda. Siwezi kujua kama kuna mbingu au jahanamu. Siwezi kujua ninapaswa kufanya nini ili niweze kuokolewa kwa kuangalia tu ardhi chini ya miguu yangu. Iweje sasa, Je, ninaifahamu nia ya Mungu? Je, ninawezaje kuyajua mapenzi yake kwangu? Na Je, ninawezaje kujua kipi ninapaswa kukifanya ili niokolewe?

SEHEMU YA MARUDIO: JE, ASILI INATUELEZA NINI KUHUSU MUNGU?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Hoja ya William Paley kuhusu uwepo wa Mungu inategemea ushahidi wa Mungu unaopatikana katika _____.
2. Kulingana na Warumi 1: 20, watu ambao wamekataa kumwamini Mungu hawana _____ kwa sababu Mungu ametupatia ushahidi wa kutosha wa uwepo wake.
3. Kama kuna ubunifu wa kitu fulani basi ni lazima kuwepo na _____.
4. Ushahidi unaotuzunguka katika asili unatueleza kwamba Mungu ni _____ mwenye akili ambaye ana uwezo wa kuumba na kuutimizia huu ulimwengu wenye mambo mengi.
5. Wanadamu hawawezi kuijua nia ya Mungu kwa kuangalia _____ -au _____ katika aina yoyote.
6. Kwa kuangalia ushahidi wa Mungu katika asili, Je, tunaweza kuyafahamu mapenzi ya Mungu katika maisha yetu? NDIYO/ HAPANA
7. Kwa kuiangalia asili, Je, tunaweza kujua kwamba mbingu au jahanamu vipo? NDIYO / HAPANA.

Sura ya 2

8. Je, mtu anaweza kujua kipi cha kufanya ili aokolewe kwa kuyaangalia majani, miamba, miti, n.k? NDIYO / HAPANA.

Sehemu ya Majibu kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA inapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Kulingana na mstari hapo chini, Je, unapaswa kumwamini Mungu ili uweze kuokolewa? NDIYO / HAPANA.

Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao. (Waebrania 11:6)

- B. Je, unamwamini Mungu? NDIYO/ HAPANA

MASUALA YA KUZUNGUMZA

- A. Je, ni kwa jinsi gani vitu kama utata wa chembe, au utata wa ulimwengu vinatoa ushahidi wa uwepo wa Mungu?
- B. Je, ni kwa nini wanadamu *hawawezi* kuelewa yote wanayohitajika kuyafahamu kuhusu Mungu kwa kuangalia tu vitu vinavyowazunguka katika asili?



JE, TUNaweza KUFAHAMU NIA YA MUNGU?

Kwenye Biblia, mtume Paulo alilizingumzia suala hilo hilo:

Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu. Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. Na twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho ... (I Wakorintho 2:11-13)

Kutoka katika kifungu hiki tunajifunza kwamba mwanadamu, yeye mwenyewe, hana uwezo wa kuifahamu nia ya Mungu. Kwa maneno mengine, hatuwezi kuijua nia ya Mungu kwa kuangalia tu katika ulimwengu unaotuzunguka au kwa kuchunguza ndani ya nafsi zetu.

Pili, tunajifunza kwamba Mungu aliidhihirisha nia yake kwa njia ya Roho Mtakatifu. Roho aliwafunulia wanadamu

kile ambacho mwanadamu, yeye peke yake, asingeweza kukifahamu.

Tatu, tunajifunza kwamba ufunuo wa nia ya Mungu unawezekana kwa kupitia mafundisho ya Roho. Tunafikia kuifahamu nia ya Mungu, si kwa kupitia hisia ambazo tunazo katika mioyo yetu, lakini kupitia kile ambacho Roho hufundisha katika maneno. Hayo maneno yanapatikana kwenye Biblia. Biblia ni nia ya Mungu iliyodhihirishwa kupitia Roho Mtakatifu. Hufahamika kama “Maandiko”. Hebu tuangalie kile Biblia inachozungumza kuhusu asili na dhumuni la maandiko.

Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema. (2 Timotheo 3:16-17)

Maandiko, Paulo anasema, huja kwa uvuvio. Katika kifungu hiki, neno “Pumzi” kihalisia linamaanisha “Pumzi ya Mungu”

Kuhusu Muumbaji

Unapoiendea lugha ya Kiyunani, ambayo ndiyo ilitumika katika kuliandika Agano Jipya, utagundua kwamba neno ni *theopneustos*, ambalo ni neno lililounganishwa. Sehemu ya kwanza inamaanisha “Mungu” wakati sehemu ya pili inamaanisha “pumzi”. Hivyo basi, Paulo anasema kwamba maandiko yote ni pumzi halisi “liyopumuliwa na Mungu”

Chuck Homer
Mkufunzi na mhudumu wa Biblia.

Kwa maneno mengine, kama vile Mungu alivyompulizia mwanadamu na akafanyika kuwa nafsi hai, Mungu alipulizia ujumbe ambao tunauita “Biblia” uhai. Biblia i hai na inatenda kazi. Hatuna maandishi mfu. Tunao ujumbe ulio hai ambao umetoka moja kwa moja katika nia ya Mungu.

Keith Mosher Sr.
Mkufunzi na Mhudumu wa Biblia.

Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu, bali

wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, waki-ongozwa na Roho Mtakatifu (2 Petro 1:20-21)

Hivyo, tunaweza kuona kwa dhahiri kwamba Biblia haikutokana na mwanadamu. Biblia imetokana na Roho Mtakatifu. Ni nia ya Mungu. Hivyo basi, tunaweza kuiendea Biblia ili kujifunza ukweli kuhusu Mungu. Hebu na tujibu basi, swali kuu la tatu: “Je, Biblia inatueleza nini kuhusu Mungu?”



SEHEMU YA MARUDIO: JE, TUNAWEZAJE KUFAHAMU NIA YA MUNGU?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kando ya Biblia, Je, mwanadamu anaweza kuifahamu nia ya Mungu? NDIYO / HAPANA
2. Je, mtu anaweza kujua nia ya Mungu kwa kupitia “hisia” ndani ya moyo? NDIYO / HAPANA
3. Biblia inaifunua nia ya Mungu na inafahamika kupitia Roho wa Mungu. Biblia pia hufahamika kama _____.
4. Kulingana na 2 Timotheo 3: 16-17, Je, maandiko yote yana pumzi ya Mungu? NDIYO / HAPANA.
5. Ni kwa kupitia _____ tu, ndipo tunapoweza kuifahamu nia ya Mungu.
6. Neno la Kiswahili “pumzi” linatokana na maneno ya Kiyunani ambayo humaanisha _____.
7. Biblia ni matokeo ya _____

Sura ya 2

8. Je, 2 Petro 1:20-21 inafundisha kwamba maandiko (Biblia) ni matokeo ya nia ya mwanadamu pekee? NDIYO / HAPANA

Sehemu ya Majibu kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA inapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASWALA YA MAAMUZI

- A. Je, unaamini kwamba Biblia ni neno la Mungu lililovuviwa? NDIYO/ HAPANA.
B. Je, unatafuta kwa haka kulielewa neno la Mungu? NDIYO / HAPANA.

MASUALA YA KUZUNGUMZA

- A. Jadili sifa mbalimbali za Biblia ambazo zinathibitisha kwamba haiwezi kuwa ni matokeo ya nia/ akili ya wanadamu.
B. Je, ni kwa nini Mungu alihitaji kumpatia mwanadamu neno lake na mawazo yake katika njia ya *maandishi*?



JE, BIBLIA INATUELEZA NINI KUHUSU MUNGU?

Ili kujibu hili swali, hebu tuichunguze kauli iliyosemwa na mtume Paulo katika eneo litwalo Mlima wa Kuabudia, ambao ulikuwa ukipatikana ndani ya Athene, Ugiriki. Hiyo hotuba inapatikana katika sura ya kumi na saba ya kitabu cha Mdo. Kwa kuanzia, hebu tuiweke hiyo historia katika mazingira yake yanayozungumziwa.

Baada ya Paulo kuongolewa kwa Kristo, haikuchukua muda kabla hajaanza kuisambaza Injili (“Habari njema”) ya Kristo. Kama alivyokuwa akisafiri kwenye miji kama Likia, Filipi na Thessalonike, alitumia muda wake kuwaeleza wengine kuhusu Yesu na ufalme wa Mungu.

Hata hivyo, wakati alipofika Athene, alikutana na mji ambao ulikuwa umezama kabisa katika ibada ya sanamu. Watu wa Athene walikuwa ni wa kidini sana – washika dini na wachawi sana kiasi cha kuisimamisha madhabahu yenye maelezo yanayosomeka: KWA MUNGU ASIYEJULIKANA”. Labda walihofia uwezekano wa kumkwaza mungu fulani wasiye mfahamu, ndipo wakaisimamisha madhabahu hii kwa hesima ya huyu Mungu ambaye hawajui chochote kumhusu yeye.

Paulo pia alikutana na wanafalsafa mbalimbali na wasomi wa siku zake, Athene ilifahamika sana

kwa wanafalsafa wake, pamoja na msisitizo wake kwenye siasa, fasihi na kujifunza. Lakini bado, Paulo alipokuwa amesimama kwenye Mlima wa Ibada (ambako mahakama ya kidini na maadili ilipokuwa ikiendeshwa mara kwa

mara), alieleza kwamba Muumbaji wa kweli wa Ulimwengu alikuwa *anavutiwa sana*, na kujihusisha sana na mambo ya wanadamu. Hebu sasa na tusome kile ambacho Paulo aliwafunulia watu wa Athene kuhusu Mungu ambaye wanamwita “Mungu asiyejulikana”.

... watu wa Athene, katika mambo yote naona ya kuwa ninyi ni watu wa kutafakari sana mambo ya dini. Kwa sababu nilipokuwa nikipita huko na huko na kuyaona mambo ya ibada yenu, naliona madhabahu iliyoandikwa maneno haya, KWA MUNGU ASIYE JULIKANA. Basi mimi nawahubirini habari zake yeye ambaye ninyi mnamwabudu bila kumjua. Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono, wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu chochote, kwa maana ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote. Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae katika uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao (Mdo 17:22-26)

Kama tunavyojaribu kulijibu swali, “Je, Biblia inatueleza nini kuhusu Mungu?” tunajifunza mambo matatu kutoka katika mahubiri ya Paulo.

Kuhusu Muumbaji

1. Mungu ndiye Muumba wa vitu vyote.

Mungu aliufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo. Kuelezea kwamba huu uumbaji wa ajibu na huu ulimwengu usioelezeka kwamba vimetokea tu kawaida, ni jambo ambalo si la kufikirika. Katika siku za Paulo, imani kwamba Mungu yupo ilikuwa inafahamika sana na ilikuwa ina msingi sana. Lakini bado, kama Paulo alivyoonesha, kuna *Mungu mmoja tu* ambaye ameviumba vitu vyote. Hata hivyo, kama Paulo alivyoeleza baadaye katika hotuba yake, Hatupaswi kumwabudu Mungu kwa ujinga. Hatupaswi kuwa kama wale watu wa Athene ambao walimwabudu Mungu bure, kulingana na matakwa ya dhamiri zao wenyewe. Paulo aliwafunulia kwamba Mungu ni mtawala wa dunia mwenye nguvu, na kwamba yeye ndiye muumba wa vitu vyote. Kutokana na kwamba yeye ndiye muumba wa vitu vyote, tunapaswa kumwabudu yeye kulingana na matakwa ya mapenzi yake. Hatupaswi kumwabudu Mungu kwa ujinga.

2. Mungu huwafikia watu wote.

Hebu tuangalie kutoka katika kifungu cha Mdo 17 kwamba Mungu huwafikia wote. Soma kile Paulo alichokisema alipokuwa akiendelea na hotuba yake.

Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao, ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa papasa, wakamwone, ijapoku-

wa hawi mbali na kila mmoja wetu. Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu. Kama vile mmoja wenu, mtunga mas-hairi alivyosema, Maana sisi sote tu wazao wake. Basi, kwa kuwa sisi tu wazo wa Mungu, haitupasi kudhani ya kuwa Uungu ni mfano wa dhahabu au fedha au jiwe, vitu vilivyochongwa kwa ustadi na akili za wanadamu (Mdo 17:26-29)

Hayo maneno kutoka wa mtume Paulo yanafaraji sana, kwa sababu yanatufunulia kwamba Mungu anajihusisha na uumbaji wake. Ameweka mipaka ya makazi ya mwanadamu, na amekuwa akihusika katika masuala ya wanadamu na katika kukua na kuanguka kwa mataifa. Hata sasa, mambo mabaya yanayotutokea katika maisha haya yanaweza yakatumika kama lengo – kutukumbusha kumtafuta Mungu.

Tunapompata Mungu, tunatambua kwamba yeye si kama miungu ya upagani. Yeye yuko tofauti kabisa na hiyo miungu. Huyu Mungu mmoja aliye hai hatengenezwi kwa mawe au dhahabu, na habadiliki kwa mitindo kupitia njia za mwanadamu. Hakai katika hema zilizofanywa kwa mikono ya wanadamu. Mungu mmoja aishiye ni roho. Ana nafsi. Mungu mmoja wa kweli aishiye anajihusisha na mambo ya wanadamu.

Yeye ndiye anayetujali. Anatutimizia, Yeye ndiye anayetutimizia mahitaji yetu, ya kimwili na ya kiroho. Hunyesha mvua yake kwa wema na wabaya. Alimtuma mwanawe afe kwa ajili ya wote wasio haki, ili kwamba tufanyike kuwa



Sura ya 2

watoto Wake. Kuwa na uwezo wa kwenda na kuishi naye milele kwenye nyumba yake ni zaidi ya uwezo wetu wa kuelewa. Neno “Baba” huleta katika akili zetu dhana ya familia yenye upendo.

**B.J. Clark
Mhudumu**

Katika 1 Yohana 4:8, mtume Yohana alisema kwamba, “Mungu ni pendo” Si tu kwama yeye ni pendo, lakini kulingana na Biblia yeye pia ni Baba yetu. Kama Baba, anatamani kuwa na uhusiano na wale aliowaumba. Kwa hakika, Mungu anatutaka sisi tumpende. Sisi pia hutamani kupendwa. Kila mmoja wetu hutamani kuwa mali ya mtu fulani. Kila mmoja wetu hutamani uhusiano. Mungu wa kwenye Biblia anaweza kutupatia huo.

Mwanadamu, katika miaka yote, ametafuta kuwa mali ya mtu mwingine” wakati watu walipoujenga mnara wa Babeli, walitafuta kujitengenezea jina, na waliungana pamoja kwa sababu ya lengo la kimwili. Katika zama zingine katika historia, watu waliutafuta upendo ambao ulikuwa umepotea katika maisha yao. Waliviacha vitu vizuri ambavyo vilikuwa ni sawa kwao. Walikuwa na uhusiano sahihi na marafiki na familia zao, halafu bado wakatafuta vitu vingine ambavyo havikuwa sahihi. Kuwa na afya ya akili leo ni kuwa na vyanzo vingi kwa ajili ya watu kutumia wanapoutafuta huu “upendo uliopotea” katika maisha yao. Watu huwaendea washauri, wanaaikolojia na wataalamu wa magojwa ya akili kila siku. Huwafuata nchi nzima, wakitafuta majibu ya kuepuka kwa hila. Lakini bado, majibu wanayoyatafuta hata hivyo ni sahihi mbele zao. Mungu ameutoa upendo kwa mwanadamu. Ametoa nafasi kwetu sisi kukua na kuwa na nguvu, lakini bado wakati mwingine tunalipuuzia hilo. Kile ambacho tunapaswa kukifanya ni kutambua kwamba Mungu amemtoa mwanawe wa pekee ili sisi tupate kuishi. Ingawa tunaweza kupata misaada kutoka katika vyanzo vingine, Kile ambacho tunapaswa kukifanya kwa hakika ni kuirejea Biblia. Tunapaswa kujifunza, kwa sababu inaelezea upendo mkuu ambao Mungu ametupa. Hakuna hitaji la kutafuta zaidi, kwa sababu majibu yako mbele yetu.

**Dr. Stephen Springer
Mtaalamu mshauri mwenye leseni
na Profesa wa Chuo Kikuu**

Ndiyo, Mungu kwa hakika anatupenda. Anatujali kwa undani sana. Anaitambua huzuni yetu na maumivu ya mioyo yetu. Yeye hutufikia kila mmoja wetu. Kama mtume Paulo alivyosema, kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda na kuwa na uhai wetu. Kwa maneno mengine, ni katika Mungu tunapopata sababu/ dhumuni la kuwepo kwetu.

Hebu tusiangalie tu kwamba Mungu ni Muumba wa wote, na kwamba humfikia kila mmoja wetu, lakini pia Mungu hutaka kumpa kila mtu wokovu.

3. Mungu hutoa wokovu kwa wote.

Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni, bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu. Kwa maana ameweka siku atakayo wahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua, naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufu katika wafu (Mdo 17:30-31).

Siku moja Mungu atauhukumu ulimwengu. Kwa sababu atauhukumu ulimwengu, ameitengeneza njia ili kila mtu apate kuokoka. Kwa hakika, *Mungu anataka kila mtu aokolewe*. Hivyo, ametupatia sisi sote fursa sawa ili tuweze kuokolewa kwa njia ya ufufuko wa mwanawe, Yesu.

Kitu kimoja ambacho tunahitajika kukielewa ni kwamba, Mungu huwapenda wadhambi wote – kila mtu, kila mahali, bila kujali kile walichokifanya. Si ukubwa wala wingi wa dhambi zetu utakuwa ni kikwazo cha wokovu wetu. Hata “mtenda dhambi mkuu” (kama Paulo alivyojielezea yeye mwenyewe) aliipokea neema ya Mungu. Katika I Wakorintho 15:10, alisema, “kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo” Paulo alishafanya uharibifu mwingi kwenye Kanisa, lakini bado Yesu alimsamehe.

**B.J. Clarke
Mhudumu**



Kuhusu Muumbaji

Bwana atamsamehe kila mmoja ambaye atamgeukia kwa hakika. Tunasoma katika 2 Petro 3:9, “Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyodhania kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba”.

Garland Elkins
Mkufunzi na mhudumu wa Biblia.

Mungu hayupo tayari mtu *ye yote* apotee. Anamtaka *kila mmoja* afikilie toba. Kulingana na Yohana 3:16, Mungu alipenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa pekee afe ili kwamba mimi na wewe tusiteseke katika adhabu ya milele. Mungu anataka kila mmoja aokolewe.

Ili hali Mungu anataka kila mmoja aokolewe, Mungu anatarajia kitu fulani kama malipo.

Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni, bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu (Mdo 17:30)

Je, umekiona kile Mungu anachokitarajia? Kulingana na mtume Paulo, Mungu anatutaka wote tutubu. Soma kile Yesu alichokisema kuhusu hili katika Injili kulingana na Luka:

Nawaambia, sivyo, lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo (Luka 13:3)

Hitimisho ni kwamba, toba ni badiliko la moyo na nia. Wakati mtu anapotubu kwa kubadilisha moyo na nia yake kuhusu dhambi, na kugeuka kwa kufanya kile kilichoamriwa na Mungu, Huyu mtu ameifikilia toba.

Alfred Washington
Mhudumu

Toba ni uamuzi wa nia/ akili ambayo husema, “Mungu ameniambia nifanye hili, na kama sitalifanya, Ninatenda dhambi dhidi ya Mungu. Mungu alimtuma mwanawe kwa ajili yangu. Ananipenda. Ninajua ninamuumiza kama situbu. Hivyo, nitabadilisha jinsi ninavyofikiri na nitafanya chochote kile Mungu atakacho niambia nifanye” Hiyo ndiyo sababu ya toba kuwa ni amri ngumu. Mtu anapaswa kusema, “Sizifuati njia zungu mwenyewe tena. Nitafanya kile Mungu atakacho niambia nifanye” Toba ni badiliko la akili/nia linalotegemea huzuni ya namna ya Mungu.

Keith Mosher Sr.
Mkufunzi na mhudumu wa Biblia.

Toba hutarajiwa kwa watu wote. Haijalisha kwamba ni matajiri au masikini, wasomi au wasiowasomi. Haijalishi kwamba ni wapi mtu amezaliwa. Haijalishi kwamba wazazi wetu walikuwa ni akina nani, au watoto wetu siku moja watakuwa ni akina nani. Mungu humtarajia *kila mmoja* atubu.

Lakini, Je ni *kwa nini* toba ni ya muhimu? Je, ni *kwa nini* Mungu anatuita wewe na mimi tutubu?

Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki ... (Mdo 17:31)

kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiriri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya. Basi tukijua hofu ya Bwana, twawavuta wanadamu ... (2 Wakorintho 5:10-11)

Hivyo, toba ni ya muhimu kwa sababu Mungu atawahukumu ulimwengu siku moja. Kila mmoja wetu atawajibishwa kwa kile alichokifanya, pamoja na kile alichoshindwa kukifanya. Mungu anatarajia tutubu. Anatarajia tugeuke kutoka katika njia na fikra potofu. Na kama hatutafanya hivyo, *tutateseka* kwenye hukumu ya Mungu. *Tutateseka* ghadhabu na hasira yake.

Unaweza ukawa unajiuliza, “Kama Mungu anataka kumuokoa kila mtu, Je, ni *kwa nini* awaadhibu wale wasio tubu?” Jibu ni kwa sababu Mungu ni wa haki (Ufunuo 15:3) na asiye na upendeleo (Warumi 2:5). Kwa sababu yeye ni wa haki, ni lazima aadhibu utendaji wa makosa. Kwa sababu yeye hana upendeleo, ni lazima awanidhamishe wale ambao ni wakaidi. Hebu mfikirie, kwa mfano, hakimu kwenye jamii yako ambaye anakataa kumwadhibu mhalifu mwenye hatia. Je, ungelimchukulia huyu hakimu kwamba ni mwenye haki na hana upendeleo? Je, hungetarajia (na kwa hakika kudai!) kwamba hakimu huwahukumu wale wasioishika sheria? Katika hali inayofanana, Mungu, hakimu wa ulimwengu wote (Mwanzo 18:25), atawahukumu wale ambao hawakuzishika sheria zake? Mungu, kama



Sura ya 2

Mungu mwenye haki, anataka kila mtu aokolewe. Lakini pia atawahukumu wale wasiotubu. Iangalie hukumu, kama inavyoelezewa na mtume Yohana.

Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesi-mama mbele ya hicho kiti cha enzi, na vitabu vikafunguliwa, na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni kitabu cha uzima, na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao, (Ufunuo 20:12)

Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. Warumi 14:11-12 na 2 Wakorintho 5:10 zote zinaeleza kwamba tutahukumiwa “kulingana na matendo yetu” Hili linasababisha hukumu iwe ya kutisha sana.

Curtis Cates
Mkufunzi na mhudumu wa Biblia.

Sisi wote tutakuwepo kwenye hukumu. Hilo linakujumuiisha na wewe. Siku moja utasimama mbele za Mungu na

kutoa habari ya vitu ulivyovifanya hapa duniani. Kama ulitubu na kumgeukia Mungu, utaokolewa na kuishi milele. Tunaweza kuokolewa kwa nguvu za Mungu na ufufuko wa Yesu Kristo kutoka katika wafu.

Katika kuutafuta kwetu ukweli, hebu tuangalie vitu vitatu ambavyo tumejifunza:

1. **Hatuwezi kuifahamu nia ya Mungu kwa kuangalia uumbaji.** Ili hali uumbaji unaotuzunguka kwa hakika unatoa ushahidi madhubuti kwamba Mungu yupo, hatuwezi kuifahamu nia yake kwa kuuangalia uumbaji tu.
2. **Mungu amejifunua kwetu kupitia Roho Mtakatifu.** Mungu ameidhihirisha nia yake kwa njia ya neno lili-loandikwa – Biblia.
3. **Biblia inatueleza kwamba Mungu ndiye muumba wa vyote, na kwamba yeye huwafikia watu wote, na hutaka kuwaokoa watu wote.**

SEHEMU YA MARUDIO: JE, BIBLIA HUTUELEZA NINI KUHUSU MUNGU?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Neno “Injili” linamaanisha _____
2. Kulingana na Mdo 17:22-26, Je, Mungu ni Bwana wa mbingu na nchi? NDIYO/HAPANA
3. Kulingana na Mdo 17:24, Je, Mungu aliyehai anakaa katika mahekalu yaliyotengenezwa kwa mikono? NDIYO / HAPANA
4. Kulingana na Mdo 17:30-31, kila mtu anapaswa _____.
5. Kulingana na Mdo 17:27, Mungu ni _____ kwa ye yote kati yetu.
6. Kulingana na mstari hapo chini, mtume Yohana alisema kwamba “Mungu ni _____”

Yeye asiyepeleka, hamjui Mungu, kwa maana Mungu ni upendo (I Yohana 4:8)

7. Yesu alisema katika Luka 13:3 kwamba watu wasipo _____, wataangamia.
8. Kulingana na mstari hapo chini, Je, Mungu anakupenda? NDIYO/HAPANA.

Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwangu, hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele (Yohana 3:16).

Kuhusu Muumbaji

9. Je, Bwana anataka wewe upotee? NDIYO/ HAPANA

10. Je, mstari hapo chini unaeleza kwamba Mungu ni Mungu wa *haki*? NDIYO/ HAPANA.

Nao wauimba wimbo wa Musa, mtumwa wa Mungu, na wimbo wa Mwana Kondoo, wakisema, Ni mkuu, na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi, ni za haki, na za kweli njia zako, Ee Mfalme wa mataifa (Ufunuo 15:3)

11. Je, hakimu wa kidunia anaweza kuwa wa haki kama akikataa kumwadhibu mhalifu mwenye hatia? NDIYO/HAPANA

12. Kulingana na Ufunuo 20:12, watu wote siku moja watahukumiwa kulingana na matendo yao. Je, hilo linakuhusisha wewe? NDIYO/HAPANA

Sehemu ya Majibu kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA inapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

A. Je, umeshawahi kumwabudu Mungu bure au kwa ujinga? NDIYO / HAPANA

B. Kama wakati fulani katika darasa hili uligundua kwamba ulikuwa unamwabudu Mungu bure, Je, utatubu? NDIYO / HAPANA

C. Je, uko tayari wakati huu kusimama mbele za Mungu kutoa habari ya matendo yako? NDIYO / HAPANA.

MASUALA YA MAZUNGUMZO

A. Je, ni kwa nini ni lazima Mungu awaadhibu watu ambao ni watenda dhambi na ambao hawajazitubia dhambi zao?

B. Kulingana na 2 Petro 3:9, Mungu “huvumilia”. Hiyo inamaanisha nini?



HITIMISHO

Mungu anataka kukuokoa wewe. Muumba mkuu wa ulimwengu huu anakupenda na anakutaka uyatii mapenzi yake.

Je, *utaitikia* mapenzi yake? Katika siku za Paulo, baadhi waliukataa ukweli kuhusu Muumba. Hawakutubia dhambi zao, wakati walipokabiliwa na kile kilicho kweli.

Lakini vipi kuhusu *wewe*? Vipi kama, katika kuutafuta uk-

weli, umegundua kwamba kile ulichokuwa unafundishwa au kile unachokiamini sasa, ni kinyume na kile Biblia inachokifundisha? Je, utageuka? Je, utabadilika? Je, utafanya vitu katika njia ya Mungu? Katika safari yetu – kuutafuta kwetu ukweli – Ninatumaini kwamba utajichunguza ili uone kama kwa hakika upo kwenye imani au la. Yesu alisema, “tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru” (Yohana 8:32)

Sura ya 2

MARUDIO YA SURA

Majibu ya maswali yafuatayo yanaweza kupatikana ndani ya sura hii.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na Warumi 1:20, Je, uwepo wa Mungu unaonekana dhahiri katika dunia? NDIYO / HAPANA
2. Kulingana na 2 Petro 1:20-21, Je, maandiko asili yake ni Mungu au mwanadamu? _____
3. Kulingana na 2 Wakorintho 5:10, kila mtu atasimama mbele ya kiti cha _____ cha Kristo.
4. Kulingana na Yohana 3:16 na 2 Petro 3:9, Je, Mungu anataka kila mtu aokolewe? NDIYO / HAPANA

MASWALI YA KUTILIA MKAZO

1. Je, Biblia ni matokeo tu ya akili/nia ya wanadamu? NDIYO/HAPANA
2. Je, watu wanaweza wakafahamu mapenzi ya Mungu kwenye maisha yao kwa kile wanachojisikia tu kwenye mioyo yao? NDIYO / HAPANA
3. Je, Mungu atawaadhibu wale ambao hawazishiki amri zake? NDIYO / HAPANA.

Sehemu ya Majawabu kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA na MASWALI YA KUTILIA MKAZO yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

VITU UNAVYOPASWA KUVIJUA

- Mungu ndiye muumba wa vyote.
- Mwanadamu hawezi kujua nia/ akili ya Mungu kwa kuuangalia uumbaji unaomzunguka.
- Mwanadamu, yeye mwenyewe, hawezi kujua nia ya Mungu.

- Roho wa Mungu ameidhihirisha nia/akili ya Mungu kupitia mafundisho
- Mungu huwafikia watu wote.
- Mungu hutoa wokovu kwa wote.
- Mungu atawaadhibu wale ambao hawajatubu.

CHIMBA ZAIDI ...

Masomo hapo chini yamekusudiwa kwa wale ambao wangelipenda kujifunza somo hili kwa undani zaidi. Kuna taarifa ambazo hazikujadiliwa katika somo.



MUNGU NDIYE MUUMBA

Hapo mwanzo Mungu alizifanya mbingu na nchi (Mwanzo 1:1)

Nikiziangalia mbingu zako, kazi za vidole vyako, Mwezi na nyota ulizoziratibisha, Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, Na binadamu hata umwangelie?(Zaburi 8:3-4).

Mbingu za uhubiri utukufu wa Mungu, na anga laitangaza kazi ya mikono yake(Zaburi 19:1)

Jueni kwamba BWANA ndiye Mungu, Ndiye aliyetumba na sisi tu watu wake, tu watu wake, na kondoo wa malisho yake (Zaburi 100:3)

Mungu aliyefanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono (Mdo 17:24)

Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuu-pokea utukufu na heshima na uweza, kwa kuwa wewe ndiye uliyevumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa (Ufunuo 4:11).

VITU VYA KUFIKIRIA WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

1. Je, Mwanzo 1:1 inafundisha kwamba Mungu alizifanya mbingu na nchi? NDIYO/ HAPANA
2. Je, Zaburi 8:3-4 na 19:1 zinafundisha kwamba Mungu alizifanya mbingu na vitu vilivyomo? NDIYO / HAPANA
3. Kulingana na Zaburi 100:3, Je ni nani alitumba sisi?

Kuhusu Muumbaji

4. Mungu “aliyeufanya _____ na _____ ndani yake” (Mdo 17:24)

5. Kulingana na Ufunuo 4:11, Mungu aliviumba _____



MUNGU NI MWENYE MAARIFA (ANAJUA YOTE)

Kwa maana njia za mwanadamu zi mbele za macho ya Bwana, na mienendo yake yote huitafakari (Mithali 5:21)

Macho ya Bwana yako kila mahali, yakimchunguza mbaya na mwema (Mithali 15:3)

Kumbukeni mambo ya zamani za kale, maana mimi ni Mungu, wala hapana mwingine, mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi, nitangazaye mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado, nikisema, Shauri langu litasimama, nami nitatenda mapenzi yangu yote” (Isaya 46:9-10)

Akawaambia, “ninyi ndinyi mnaojidai haki mbele ya wanadamu, lakini Mungu awajua mioyo yenu, kwa kuwa lililotukuka kwa wanadamu, huwa chukizo mbele za Mungu” (Luka 16:15)

Kisha wakaomba, wakasema, Wewe, Bwana, ujuaye mioyo ya watu wote, tuonyeshe ni nani uliyemchagua katika hawa wawili” (Mdo 1:24)

Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu (Waebrania 4:13)

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI UNAPOCHIMBA ZAIDI

6. Je, Mithali 5:21 na 15:3 zinafundisha kwamba Mungu anajua kila kitu wakifanyacho wanadamu? NDIYO / HAPANA

7. Kulingana na Isaya 46:9-10, Je, Mungu anajua nini kitatokea hata kabla hakijatokea? NDIYO / HAPANA

8. Mungu anajua _____ ya kila mtu. (Luka 16:15 na Mdo 1:24).

9. Kulingana na Waebrania 4:13, _____ vi utupu na kufunuliwa machoni pa Mungu.

10. Kulingana na Waebrania 4:13, tunapaswa kutoa _____ kwa Mungu kwa ajili ya matendo yetu.



MUNGU NI MWENYE KUDURA (MWEYE NGUVU ZOTE)

Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuilika (Ayubu 42:2)

Kwa Neno la Bwana mbingu zilifanyika, Na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake. Hukusanya maji ya bahari chungu chungu, huviweka vilindi katika ghala. Nchi yote na imwogope BWANA, wote wakaao duni-ani na wamche. Maana yeye alisema, ikawa, na yeye aliamuru, ikasimama. (Zaburi 33:6-9)

Yesu akawakazia macho, akasema, “ kwa wanadamu haiwezekani, bali kwa Mungu sivyoyote, maana yote yawezekana kwa Mungu” (Marko 10:27)

Kwa maaana twafahamu yakuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana haviku-fanywa kwa vitu vilivyo dhahiri (Waebrania 11:3)

“Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, asema Bwana Mungu, aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi” (Ufunuo 1:8)

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

11. Ayubu alisema kwamba Mungu anaweza kufanya _____ (Ayubu 42:2).

12. Mungu ana nguvu sana kiasi kwamba “Yeye _____, na kilifanyika, Yeye _____, na ikasimama” (Zaburi 33:6-9).

13. “Kwa Mungu _____ yawezekana” (Marko 10:27).

14. Kulingana na Waebrania 11:3, Je, Mungu aliufanya ulimwengu kwa kutumia vitu vilivyo kuweko? NDIYO / HAPANA

15. Kulingana na Ufunuo 1:8, Bwana ni _____.



MUNGU ANAPATIKANA KILA MAHALI (KUWA KILA MAHALI)

Lakini Mungu je? Atakaa kweli kweli juu ya nchi? Tazama, mbingu hazikutoshi, wala mbingu za mbingu, sem-buse nyumba hii niliyojenga! (I Wafalme 8:27)

Niende wapi nijiepushe na roho yako? Niende wapi

Sura ya 2

nijiepushe na uso wako? Kama ningepanda mbinguni, wewe uko, Ningefanya kuzimu kitanda changu, Wewe uko, Ningezitwaa mbawa za asubuhi, Na kukaa pande za mwisho za bahari, Huko nako mkono wako utaniongoza, Na mkono wako wa kuume utanishika. (Zaburi 139:7-10)

Ombeni, nanyi mtapewa, tafuteni, nanyi mtaona, bisheni, nanyi mtafunguliwa, kwa maana kila aombaye hupokea, naye atafutaye huona, naye abishaye atafunguliwa. (Mathayo 7:7-8)

Ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa papasa, wakamwone, iwapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu (Mdo 17:27)

Ni nani atakeyetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? Kama ilivyoandikwa, ya kwamba, kwa ajili yako tutauawa mchana kutwa, Tumehesabiwa kuwa kama kondoo wa kuchinjwa. Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayo kuwepo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyochini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu. (Warumi 8:35-39)

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

16. Maelezo ya Selemani kwenye I Wafalme 8:27 yanatonesha kwamba Mungu yupo kila mahali kwa sababu mbingu na mbingu za mbingu _____ Mungu.
17. Zaburi 139:7 inafundisha kwamba hakuna mahali tunapoweza _____ kutoka katika uwepo wa Mungu.
18. Je, Mathayo 7:7-8 na Mdo 17:27 zinafundisha kwamba tunapomtafuta Mungu, tutampata? NDIYO / HAPANA.
19. Kulingana na Mdo 17:27, Je, Mungu yupo karibu na baadhi ya watu na kuwa mbali na watu wengine? NDIYO / HAPANA
20. Je, Warumi 8:35-39 inafundisha kwamba baadhi ya vitu fulani vinaweza kututenga sisi na upendo wa Mungu? NDIYO / HAPANA



MUNGU NI MWENYE HURUMA ZOTE (WEMA WOTE)

Ni huruma za BWANA kwamba hatuangamii, kwa kuwa rehema zake hazikomi. Ni mpya kila siku asubuhi, uaminifu wako ni mkuu. (Maombolezo 3:22-23)

Msisumbuke, basi, mkisema, Tule nini? Au Tunywe nini? Au tuvae nini? Kwa maana hayo yote mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa (Mathayo 6:31-33)

Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu, ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli (I Timotheo 2:3-4)

Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga, kwake hakuna kubadilika wala kivuli cha kugeuka-geuka (Yakobo 1:17)

Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyodhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba (2 Petro 3:9)

Yeye asiyependa, hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo (I Yohana 4:8)

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

21. “_____ zake hazikomi, ni mpya kila asubuhi” (Maombolezo 3:22-23)
22. Je, Mathayo 6:31 inafundisha kwamba Mungu atatupa-tia mahitaji yetu ya kimwili kama sisi ni wenye haki na tunaomtafuta yeye? NDIYO / HAPANA
23. Kulingana na Yakobo 1:17, kila _____ na kila _____ hutoka kwa Mungu.
24. Kulingana na I Timotheo 2:3-4 na 2 Petro 3:9, Je, Mungu anataka kila mtu aokolewe? NDIYO / HAPANA.
25. “Mungu ni _____” (I Yohana 4:8)

Sehemu ya Majibu kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA na MASWALI YA KUCHIMBA ZAIDI yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.



Tafuta Ukweli

KUHUSU MAMLAKA KWENYE DINI



Sura ya 3

Katika ulimwengu wa leo wa kidini, kunamjadala mkuu kuhusu kipi ni sahihi na kipi si sahihi. Inapofikia kwenye masuala ya imani, kunaidadi kubwa ya tofauti ya mitazamo. Lakini, ni upi ulio sahihi? Na ni nani anayeamua kipi ni sahihi? Je, ni nani anayetunga sheria? Je, ni nani au ni nini ambacho ndicho mamlaka ya mwisho kwenye masuala ya kidini? Je, ni Kanisa, Biblia, vitabu vya muongozo, au baraza la wasomi? Ni nani au ni nini, chenye mamlaka katika masuala ya kidini? Kwa maneno mengine, ni nani anayetunga sheria? Na je, ni wapi tunapoweza kupata majibu?

UTANGULIZI


Ili kujua sheria ni zipi, na ni wapi zinapatikana, kuna vitu viwili ambavyo kwa hakika ni muhimu kwa ajili ya kila jiti-hada. Katika uwanja wa mashindano ya riadha, kitabu cha sheria/ kanuni na mamlaka ni vya “lazima”. Wakati timu zinapokutana ili kushindana katika nyanja ya riadha, wana-fanya hivyo, wakiwa wamekubaliana na kitabu cha kanuni kilichoanzishwa kwamba imekubaliwa na kuthibitishwa kabla na mtu mwenye mamlaka au bodi. Kanuni ya kuwa na kifungu cha sheria au kifungu cha mamlaka ni kanuni in-ayokubalika mahali pote, iwe inahusiana na michezo, asasi za kiraia, shughuli za shule, kanisa, au taifa. Kila mmoja huelewa umuhimu na ulazima wa kuwa na mamlaka inayo-tambulika au kitabu kilichoanzishwa cha sheria.

Katika kila tukio la mchezo, ni lazima kuwepo na mam-laka inayotambulika na kanuni zilizoanzishwa. Bila kuwa na kitabu cha kanuni au bodi au mtu mwenye mamlaka, mchezo hautapaswa kucheza. Chukua kwa mfano, Mi-chezo ya Olimpiki ya majira ya joto ambayo huendeshwa kila baada ya miaka minne kwenye maeneo mbalimbali duniani kote. Hizo nchi na washiriki wake zinaweza zikafa-nana katika sare/unifomu na katika njia fulani, kushiriki katika michezo hiyo kwa sababu wote wamekubaliana katika umuhimu wa kuwa na kiwango kimoja cha mamlaka na kifungu kimoja cha sheria zitakazofuatwa. Kwa Michezo ya Olimpiki, hicho kiwango cha mamlaka kinasimami-wa na mamlaka kuu, inayofahamika kama Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki. Kazi ya kamati ni kuchagua kutoka miongoni mwa wajumbe wake, raisi na bodi ya utendaji sasa, wanaanzisha sheria na miongozo, na kumchagua mkurugenzi mkuu ili atoe msaada wa kuandika na kuzisimamia hizo kanuni. Kutoka katika huu mchakato, kitabu cha kanuni huanzishwa. Hiki kitabu cha kanuni ndi-po hufanyika kuwa maandishi ya mamlaka yanayoweka vikomo, sheria za kila mchezo, na ni kwa jinsi gani hiyo michezo itaamuliwa. Bila ngazi za mamlaka na kitabu cha kanuni, kutakuwa na kuchanganyikiwa na machafuko. Kukubaliana katika kiwango cha mamlaka na kitabu cha kanuni ni vitu vya “lazima” kabisa.”

Charles Smith
Mwamuzi

Sasa, hebu tugeuzie usikivu wetu kwenye kitu ambacho ni muhimu zaidi kuliko tukio lolote la kimichezo. Hebu tugeuzie usikivu wetu katika ulimwengu wa kidini, na kuji-uliza: “Je, kuna mamlaka moja katika dini? Je, kuna nyara-ka moja yenye mamlaka au kitabu cha kanuni katika dini?”

Mpango wa Mamlaka Ya Olimpiki



Kuhusu Mamlaka Kwenye Dini

Kama – katika kubainisha kanuni za kanisa, jinsi gani lili-vyopangiliwa, au ni namna gani ya kuabudu – mtu mmoja anakiendea kitabu cha mwongozo ili kupata mwongozo, na mwingine anayaendea maamuzi yaliyofanywa na makubaliano ya kujitoa, na bado kundi lingine hufanya maamuzi kulingana na kile “wanachokihisi katika mioyo yao,” hawa watu hawataweza kufikia aina yeyote ya makubaliano. Hawatakuwa na uwezo wa kucheza katika “kiwanja kimoja.”

Kama umoja na makubaliano yangetokea – na ukweli kamili kuhusu kipi cha kuamini, jinsi ya kuishi na jinsi ya kuabudu utapatikana – ndipo tutakapoanza kwa kuangalia ni yupi mwenye haki ya kuunda sheria na ni wapi hizo sheria zimeandikwa. Tukijua kipi ni kiwango chetu cha mamlaka, kitaathiri hatma ya umilele wetu! Kuutafuta ukweli kuhusu mamlaka kwenye dini, ndipo utakuwa na umuhimu zaidi. Hivyo basi, hebu tujiulize maswali manne ya msingi/muhimu:

1. Je, mamlaka ni nini?
2. Je, ni nani au ni nini ambacho ndicho mamlaka katika dini?
3. Je, haya mamlaka yalidhihirishwaje?
4. Je, leokuna kiwango zaidi ya kimoja cha mamlaka?



JE, MAMLAKA NI NINI?

Hebu tuanze kutafuta kwa kujiuliza, “Je, mamlaka ni nini?” Tumelitumia neno “mamlaka” mara kadhaa mpaka kufikia hapa, lakini, Je, linamaanisha nini? Kulingana na Kamusi ya English – Swahili ya (TUKI), neno “mamlaka” linamaanisha “haki au nguvu za kulazimisha utii, maadili au nguvu za kisheria, haki ya kuamuru au kupewa maamuzi ya mwisho.”

Mfano mzuri wa fafanuzi hii unapatikana kwenye Mathayo 8:9, ambapo akida wa Kirumi (ambaye alimwomba Yesu amponye mtumishi wake) alisema:

Kwa maana mimi nami ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu, nikimwambia huyu, nenda, huenda, na huyu, njoo, huja, na mtumwa wangu, fanya hivi, hufanya (Mathayo 8:9).

Hivyo, mamlaka, inahusisha haki ya kuamuru na nguvu ya kutunga sheria. Mzizi wa neno mamlaka ni “mtunzi”. Mtunzi ni “mtu anayeanzisha au kuunda kitu” (TUKI – English – Swahili Dictionary). Neno linamhusu mtu ambaye ni mwanzilishi au mbunifu wa kitu fulani. Hivyo neno “mamlaka” linaelezea moja au zaidi ya dhana zifuatazo:

- Haki au uwezo wa kuamuru au kutoa maamuzi ya mwisho.
- Haki au mamlaka ya kisheria
- Mwanzilishi au mwasisi wa kitu fulani.

Lakini vipi kuhusu mamlaka ya kidini? Kama tunavyoendelea na uchunguzi wetu wa kuutafuta ukweli kuhusu mamlaka katika dini, hebu tujiulize swali letu kuu la pili: “Je, ni nani au ni nini ambacho ndicho mamlaka katika dini?”

SEHEMU YA MARUDIO: JE, MAMLAKA NI NINI?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Takribani katika kila eneo katika maisha, ni muhimu kufahamu sheria ni zipi na _____, _____, _____.
2. Ni muhimu kuwa na kipimo, kutambua kitabu cha mwongozo (au mamlaka) katika michezo, vyama vya kijamii, vikundi vya shule, mataifa na kanisa? NDIYO/ HAPANA
3. Kulingana na kamusi ya TUKI – English – Swahili, neno “mamlaka” linamaanisha “haki au uwezo wa kusesitiza utii, haki au mamlaka ya kisheria, haki ya _____ au kutoa _____ ya mwisho”.

Sura ya 3

4. Je, mgawanyiko wa kidini upo miongoni mwa wale wanaodai kumfuata Kristo? NDIYO/ HAPANA.
5. Kulingana na mstari hapo chini, Je, Mungu anataka kuwe na migawanyiko miongoni mwa wafuasi wake? NDIYO / HAPANA

Basi ndugu, nawasihi, kwa jina lake Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja, wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja (I Wakorintho 1:10).

6. Kama umoja na makubaliano yanapaswa kuwepo miongoni mwa wafuasi wa Kristo, Je, hao wafuasi wanapaswa kukubaliana kwenye kiwango kimoja cha mamlaka (m.f. kukubaliana kuhusu kitabu kimoja cha sheria)? NDIYO / HAPANA.

SEHEMU YA MAJIBU kwa ajili ya **MASWALI YA KUJIFUNZIA** inapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Je, wewe uko tayari kudumu katika maelekezo ya Mungu kwamba watu wake “wote wanene mamoja” ili kwamba pasiwe na mgawanyiko katika kanisa la Bwana (I Wakorintho 1:10)? NDIYO / HAPANA
- B. Je, uko tayari kujinyenyekeza kwa Mungu na upanga wake, Biblia, kama mamlaka ya mwisho katika maisha yako? NDIYO / HAPANA.

MASUALA YA KUZUNGUMZA

- A. Je, ni kwa nini wachezaji, makocha na timu hawana haki ya kubadilisha au kufuta kutoka, au kuongeza katika kitabu cha kanuni/sheria?
- B. Katika kuangalia kanuni za kanisa na mpangilio wake, Je, ni nini kitatokea kama kundi moja litageukia kitabu cha mwongozo ili kupata mwongozo, kundi lingine limekifuata kile ambacho mkutano wa maamuzi umeamua kulingana na ni kitu gani “wanachojisikia kuwa ni sahihi katika mioyo yao?”



NI NANI, AU NI NINI AMBACHO NDICHO MAMLAKA KATIKA DINI?

Je, ni nani ana haki ya kutoa amri na kuunda sheria, zinazohusu jinsi tunavyopaswa kuishi maisha yetu, au jinsi ya kuabudu? Je, ni nani mwenye mamlaka ya mwisho ya kisheria kuhusiana na hivi vitu?

Mungu ndiye chanzo cha msingi cha dini na mamlaka ya haki. Wakati Yesu alipokuwa kwenye hukumu mbele ya Pilato na kukataa kujibu swali, Pilato alisema, “Nina haki ya kukuhukumu kifo” Yesu akasema, “hunauwezo huo hata kidogo, isipokuwa umepewa kutoka juu,” ambayo inamaanisha kwamba Mungu ndiye chanzo cha mamlaka na nguvu zote.

James Meadows
Mkufunzi na mhudumu wa Biblia.

Katika Mdo. 17:24, Biblia inasema kwamba Mungu ndiye mamlaka ya mwisho. Ndiye Bwana wa ulimwengu huu. Aliuumba ulimwengu huu. Mwanadamu na wanyama wote wako chini yake na kwenye maamuzi yake. Zaburi 95:5-6 inaonyesha kwamba dunia ni mali yake. Ni nyumba yake, naye ndiye muumba wake. Hivyo basi, wote waishio katika nyumba hii wako chini ya amri na maamuzi yake.

Ben Moseley
Profesa wa chuo kikuu na Mhudumu.

Chukua, kwa mfano, nyumba ambayo umeijenga kwa mikono yako mwenyewe – nyumba ambayo umeiunda na kuipendzesha kwa pesa zako mwenyewe, na ambapo wewe na familia yako mnaishi. Je, usingelikuwa na haki ya kuanzisha sheria kuhusu ni nini cha kufanya na ni kipi hikipaswi kufanywa katika nyumba au kwenye nyumba? Je, usingelikuwa na haki ya kuanzisha baadhi ya sheria na miongozo kwa wale wanaoishi ndani ya nyumba yako? Kwa hakika ungelifanya hivyo! Na wale ambao wanaishi

Kuhusu Mamlaka Kwenye Dini

kwenye nyumba yako wasingelikuwa na haki ya kubadilisha au kuharibu sheria bila ruhusa yako. Katika hali inayofanana, Mungu ameweka sheria na miongozo kwa kila mmoja wetu. Aliujenga ulimwengu huu. Ndiye muumba wa ulimwengu huu. Ni nyumba yake, na yeye ameweka sheria. Nyumba ni mali yake. Si juu yetu kubadilisha sheria zinazohusu jinsi ya kuishi katika ile nyumba. Ndiye mmiliki, mjenzi na mwendelezaji wa uumbaji huu mkuu. Hivyo, yeye ana haki ya kutawala shughuli za wanadamu kwa sababu yeye ana mamlaka yote.

Sasa, hebu turejee kwenye Biblia tuone inasemaje kuhusu mamlaka ya Mungu. Kama tunavyofanya, hebu tuone ni nani mwingine mwenye mamlaka dhidi ya viumbe vyote.

Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. (Waebrania 1:1-2).

Kulingana na hii mistari, Mungu ameamua kutawala na kuuamuru uumbaji wake siku hizi kupitia Mwanawe, Yesu Kristo. Kulingana na Waebrania 1:2, Mungu amemchagua Yesu awe “mrithi wa vitu vyote.” Kama Mwana wa pekee wa kweli wa Mungu, Kristo amepewa vitu vyote na Mungu. Ukweli huu unaelezewa zaidi katika Yohana 3:35: “Baba ampenda Mwana, naye amempa vyote mkononi mwake.” Vitu vyote vimekabidhiwa mikononi mwa Yesu. Moja kati ya vitu hivyo ni kuhusu mamlaka dhidi ya uumbaji.

....Baba, saa imekwisha kufika. Mtukuze Mwanao, ili Mwana wako naye akutukuze wewe, kama vile ulivyompa mamlaka juu ya wote wenye mwili, ili kwamba wote uliomba awape uzima wa milele (Yohana 17:1-2)

Kutoka katika mistari hii, na mingine tuliyoiangalia, tunaweza kujifunza kwamba kwa hakika Mungu ndiye chanzo cha msingi cha mamlaka. Pia tunajifunza, hata hivyo kwamba, amempa Mwanawe Yesu mamlaka yote (“Amempa vyote mkononi mwake”, Yohana 3:35).

Kristo ndiye mamlaka yetu katika dini. Katika Mathayo 28:18-19, Kristo alisema, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi.”

**Curtis Cates
Mkufunzi wa Biblia na mhudumu**

Lakini ni kitu gani mahususi ambacho Mungu alikiweka mikononi mwa Kristo?

Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo, kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake, aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wa kuume katika ulimwengu wa roho, juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu na usultani, na kila jina litajwalwo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia, akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa, ambalo, ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote. (Waefeso 1:19-23)

Kulingana na kile tulichokisoma punde, Yesu ana mamlaka yote


- **Ana mamlaka dhidi ya mamlaka zote.**
- **Yeye yuko juu ya kila jina.**
- **Vitu vyote vimewekwa chini ya miguu yake.**
- **Yeye ndiye kichwa cha kanisa.**

Bayana kabisa, Yesu ana mamlaka yote. Haya mamlaka ni kitu ambacho yeye mwenyewe binafsi alidai, kama Mathayo 28:18 inaweka wazi: “Nimepewa mamlaka yote, mbinguni na duniani.”

Je, ni mamlaka kiasi gani aliyonayo Yesu? Anayamiliki yote. Hivyo, katika kujibu swali la pili kuhusu, Ni nani aliyemamlaka katika dini, ni lazima tuseme kwa msisitizo kwamba Mungu ndiye mamlaka ya mwisho dhidi ya ulimwengu, na ya kwamba ameyatoa mamlaka haya kwa mwanawe, Yesu.

Kristo ndiye mamlaka yetu katika dini, kama Mathayo 28:18 inavyoonesha, Kristo alisema, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani” Mungu alisema, akimzungumzia Yesu, kwamba Yeye ni mwanawe mpendwa, na kwamba wanadamu wanapaswa kumtii yeye (Mathayo 17:5)

**Bobby Liddell
Mkufunzi na mhudumu wa Biblia**



SEHEMU YA MARUDIO: NI NANI AU NI NINI AMBACHO NDICHO MAMLAKA KATIKA DINI?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na mstari hapo chini, Je, Mungu alikufanya au “alikuumba” wewe? NDIYO / HAPANA.

Kwa kuwa BWANA ni Mungu mkuu, Na mfalme mkuu juu ya miungu yote. Mkononi mwake zimo bonde za dunia, Hata vilele vya milima ni vyake. Bahari ni yake, ndiye aliyeifanya, na mikono yake iliumba nchi kavu. Njoni, tuabudu, tusujudu, Tupige magoti mbele za BWANA aliyetuumba. (Zaburi 95:5-6)

2. Kulingana na mstari hapo chini, kutokana na kwamba Mungu ndiye aliyeumba kila kitu, Je, yeye ni Bwana (mwenye mamlaka yote) wa mbinguni na duniani? NDIYO / HAPANA

Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono (Mdo. 17:24)

3. Je, Mungu ana haki ya kuweka sheria kuhusu jinsi tunavyopaswa kuishi wakati tunakaa juu ya dunia ambayo ameiumba? NDIYO / HAPANA

4. Kulingana na Mathayo 28:18, Je, Yesu ana mamlaka dhidi ya mbingu na nchi? NDIYO / HAPANA

5. Kulingana na Yohana 17:1-2 na mstari hapo chini, Je, ni nani aliyempa Yesu mamlaka yote?

Baba ampenda Mwana, naye amempa vyote mkononi mwake (Yohana 3:35)

6. Kulingana na Waefeso 1:19-23, Yesu ana nguvu (mamlaka) dhidi ya _____, “ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.”

MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Je, unaamini kwamba Mungu ni “Bwana wa mbingu na nchi”? NDIYO / HAPANA

- B. Je, uko tayari kumtii Yesu kwa chochote kile atakacho kuambia ufanye? NDIYO / HAPANA

MASUALA YA KUZUNGUMZA

- A. Kama umelipia kwa ajili ya kujenga na kuimiliki nyumba, basi hilo litakupa wewe haki ya kusema kwamba ni nini kinapaswa kutokea kwenye, au katika hiyo nyumba. Je, ni kwa jinsi gani hii kanuni inatumika kwa Mungu, ambaye “aliufanya” ulimwengu?

Kuhusu Mamlaka Kwenye Dini

- B. Kulingana na mstari hapo chini, Mungu anawaamuru wanadamu wote kila mahali watubu kwa ajili ya dhambi zao. Je, ni kwa nini ana mamlaka ya kutoa amri kama hii? Je, mwitikio wa watu waliopo duniani unapaswa kuwa wa namna gani dhidi ya amri za Mungu?

Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni, bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu (Mdo. 17:30)



JE, HAYA MAMLAKA YALIDHIHIRISHWA KWA NJIA GANI?

Sasa, hebu tujiulize: “Je, mamlaka haya yalidhihirishwa kwa njia gani?” Kwa maneno mengine, Je, ni kwa namna gani Kristo ana tawala uumbaji wake? Je, ni kwa jinsi gani anaanzisha sheria dhidi ya huo uumbaji? Hebu turudi kwa kitambo kidogo kwenye mada yetu ya michezo. Hebu tuseme wewe au mimi tulikwenda kushiriki katika mashindano ya kukimbia. Ili kwamba tuweze kufanya hivyo, Je, tusingelipaswa kujua sheria zake ni zipi? Ama kwa hakika tungelipaswa. Lakini kwa kujua tu mwenye mamlaka ni nani, au bodi yenye mamlaka ni ipi, kwa hakika havitoshi kabisa. Tungelihitaji aina fulani ya mawasiliano kutoka katika chombo hicho ili kuweza kujua jinsi tunavyopaswa kucheza mchezo - kama vile Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki wakati washiriki wake wanapowasilisha sheria zao kwa wachezaji, makocha, waamuzi na mataifa.

Vivyo hivyo, katika kukabiliana na masuala ya kidini, ni muhimu tukijua kwamba Mungu ndiye mwenye mamlaka ya mwisho. Lakini kwamba, katika hilo lenyewe, bado halitoshi. Katika kukimbia mbio za maisha, ni lazima tufahamu kwamba sheria ni zipi. Ni lazima tujui kile ambacho Yesu anataka tufanye. Kumbuka kile Yesu alichosema katika Mathayo 7:21 – “Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.” Hivyo basi, tunapaswa kujua sheria na amri za Mungu ni zipi – sheria na amri ambazo zimetolewa na Mungu kwa Mwanawe Yesu.

Lakini, ni kwa jinsi gani Yesu anatoa amri zake? Je, ni kwa jinsi gani aliyatumia mamlaka yake? Je, ni kwa jinsi gani Yesu “anatuongoza” ili tuweze kufanya kitu ambacho anatataka tufanye? Je, ni kwa jinsi gani aliyawasilisha mapenzi yake kwetu? Je, hutujia kwa njia ya ndoto? Je, huijaza mioyo yetu kwa ujumbe wa muhimu?

Ili kuwa na hakika, wakati fulani Mungu aliyawakilisha mapenzi yake kwa mwanadamu katika baadhi ya njia maalumu sana. Kwa mfano, Mungu alizungumza na Musa moja kwa moja kupitia katika kichaka kilichokuwa kiki-

ungua (Kutoka 3:4). Pia aliwasilisha kwa njia ya ndoto, kama kwenye suala la Yakobo (Mwanzo 31:11). Wakati fulani kulipokuwa na sherehe iliyodhaminiwa na mfalme wa Babeli, Mungu alitumia mkono kama wa mwanadamu kuandika ujumbe wa muhimu kwenye ukuta (Danieli 5:5), katika tukio lingine, Mungu alimruhusu punda kuzungumza na nabii aliyeitwa Balaamu (Hesabu 22:28). Lakini, Je, ni kwa njia hizi Mungu anayafunua mapenzi yake leo? Je, hizi bado ni njia ambazo anatumia na kutuongoza nazo leo? Biblia inatoa jibu.

Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu (Waebrania 1:1-2)

Ndiyo, wakati fulani Mungu alizungumza kwa njia mbalimbali. Lakini kulingana na Waebrania 1:1-2, leo anazungumza nasi kupitia Mwana wake. Ni kwa kupitia Yesu Kristo ndipo tunapozifahamu sheria na amri za Mungu.

Wakati Yesu alipokuwa duniani, alizitoa hizo sheria na amri kwa njia ya mdomo – hilo ni, kulingana na neno lililolenwa. Kulingana na Marko 1:38, sehemu ya msingi ya huduma ya Bwana ya hadhara ilikuwa ni kuhubiri na kufundisha. Yesu alikuwa na huruma sana. Alikuwa anawajali sana watu, na alitaka wafahamu ni kwa jinsi gani watakuwa na furaha. Hivyo basi, aliwafundisha maneno na amri za Mungu. Mahubiri ya Kristo yalikuwa ya huruma na yakukemea kwa wakati mmoja, lakini pia yalikuwa ni yenye mamlaka.

Hotuba alizozitoa zilizungumza moja kwa moja na watu kama alivyokuwa akiwaonya watu wageuke kutoka katika tabia zao zisizo za kimungu na kuyaacha mapokeo ya kidini yasiyo halali. Alitoa amri mahususi kuhusu jinsi ya kuishi na kuepukana na dhambi. Mara nyingi alifundisha vitu kama:

- “Usiape” (Mathayo 5:34).
- “Wapendeni maadui zenu” (Mathayo 5:44).
- “Tweni macho na chachu ya Mafarisayo” (Mathayo 16:6).

Sura ya 3

- “Mpende Bwana Mungu wako” (Mathayo 22:37).
- “Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu” (Mathayo 6:33).
- “Tafuteni nanyi mtapata” (Mathayo 7:7).
- “Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba” (Mathayo 7:13).
- “Jihadharini na manabii wa uongo” (Mathayo 7:15).
- “Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa” (Luka 6:38).

Maneno yake yenye nguvu yalipokelewa kwa heshima na mshangao, kama ilivyofunuliwa na Mathayo akiizungumzia hotuba ya Kristo ya mlimani.

Ikawa, Yesu alipoyamaliza maneno hayo, makutano walishangaa mno kwa mafundisho yake, kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi wao (Mathayo 7:28-29).

Kwa hakika, maneno yaliyonenwa na Kristo yalikuwa ni yenye mamlaka. Kwa maneno yake, Yesu angeliweza kutuliza dhoruba (Marko 4:39), kumtakasa mkoma (Mathayo 8:3), au kufufua wafu (Yohana 11:43). Hata hivyo, angalia kile Yesu alichokisema kuhusu nguvu na umuhimu wa neno lake kwa ajili ya kuyabadilisha maisha ya wenye dhambi.

Roho ndiyo itiyayo uzima, mwili haufai kitu, maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima (Yohana 6:63).

Maneno ya Yesu yana nguvu. Wakati alipokuwa hapa duniani, aliwaita wenye dhambi ili wabadilishwe na kufanana na mapenzi yake. Alifanya hayo kwa njia ya kunena. Kupitia mahubiri na mafundisho yake, aliwaamuru watu wabadilike na kufanana na mamlaka ya mwisho itokayo mbinguni. Aliwaamuru watu wa siku hizo kwa maneno aliyonena.

Lakini, vipi kuhusu leo? Kama, wakati alipokuwa duniani, Yesu alitumia mamlaka yake kwa njia ya neno alilolinena, Je, ni kwa jinsi gani anayatumia mamlaka yake leo? Kutokana na kwamba hayupo pamoja nasi katika hali ya kimwili, ni nini, au ni nani ambaye ndiye mamlaka yetu?

Katika kulijibu hili swali, hebu tusome kile ambacho waandishi wa Agano Jipya walichofundisha kuhusu chanzo na mamlaka ya uandishi wao wenyewe:

Kwa maana, ndugu zangu, injili hiyo niliyowahubiri, nawajulilisha ya kuwa siyo ya namna ya kibinadamu. Kwa kuwa sikuipokea kwa mwanadamu wala sikufundishwa na mwanadamu, bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo (Wagalatia 1:11-12).

Angalia mtume Yohana aliagizwa na Yesu kuyaandikia makanisa saba ya Asia:

Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana, nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu, ikisema, “Mimi ni alfa na Omega, mwanzo na mwisho,”

Haya uyaonayo uyaandike katika chuo, ukayapeleke kwa hayo makanisa saba ...” (Ufunuo 1:10-11).

Yohana aliambiwa na Yesu aandike kile alichokiona. Yeye pamoja na waandishi wengine wa Agano Jipya waliagizwa kuandika ufunuo wa Yesu Kristo. Hata hivyo, ni muhimu kujua kwamba wakati hawa watu walipo andika Biblia, walifanya hivyo chini ya uongozi na maelekezo ya Roho Mtakatifu.

Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu (2 Petro 1:20-21).

Hii mistari, na mingine kama hii, ni michache tu kati ya rejea nyingi ambazo zinadhihirisha kwamba kile kilichandikwa kwenye Biblia si maneno ya wanadamu, lakini badala yake ni maneno na mapenzi ya Yesu Kristo, kama yalivyofunuliwa na Roho Mtakatifu wa Mungu.

Manabii wote (hiyo ni, wale wote walioandika Biblia) waliongozwa na Roho Mtakatifu. Walikuwa “wakichukuliwa pamoja” katika uandishi wao ili kwamba kile tulichonacho kwenye Biblia kiwe ni pumzi ya Mungu, amri za Mungu, na utawala wake katika maisha yetu.

**Chuck Homer
Mkufunzi na mhudumu wa Biblia**

Katika kutokuwepo kwa Bwana, ametupa neno lililoandikwa ili liyaongoze matendo yetu na kuzitawala hatua zetu. Agano Jipya ndilo jalada la Bwana la mamlaka ambalo tunapaswa kulitii na kulifuata. Paulo katika 1 Wakorintho 9:21, analizungumzia kama “sheria,” na katika Wagalatia 6:2, inatajwa hiyo sheria kama “sheria ya Kristo” ambayo inapaswa “kufuatwa” (mfano, kuitii). Ni Paulo aliyefunua katika Wagalatia 6:16, “Utawala wa Mungu,” au kiwango, ambacho mwanadamu anapaswa kuishi kwacho kama anataka kuipata amani na rehema ya Mungu.

Hebu tugeukie tena mfano wetu wa michezo ya Olimpiki. Angalia tena jinsi mamlaka ya Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki inavyofanyiwa kazi, na matokeo ya mwisho katika kitabu cha sheria/kanuni za Olimpiki. Kama mwanamichezo au mwamuzi anataka kujua kipi kifanyike na kipi kisifanyike, ndipo hukiendea kitabu cha sheria ili kwamba aweze kukubaliwa na kutambuliwa na mamlaka ya bodi ya Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki.

Katika michezo ya Olimpiki, sheria zinazotambuliwa ni lazima zizingatiwe, zijifunzwe na kuzitii ili uweze kushiriki ipasavyo katika tukio lolote. Vivyo hivyo, katika kuishi ipasavyo mbele za Mungu, watu binafsi na Kanisa ni lazima wazingatie, wajifunze na kulitii Agano Jipya la Kristo ili waweze kuishi maisha ya kikristo ipasavyo. Kulingana na kile mtume Paulo alichokiandika katika barua kwa Timotheo, kama tunataka kushinda zawadi ya mbinguni, tu-

Kuhusu Mamlaka Kwenye Dini

napaswa kuishi maisha yanayolingana na sheria zilizowe-
kwa na Mungu.

Katika masuala ya kidini, Mungu (mfano. Uungu) ndiye Mamlaka Kuu dhidi ya vitu vyote. Yesu, kama sehemu ya Uungu, amepewa “mamlaka yote mbinguni na duniani” (Mathayo 28:18). Wakati akiwa duniani, Yesu ali-ahidi kwamba Roho Mtakatifu atatumwa katika jina la Kristo ili awaongoze mitume katika uandishi wa Maandiko Matakatifu. Maandiko – kile tunacho kijua leo kama Bib-
lia – ni ufunuo wa Mungu kwa mwanadamu. Tumepewa Biblia kama kitabu cha mwongozo au sheria ambacho kwa-
cho tunapaswa kuishi, na hivyo tunaweza kuzijua sheria za Mungu, ambaye ndiye Mamlaka yetu Kuu.

*Ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu. Hakuna apigaye vita ajitiaye ka-
tika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliy-
emwandika awe askari. Hata mtu akishindana
katika michezo hapewi taji, asiposhindana kwa
halali (2 Timotheo 2:3-5).*

Leo, kwenye Biblia ndipo tunapopata sheria kwa ajili ya kukimbilia mbio za kikristo. Ni kitabu cha sheria ambacho mimi na wewe tunakifuata kama tunataka kwenda mbinguni. Kama tukizikataa sheria ambazo zinapatikana ndani ya Bib-
lia, na kama tukikataa kujinidhamisha nafsi zetu katika “ku-
kimbia mbio,” ndipo tutakapo ondolewa kwa kutokuwa na sifa. Hili ndilo jambo lilelile ambalo mtume Paulo alilokuwa

Mpango wa Mamlaka Ya Olimpiki

**Kamati ya
Kimataifa ya Olimpiki**
(Mamlaka Kuu)



**Rais na bodi ya
watendaji wakuu**
(Huanzisha kanuni na Miongozo)



Mkurugenzi mkuu
(Husimamia kanuni)



**Kitabu cha
Kanuni cha Olimpiki**
(Kiwango cha Mamlaka)



Mpango wa Mamlaka ya Kiroho

MUNGU
(Mamlaka Kuu)



**MWANA WA
MUNGU-YESU**
(Ana mamlaka yote
mbinguni na duniani)



**ROHO
MTAKATIFU**
(Aliifunua Kweli
yote kwa Mitume)



BIBLIA
(Kiwango cha Mamlaka)



Sura ya 3

anamaanisha aliposema, “nautesa mwili wangu na kuutumikisha, isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa” (1 Wakorintho 9:27). Kitabu cha sheria kitakachotumika kuhukumu ama tuna sifa au la, ni Agano Jipya la Yesu Kristo. Kristo mwenyewe alisema:

Yeye anikataaye mimi, asiye yakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho (Yohana 12:48).

Kulingana na Yesu, Neno lake – kama lilivyofunuliwa katika Agano Jipya – ndilo litakalo mhukumu kila mmoja wetu siku ya mwisho. Leo, Yesu bado ana mamlaka, na agano

lake lililoandikwa limefunuliwa katika Agano Jipya, ambalo linatutawala sisi hata sasa.

Hivyo, katika kulijibu swali la tatu, “Je, mamlaka haya yemedhihirishwa kwa njia gani?” ni hakika kwamba tuta-fikia hitimisho kwamba, Mungu ameyadhihirisha mamlaka yake kupitia neno lililoandikwa, yaani Biblia. Hivyo basi, Biblia, inapaswa kuchukuliwa kama chanzo cha msingi kwa ajili ya kugundua kipi ni sahihi na kipi si sahihi. Biblia ina amri za Mungu na maelekezo kwa ajili ya kuishi maisha ya kikristo. Inahusisha hadithi inayohusu upendo wake na amri zake kwa ajili ya maisha.



SEHEMU YA MARUDIO: JE, HAYA MAMLAKA YAMEDHIHIRISHWA KWA NJIA GANI?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Siku za nyuma, Mungu aliwasiliana na watu wake kupitia njia mbalimbali (ndoto, kichaka kina- chowaka moto, akizungumza kupitia wanyama, n.k). Kulingana na Waebrania 1:1-2, Je, Mungu bado anazitumia njia hizo ili kuzungumza na watu wake leo? NDIYO/HAPANA
2. Kulingana na Waebrania 1:1-2, Mungu anasema na watu leo kwa njia ya _____.
3. Kulingana na mstari hapo chini, Je, sisi leo, tunazifahamu sheria za Mungu kupitia Yesu Kristo? NDIYO / HAPANA
Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililo- linena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho. Kwa sababu mimi sikunena kwa nafsi yangu tu, bali Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema. Nami najua ya kuwa agizo lake ni uzima wa milele, basi hayo ninenayo mimi, kama Baba alivyoniambia, ndivyo ninenavyo (Yohana 12:48-50).
4. Kulingana na Mathayo 7:28-29, Je, maneno ya Yesu ni yenye mamlaka? NDIYO / HAPANA

Kuhusu Mamlaka Kwenye Dini

5. Akiwa duniani, Yesu aliyatumia mamlaka yake kwa njia ya neno lake alilolinena, lakini leo anayatumia mamlaka yake kwa njia ya neno lake lililo _____, Biblia.
 6. Kulingana na 2 Petro 1:20-21, watu walioandika Biblia walifanya hivyo chini ya uongozi wa _____.
 7. Kulingana na mstari hapo chini, ufunuo ulioandikwa wa Kristo pia unatambulika kama _____ ya _____.
- Mchukuliane mizigo na kuitimiza hiyo sheria ya Kristo (Wagalatia 6:2).*
8. Katika kukimbia mbio za ukristo Biblia ndiyo _____ wewe na mimi tunapaswa kuifuata kama tunataka kwenda mbinguni.
 9. Kulingana na 1 Wakorintho 9:27, Je, mkristo anaweza kukataliwa asiingie mbinguni? NDIYO / HAPANA.
 10. Kulingana na Yohana 12:48, siku ya hukumu tutahukumiwa kwa maneno ya _____.
 11. Kulingana na mstari hapo chini, Je, maneno ya Yesu yana nguvu ya kutusafisha dhambi? NDIYO/HAPANA

Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia (Yohana 15:3).

12. Kulingana na Yohana 6:63, Maneno ya Yesu ni _____ na _____.

Sehemu ya majibu kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA inapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Je, unaamini kwamba Yesu Kristo ana mamlaka dhidi ya maisha yako? NDIYO / HAPANA
- B. Je, uko tayari kuzitii amri na sheria za Mungu? NDIYO / HAPANA.
- C. Je, unamkubali Yesu kama ndiye kichwa cha kanisa? NDIYO / HAPANA.

MASUALA YA KUZUNGUMZA

- A. Kama Yesu ndiye kichwa cha kanisa, hilo linasema nini kuhusu makanisa ambayo wanaume, wanawake au kikundi cha watu ambacho ndicho kichwa chao?
- B. Kulingana na mstari hapo chini, taja vitu vinne ambavyo Mungu amempa Yesu mamlaka dhidi yake.

Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa, ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote (Waefeso 1:19-23).



Sura ya 3

JE, LEO, KUNA KIWANGO ZAIDI YA KIMOJA CHA MAMLAKA?

Hata hivyo, sasa, hebu tujiulize swali: “Je, Biblia ndicho kitabu pekee cha kanuni/sheria tunachokihitaji?” Je, kuna kiwango zaidi ya kimoja cha mamlaka leo? Je, kuna makundi mengine ya kidini ambayo yanaongeza na kutumia vitu vingine au badala ya Agano Jipya? Hebu tumwache huyu mwana theolojia ajibu hilo swali:

Baadhi wanatilia mkazo sana kwenye Biblia kuliko wengine wafanyavyo. Baadhi hutilia mkazo katika mambo yaliyopita, kitu fulani kilichoandikwa na mwanadamu, kitu fulani kilicho semwa na wanadamu, au kitu fulani kilichokubaliwa na wanadamu. Nina vitabu viwili ambavyo vinazungumzia zaidi sawa na hiki tunacho kizungumzia hapa. Kitabu kimoja, Kitabu cha Nidhamu, kinatoka katika kitabu cha kikundi fulani cha kidini, na kinasema, “Hii Nidhamu ni kitabu cha sheria za (Kanisa). Ni matokeo ya mikutano mingi ya jumla ya historia ya makundi ya kidini, ambayo sasa yanaunda Kanisa. Nidhamu ndicho chombo cha kuweka sheria, mipango, dola, na mchakato ambayo kwayo (Makanisa) yanajitawala.” Hiki ndicho kitabu ambacho kinazidishwa katika Biblia. Ni kitendo cha kawaida kwa baadhi ya watu katika dini kutambua chanzo kinaonekana cha mamlaka tofauti na Biblia, kuliko ilivyo kwao kuitambua Biblia kama ndicho chanzo pekee cha mamlaka. Kwenye kitabu chenye jina Vifungu vya Imani, tunasoma yafuatayo: “Kiwango cha Kazi cha Kanisa kinatoa madaraka ya mamlaka iliyoandikwa ya Kanisa katika mafundisho. Kazi iliyochukuliwa kwa kupigiwa kura na kanisa kama ndilo lenye mamlaka katika imani na mafundisho ni nne” Vifungu vya Imani kinaendelea kutaja vitabu vingine vinne. Biblia ndiyo pekee kati ya vitabu hivyo. Hivyo, ndiyo, vikundi vingi vya kidini vina vitabu vyao wenyewe, sheria zao wenyewe, na amri zao wenyewe. Swali tunalopaswa kuuliza ni: “Je, tunavihitaji hivyo vitabu vingine?” Hapana, hatuvihitaji. Tunacho kile tunachokihitaji katika Biblia.

Carl Garner
Mkufunzi na mhudumu wa Biblia

Ndiyo, kuna vikundi vya kidini ambavyo vinatumia vitu vingine zaidi ya Agano Jipya kama kiwango cha mamlaka katika mambo ya kidini. Wanatoa

- Vitabu vya muongozo
- Ufundishaji wa Nidhamu
- Vifungu vya Imani
- Agano “Jingine”
- Uongofu
- Ukiri wa Imani

Je, ni kweli tunavihitaji hivi viwango vingine vya mamlaka? Je, tunaweza kuiendea Biblia pekee ili tuweze kujua ni kipi tunapaswa kufanya ili tukamilike mbele za Mungu? Je, tunaweza, kwa kusoma Biblia tu, kufahamu mambo kama ni jinsi gani ya kuliendesha kanisa, Je, ni kipi tunapaswa kufundisha, na Je, tunapaswa kuabudu kwa njia gani? Je, tunaweza kwa kupitia kujifunza kwa makini neno la Mungu, kujifunza inamaanisha nini kwa mtu kuwa mume mwema, mke mwema au mzazi mwema? Je, tunaweza kwa kupitia neno la Mungu, kujifunza jinsi ya kukabiliana na matatizo na kuyashinda magumu katika maisha yetu? Mtume Paulo alijibu maswali kama hayo alipoandika:

Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema (2 Timotheo 3:16-17)

Ndiyo, maandiko yanaweza kutukamilisha mbele za Mungu. Kwa hakika, yanapaswa kutumika kwa ajili ya:

- Mafundisho
- Kuonya (kubainisha dhambi)
- Kuwasahihisha (Kuwaongoza)
- Kuwaadibisha katika haki (maelekezo kwa kile kilicho sahihi na kile kisicho sahihi).
- Kuwaongoza kwa ajili ya kila tendo jema.

Je, kuna la kushangaza, kwamba Petro angelimzungumzia Mungu kwamba “Uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe” (2 Petro 1:3)? Hapana, hatupaswi kushangazwa na lolote kujua kwamba Biblia inatosha kuziongoza hatua zetu. Baada ya yote, Biblia ni matokeo ya Mungu anayejua yote na mwenye upendo wote ambaye anataka kutuokoa sisi na anatutaka sisi tuwe na furaha!

Lakini unaweza ukauliza, “Je, Roho hajatoa ‘ufunuo wa ziada’ tangu wakati wa mitume? Je, Roho hatufunulii jumbe mbalimbali leo, kando (tofauti) na neno?”

Angalia kile Yesu alichokisema kuhusu Roho (ambaye alimuita “Roho wa Kweli”)

Lakini huyu Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha niliyowaambia (Yohana 14:26).

Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari zake (Yohana 16:13).

Kuhusu Mamlaka Kwenye Dini

Katika kukiangalia hiki kifungu, kuna ukweli wa aina mbili tunaopaswa kuuweka akilini:

- Mitume wangeliongozwa na Roho Mtakatifu katika kuyakumbuka maneno ya Kristo.
- Mitume wangelifundishwa “mambo yote,” angeliwakumbusha “mambo yote,” na angeliwaongoza katika “kweli yote.”

Kama mitume waliongozwa katika kweli yote, sasa, Je, tunapaswa kukubali kupokea ufunuo wowote wa ziada leo? Hapana, kwa sababu yote, ina maanisha mambo yote. Kweli yote ilitolewa. Kulingana na Biblia, ukweli wote wa kiroho ulifunuliwa ndani ya kipindi cha maisha ya mitume. “Imani,” kama Yuda alivyofunua, “waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu” (Yuda 3). Imani haikutolewa kwa sehemu katika karne ya kwanza, na kukamilishwa karne kadhaa zilizofuata. Badala yake, Yuda anasema walikabidhiwa mara moja tu. Ukweli wote wa kidini ulifunuliwa katika karne ya kwanza, na hakuna injili nyingine inayopaswa kuhubiriwa, kama Paulo alivyoweka wazi alipoandika:

Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuli-yowahubiri, na alaaniwe (Wagalatia 1:8).

Paulo anasema kwamba hata malaika wa mbinguni akihubiri kitu tofauti na kile wale wa kristo wa karne ya kwanza walichokipokea, kinapaswa kukataliwa. Hivyo basi, tunapaswa kuhitimisha kwamba Injili – Ufunuo wa Yesu Kristo kama ulivyotolewa wakati wa maisha ya mitume – ndicho kiwango chetu pekee cha mamlaka ya kidini leo.



SEHEMU YA MARUDIO: JE, KUNA KIWANGO ZAIDI YA KIMOJA CHA MAMLAKA LEO?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, baadhi ya vikundi vya kidini na vikundi vyenye misingi ya kikristo vinatumia kitu tofauti na Biblia au kitu kingine cha ziada kwenye Biblia kama kiwango chao cha mamlaka ya kidini? NDIYO / HAPANA
2. Kulingana na mstari hapo chini, Je, Biblia inatukamilisha tupate kutenda kila tendo jema? NDIYO / HAPANA

Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema (2 Timotheo 3:16-17)

3. Kulingana na 2 Timotheo 3:16-17, Je, tunahitaji mapokeo, vitabu vya kiada, vitabu vya kanuni za imani (mwongozo), ukiri wa imani, au ufunuo wa siku za mwisho ili kutukamilisha mbele za Mungu? NDIYO / HAPANA
4. Kulingana na 2 Petro 1:3, “Uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo _____ na _____.”
5. Kutokana na majibu yako kwenye swali la 3 na la 4 hapo juu, Je, tunahitaji “vitabu vingine” au chanzo kingine chochote, tofauti na Biblia, kama kiwango cha mamlaka ya kidini? NDIYO / HAPANA

Sura ya 3

6. Kulingana na Yohana 16:13, katika karne ya kwanza Yesu aliwaambia mitume kwamba wataongozwa katika kweli _____.
7. Kama mitume waliongozwa katika kweli yote, Je, tunapaswa kutarajia kupokea ufunuo mwingine mpya leo? NDIYO / HAPANA
8. Kulingana na Wagalatia 1:8, Paulo alisema “Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na _____.”
9. Kulingana na Yuda 3, tunapaswa “kuishindania imani waliyokabidhiwa watakatifu _____.”

MAJIBU kwa ajili ya **MASWALI YA KUJIFUNZIA** yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Je, unaamini kwamba Biblia ni neno la Mungu lililovuviwa? NDIYO / HAPANA.
- B. Je, unafikiri kwamba watu leo wanahitaji “kitu cha zaidi ya” Biblia ili waweze kwenda mbinguni? NDIYO / HAPANA
- C. Je, uko tayari kufanya kile ambacho Biblia inakutaka ufanye ili uweze kuokolewa kutoka katika dhambi zako? NDIYO / HAPANA.

MASUALA YA KUZUNGUMZA

- A. Kulingana na 2 Timotheo 3:16-17, kuna mambo matano ambayo maandiko yanathamani kwayo. Je, mambo hayo matano ni yapi?
- B. Je, ni kwa nini wanadamu, ua vikundi vya wanadamu, wametengeneza vitabu vingine vya mamlaka ya kidini?



JE, KUNATOFAUTI GANI KATI YA AGANO JI-PYA NA AGANO LA KALE?

Sasa, kutokana na kwamba tumejifunza kwamba Mungu, kupitia Mwanawe Yesu, ndiye chanzo pekee cha mamlaka, na neno lake Takatifu, Biblia, ndicho kiwango cha mamlaka ya kidini leo, hebu tutumie muda kidogo kuzungumzia kuhusu Biblia na maagano yake mawili. Katika kutafuta kwetu ukweli kuhusu mamlaka katika dini, unaweza uka-
wa umegundua kwamba katika uhusiano wa Biblia nzima, tunaelekezwa tu katika Agano Jipya kama mamlaka yetu. Mara kwa mara unaweza ukajiuliza kama Agano la Kale ni muhimu au la. Hata hivyo Agano la Kale ni neno la Mungu pia, ama sivyo? Kwa hakika ndivyo. Agano la Kale ni sawa

na sehemu ya Biblia kama vile ilivyo kwa Agano Jipya, linapaswa kujifunzwa kwa makini sambamba na Agano Jipya. Mtume Paulo alisema kwamba Agano la Kale “liliandikwa ili kutufundisha sisi, ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini” (Warumi 15:4).

Lakini, Je, umeshawahi kustaajabu kwamba ni kwa nini linaitwa Agano la Kale? Na, Je, Agano la Kale ni sheria ya kidini tunayopaswa kuifuata leo? Hebu tumwachie mkufunzi na mtaalamu wa masomo ya Agano la Kale alijibu swali hili.

Tunapozungumzia Agano la Kale kama “la Kale,” hatumaanishi kwamba halina tena kazi au kwamba halina thamani. Badala yake, ni kama unaandika mkataba kwa mara ya pili. Unasema kwamba ulikuwa na “mkataba wa

Kuhusu Mamlaka Kwenye Dini

kale” na kwamba una “mkataba mpya.” Mungu amelifanya agano jipya au mkataba mpya, kama unaweza kusema - pamoja na watu wake. Na hicho ndicho mwandishi wa kitabu cha Waebrania anachokijadili – kwamba tumehama kutoka katika sheria ambayo ilikuwa mahususi kwa Wayahudi (kama ilivyoelezwa katika Kumbukumbu la Torati sura ya 5, wakati Mungu alipoelezea kwamba sheria ilikuwa ni kwa ajili ya watu ambao walikuwepo katika kutolewa kwa sheria kwenye mlima Sinai). Katika Yeremia 31:31-34, Mungu alisema kupitia nabii wake Yeremia kwamba, atalileta agano jipya (agano jipya au wosia mpya). Katika Waebrania 8:13. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania akinukuu kifungu hicho kutoka Yeremia 31 ili aweze kuzungumza kuhusu ni kwa jinsi gani sasa tuko chini ya agano jipya. Hivyo, watu wote leo wanawajibika chini ya sheria ya Kristo.

Denny Petrillo, Ph.D.

Profesa wa Agano la Kale na Masomo ya Kiyahudi

Kwa ufupi, tunaweza tukasema kwamba, Agano la Kale linaitwa “la kale” kwa sababu ni sheria ambayo haipo tena katika matumizi. Kulingana na Biblia, sheria hiyo walipewa waisraeli. Ilikuwa ni sheria ya muda mfupi ambayo iliandaa njia, na kuweka misingi kwa ajili ya Agano Jipya lililotolewa na Kristo. Mtume Paulo analiweka hivi:

Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani. Lakini, iwapo imani imekuja, hatupo tena chini ya kiongozi (Wagalatia 3:24-25).

Hatupo tena chini ya kiongozi. Katika karne ya kwanza, kiongozi mara zote alikuwa ni mtumwa aliyeaminiwa ambaye alikuwa na wajibu wa kuchunga maadili na elimu ya mtoto. Kama sehemu ya majukumu yake, alikuwa na kazi ya kumuongoza mtoto kwenda na kutoka shule, na kumsaidia kukua kuelekea utu uzima. Wakati mtoto anapokuwa mtu mzima, hahitaji tena (au alikuwa chini ya mamlaka ya) kiongozi. Katika mazingira ya waraka wa Wagalatia, Agano la Kale ndilo lililokuwa kiongozi. Hiyo sheria ilikuwa na wajibu wa kuwaandaa wanadamu kwa ajili ya utu uzima. Dhumuni lake lilikuwa ni kutuelekeza kwa Kristo, na mpango wa imani ulioanzishwa na Kristo. Katika Wagalatia 6:2 na 1 Wakorintho 9:21, huo mpango unatajwa kama “sheria ya Kristo.” Sheria hiyo – sheria ya Kristo – ni sheria ambayo inatufunga siku za leo. Hivyo basi, hatupo tena chini ya mamlaka ya Agano la Kale. Agano la Kale lilikuwa ni kiongozi kutuelekeza kwa Yesu.

Lakini, Je, hili linamaanisha kwamba hatupo chini ya Amri Kumi kama zinavyopatikana katika kitabu cha Kutoka? Kuongea kwa kutilia mkazo, hapana, hatupo chini ya amri hizo. Amri Kumi zilikuwa ni sehemu ya Sheria ya Zamani, na hiyo sheria iliondolewa na Yesu. Soma Waefeso 2:15 – “Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya am-

ani.” Amri kumi – pamoja na mpango wa Kilawi wa dhambi za damu, ibada ya kwenye hema, kufukiza uvumba na siku maalumu za sherehe – kwa asili zilikuwa ni za muda mfupi. Kulingana na Waebrania 10:1, mambo hayo yalikuwa ni kivuli cha mambo mema yajayo. Sheria ya zamani iliwaandaa Waisraeli, na wanadamu wote kwa ajili ya ujio wa Masihi na Agano lake Jipya.

Wakati Yesu alipokuja na kulileta Agano Jipya, Sheria ya zamani (kale) iliondolewa. Kulingana na kitabu cha Waebrania, kwamba sheria inatoweka kwa sababu imefanywa kuwa “kuukuu” na Agano Jipya la Kristo:

Kwa kule kusema, Agano Jipya, amelifanya like la kwanza kuwa kuukuu. Lakini kitu kianzacho kuwa kikuukuu na kuchakaa ki karibu na kutoweka (Waebrania 8:13)

Leo, kutokana na kwamba Agano la Kale halitumiki siku hizi, Je, inakubalika kufanya uasherati, kusema uongo au kuiba? Ama kwa hakika haikubaliki! Tisa kati ya Amri Kumi zinapatikana katika Agano Jipya. Moja tu yenye udhuru ni amri kwa ajili ya Waisraeli ya kuitunza siku ya Sabato. Katika kulinganisha na Sabato, Wakristo wanaitunza meza ya Bwana. Meza hii ilianzishwa na Yesu kwenye Mathayo 26:26-28, na ilikumbukwa na wanafunzi wa karne ya kwanza katika kila siku ya kwanza ya juma, kulingana na Mdo. 20:7. Tisa kati ya amri kumi zinapatikana ndani ya Agano Jipya, ni sehemu ya muhimu ya Agano Jipya la Kristo.

Agano hili Jipya, au “Agano Jipya la Kristo” lilidhihirishwa na Roho Mtakatifu kwa mitume wa Bwana na/au wanafunzi. Agano la Kale (katika kifungu kama vile Yeremia 31, na sehemu nyingine) linatabiri siku ambazo Agano Jipya litakapoanzishwa. Leo, Agano hilo limeshaanzishwa. Agano la Kale limeondolewa. Leo, tunaishi chini ya mamlaka ya Kristo na neno lake lililoandikwa.



SEHEMU YA MARUDIO: JE, KUNATOFAUTI GANI KATI YA AGANO LA KALE NA AGANO JIPYA?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, Agano la Kale ni neno la Mungu? NDIYO / HAPANA
2. Kulingana na Warumi 15:4, mambo yaliyoandikwa katika Agano la Kale yaliandikwa kwa ajili ya _____.
3. Kulingana na mstari hapo chini, Yesu alisema hakuja kuitangua Torati au manabii, bali _____.
Msidhani ya kuwa nalikuja kutangua torari au manabii, la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. (Mathayo 5:17)
4. Kulingana na mstari hapo chini, Mungu alitabiri kwamba siku zitakuja ambapo atafanya _____ na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda.
Angalia, siku zinakuja, asema BWANA, nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda (Yeremia 31:31)
5. Kulingana na Waebrania 8:13, "kwa kule kusema, 'agano jipya,' amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu. Lakini kitu kianzacho kuwa kikuukuu na kuchakaa ki karibu na _____.
6. Agano la Kale linaitwa "la Kale" kwa sababu ni _____ na halipo tena katika _____.
7. Kulingana na Wagalatia 3:24-25, Agano la Kale lilitumika kama _____ katika kuuandaa ulimwengu kwa ajili ya Kristo.
8. Kulingana na mstari hapo chini, Je, sisi leo tunaishi chini ya "Sheria Mpya" – "Sheria ya Kristo?" NDIYO / HAPANA
Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi; kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa kama chini ya sheria, (ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria), ili niwapate walio chini ya sheria. Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria, (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo), ili niwapate hao wasio na sheria (1 Wakoritho 9:20-21).
9. Kulingana na Waefeso 2:15, Je, Yesu aliziondoa sheria za Agano la Kale za maagizo? NDIYO / HAPANA.
10. Je, baadhi ya amri kumi kutoka katika Agano la Kale zinapatikana katika Agano Jipya? NDIYO / HAPANA

Kuhusu Mamlaka Kwenye Dini

11. Je, kuna amri yoyote kati ya amri kumi ambayo haipatikani kwenye Agano Jipya? NDIYO / HAPANA

12. Kama ndivyo, ni ipi? _____

13. Agano la Kale lilitabiri siku za kuanzishwa kwa Agano Jipya, leo tunaishi chini ya _____ la Kristo na neno _____ lake.

MAJIBU kwa ajili ya **MASWALI YA KUJIFUNZIA** yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Je, unaamini kwamba leo watu wanapaswa kuishi chini ya Agano Jipya tu? NDIYO / HAPANA
- B. Je, uko tayari kufanya kile ambacho Mungu amekuambia ukifanye katika Agano Jipya ili uweze kuokolewa? NDIYO / HAPANA

MASUALA YA KUZUNGUMZA

- A. Waebrania 10:1 inasema, “Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayo kuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao” Je, ni kwa jinsi gani sheria ilikuwa ni “kivuli cha mema yatakayokuwa?” Sentensi hii inamaanisha nini?
- B. Ili hali Yesu hakuja kuitangua sheria ya Agano la Kale, hata hivyo aliiondoa sheria (Waefeso 2: 15) alipoitimiliza. Je, hii iliwezekanaje? Je, sheria ya Agano la Kale ilikuwa ni ya muda mfupi?



HITIMISHO

Kutafuta kwetu ukweli kumetupelekea kuhitimisha kwamba:

1. Neno “mamlaka” linamaanisha haki ya kutawala au kudhibiti.
2. Mungu ndiye chanzo cha mwisho cha mamlaka.
3. Mungu amempa Yesu Kristo mamlaka yote mbinguni na duniani.
4. Agano Jipya la Kristo ni sheria ambayo wanadamu wote wanapaswa kuishi chini yake leo.
5. Kristo ameyadhihirisha mamlaka yake, na kuyafunua mapenzi yake kwetu, kwa njia ya neno lililoandikwa, Biblia.

Neno lililoandikwa linatosha kutuongoza kwenda mbinguni. Linaelezea sheria za jinsi ya kuishi hapa duniani. Na pia, kulingana na mtume Petro na mtume Paulo, ndilo tunalolihitaji ili kututosheleza katika ukuaji wetu wa kiroho.

Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamaini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu (1 Petro 2:2)

Basi imani, chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo (Warumi 10:17)

Kama unataka kukuwa kiroho, unapaswa kujifunza neno la Mungu. Kama unataka kanuni za kukimbia mbio za ukristo, unapaswa kujifunza Biblia. Katika sehemu hii, tumejifunza ukweli kuhusu ni nini au ni nani anayepaswa kuwa mamlaka yetu katika dini. Mamlaka hayo ni Mungu. Ameufunua ujumbe na mwongozo wake katika Agano Jipya kwa ajili ya kutambua mipaka ya kuishi maisha ya kikristo. Maneno ya Kristo yanapaswa kuwa kiwango cha msingi cha hukumu siku Yesu atakaporudi, kulingana na Yohana 12:48 ni matumaini yangu kwamba utaendelea na mimi kwa kadiri tunavyoenenda na hii safari ya kutafuta ukweli. Ni safari ya muhimu sana katika maisha yako. Ungana nami katika kuatafuta ukweli.

Sura ya 3

MARUDIO YA SURA

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana ndani ya sura hii.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na Mathayo 28:18, Yesu alisema, "Nimepewa mamlaka _____, mbinguni na duniani."
2. Wakati Yesu alipokuwa duniani, aliyatumia mamlaka yake na kutoa amri zake kupitia neno lake lililo nenwa. Leo, Yesu anayatumia mamlaka yake kupitia neno lake _____, Biblia.
3. Kulingana na 2 Petro 1:3, Neno la Mungu hutupa vitu vyote vipasavyo _____ na _____.

MASWALI YA KUTILIA MKAZO

1. Je, leo tunaishi chini ya Agano la Kale? NDIYO / HAPANA
2. Kulingana na Wagalatia 1:8, Je, tunapaswa kuwa tayari kuikubali injili ya aina ye yote tofauti na ile inayopatikana katika Agano Jipya? NDIYO / HAPANA
3. Kulingana na mistari hapo chini, ukweli unaweza ukapatikana katika _____ la Yesu.

ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli. Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru (Yohana 8:31-32).

MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZA na MASWALI YA KUTILIA MKAZO yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MAMBO UNAYOPASWA KUFAHAMU

- Neno "mamlaka" linamaanisha haki ya kutawala au kudhibiti.
- Mungu ndiye chanzo cha mwisho cha mamlaka.
- Yesu alipokea mamlaka yote toka kwa Mungu.
- Yesu ndiye Kichwa cha kanisa.
- Tutahukumiwa kupitia mafundisho ya Yesu.
- Mitume walivuviwa na Roho Mtakatifu katika kuandika kwao Biblia.
- Neno lililovuviwa ndilo kiongozi wetu pekee katika dini.
- Agano Jipya ni sheria ambayo tupo chini yake na ni kwa kupitia hiyo sisi tutahukumiwa.

CHIMBA ZAIDI ...

Masomo hapo chini yamekusudiwa kwa wale watu ambao wangelipenda kujifunza somo hili zaidi. Kuna habari ambazo kimsingi hazikujadiliwa ndani ya somo.



MUNGU KAMA CHANZO CHA UKWELI

Yeye Mwamba, Kazi yake ni kamilifu; Maana, njia zake zote ni haki. Mungu wa uaminifu, asiye na uovu, Yeye ndiye mwenye haki na adili (Kumbukumbu la Torati 32:4).

Roho ya Bwana ilinena ndani yangu, Na neno lake likawa ulimini mwangu (2 Samweli 23:2).

Kufafanua maneno yako kwatia nuru, Na kumfahamisha mjinga (Zaburi 119:130).

Jumla ya neno lako ni kweli, Na kila hukumu ya haki yako ni ya milele (Zaburi 119:160).

Maneno yako yalionekana, nami nikayala; na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu; maana nimeitwa kwa jina lako Ee BWANA, Mungu wa majeshi (Yeremia 15:16).

Uwatakase kwa ile kweli, neno lako ndiyo kweli (Yohana 17:17).

Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyaifasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni (1 Wakorintho 2:12-13).

Kuhusu Mamlaka Kwenye Dini

*Paulo, mtumwa wa Mungu, na mtume wa Yesu Kristo; kwa ajili ya imani ya wateule wa Mungu, na ujuzi wa kweli ile ileta-
yo utauwa; katika tumaini la uzima wa milele, ambao Mungu
asiyeweza kusema uongo aliuhidi tangu milele (Tito 1:1-2).*

*Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika
maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu.
Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwan-
adamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu,
wakiongozwa na Roho Mtakatifu (2 Petro 1:20-21).*

VITU VYA KUFIKIRIA... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

1. Kulingana na Kumbukumbu la Torati 32:4, Mungu ni Mungu wa _____.
2. Katika 2 Samweli 23:2, Daudi anasema kwamba Mungu ameliweka neno lake katika _____ cha Daudi.
3. Kulingana na Zaburi 119:130, Neno la Mungu linatoa _____ na _____.
4. Kulingana na Zaburi 119:160, Je, neno lote la Mungu ni kweli? NDIYO / HAPANA
5. Katika Yeremia 15:16, Je, Yeremia alipata furaha katika kusherehekea maneno yake mwenyewe? NDIYO / HAPANA.
6. Kulingana na Yohana 17:17, Yesu alisema neno la Mungu ni _____.
7. Je, 1 Wakorintho 2:12-13 inafundisha kwamba mambo ambayo waandishi wa Biblia waliyoyaandika yanatoka kwa Mungu? NDIYO / HAPANA.
8. Tito 1:1-2 inafundisha kwamba Mungu hawezi _____.
9. “Wanadamu _____ walivyo kuwa _____ na Roho Mtakatifu” (2 Petro 1:20-21).



UTEGEMEZI WA MWANADAMU KWA MUNGU NA NENO LAKE

Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii, akilifuata neno lako. Kwa moyo wangu wote nimekufuata, Usiniache nipotee mbali na maagizo yako. Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, Nisije nikakutenda dhambi (Zaburi 119:9-11).

Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee

akili zako mwenyewe (Mithali 3:5).

Iko njia ione kanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti (Mithali 14:12).

Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu (Mhubiri 12:13).

Ee BWANA, najua yakuwa njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake; kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu (Yeremia 10:23).

Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache (Mathayo 7:13-14).

Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni (Mathayo 7:21).

Watu hawa (Wakristo waliokuwa Beroya) walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo (Mdo 17:11).

Wala msifuatisha namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu (Warumi 12:2).

Jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema (1 Wathesalonike 5:21).

Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli (2 Timotheo 2:15).

Wapenzi, msiiamini kila roho, bali ziharibuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani (1 Yohana 4:1).

...ni makuu, na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; Ni za haki, na za kweli, njia zako, Ee Mfalme wa mataifa (Ufunuo 15:3).

VITU VYA KUFIKIRIA... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

10. Je, Zaburi 119:9-11 inafundisha kwamba sisi tunamtegemea Mungu na neno lake ili kusafisha njia zetu na kuepuka dhambi? NDIYO / HAPANA
11. Kulingana na Mithali 3:5, Je, tunapaswa kutumia uelewetu ili kutambua kipi ni sahihi na kipi si sahihi? NDIYO / HAPANA
12. “Kuna njia ione kanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia ya _____” (Mithali 14:12).

Sura ya 3

13. Kulingana na Yeremia 10:23, Je, njia ya mwanadamu ni njia sahihi? NDIYO / HAPANA.
14. Kulingana na Mathayo 7:21, Je, tunaweza kufika mbinguni kwa kufanya chochote tunachotaka kufanya? NDIYO / HAPANA
15. Je, 1 Wathesalonike 5:21 na 1 Yohana 4:1 zinafundisha kwamba tunapaswa “kujaribu” kila kitu ambacho tunafundishwa ili kwamba tuone kama kimetoka kwa Mungu? NDIYO / HAPANA
16. Kwenye Mdo 17:11, Wakristo wa Beroye “walichunguza” ili waone kama Paulo alikuwa akifundisha vitu kutoka kwa Mungu kwa _____
_____.
17. Warumi 12:2 inafundisha kwamba hatupaswi kufuatisha mambo ya _____ bali katika mapenzi ya _____.



UTEGEMEZI WA MWANADAMU KWA YESU

Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba, mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyaifanya, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga, mvua ikanyesha, mafuriki yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa. (Mathayo 7:24-27).

...Huyu ni mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye! (Mathayo 17:5).

Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli, tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru. Wakamjibu, sisi tu uzao wa Ibrahimu, wala hatujawa watumwa wa mtu wakati wote; nawe wasemaje, Mtawekwa huru? Yesu akawajibu, Amin, amin, nawaambia, kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi. Wala mtumwa hakai nyumbani siku zote, mwana hukaa siku zote. Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli” (Yohana 8:31-36).

Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli na uzima, mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi” (Yohana 14:6).

Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma (Yohana 17:3).

Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima wa milele kwa jina lake (Yohana 20:30-31).

Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya: Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua; mtu huyu alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake tangu zamani, ninyi mlimsulubisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamwua (Mdo. 2:22-23).

Maana katika yeye unakaa ukamilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili (Wakolosai 2:9).

VITU VYA KUFIKIRIA... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI


18. Je, Mdo 2:22-23 inafundisha kwamba alimpima Yesu (alimthibitisha kuwa ni wa kweli au halisi) kupitia miujiza, maajabu na ishara ambayo watu wanaomzunguka waliiona? NDIYO / HAPANA.
19. Kulingana na Yohana 17:3, uzima wa milele unapatikana kupitia kumfahamu _____ na _____.
20. Katika Mathayo 7:24-27, Yesu anafundisha kwamba kama tukisikiliza na kutii _____, lakini kama sivyo, _____.
21. Katika Mathayo 17:5, Mungu alisema tunapaswa kumsikiliza Yesu? NDIYO / HAPANA.
22. Yohana 8:31 inafundisha kwamba kama tutadumu katika neno la Kristo, tutaifahamu _____.
23. Yohana 8:33-36 inafundisha kwamba Yesu ana uwezo wa kutuweka _____.
24. Je, Yohana 14:6 inafundisha kwamba njia pekee ya kwenda kwa Mungu Baba ni kwa kupitia Yesu? NDIYO / HAPANA

MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA CHIMBA ZAIDI yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.



Tafuta Ukweli

KUHUSU KANISA



Kanisa la Kristo
(church of Christ)

Sura ya 4

Neno kanisa limetumiwa ipasavyo zaidi ya mara mia moja katika Agano Jipya. Ni hakika hili ni neno la muhimu, lakini linamaanisha nini hasa? Je, kanisa ni sehemu tu ya kuabudia? Je, ni jumla ya madhehebu yote ya kidini? Au je, ni kitu tu cha mtu binafsi au cha kiroho? Na zaidi mno, je, kanisa lina umuhimu gani? Na, je, Yesu analo kanisa ambalo tunapaswa kuwa sehemu yake ili tuweze kuokolewa?

UTANGULIZI

Je, unapofikiria kuhusu kanisa, unafikiria kuhusu jengo? Watu wengi hufikiria hivyo. Hata kamusi inalifafanua neno “kanisa” kama “jengo lililotengwa au lililowekwa wakfu kwa ajili ya ibada ya jumuiya” (*Webster’s New World Dictionary*).

Lakini je, kanisa ni jengo tu lililojengwa kwa mbao au mawe? Au kuna kitu cha zaidi? Kwa hakika kipo, kwa sababu kanisa – kama lilivyoanzishwa na Yesu Kristo lilikuwepo muda mrefu kabla hata ya kuwako kwa jengo lolote, dhehebu, au taasisi yoyote ya kikristo kuanzishwa. Sasa basi, kanisa ni nini, na nia zetu dhidi ya kanisa zinapaswa kuwaje? Kadiri tunavyotafuta katika maandiko (Biblia – neno la Mungu, na chanzo chetu cha mamlaka kwa ajili ya ukweli), hebu tuone tutagundua nini kuhusu “kanisa.”

Katika kuutafuta ukweli kuhusu kanisa, tunahitajika kujibu maswali matatu muhimu:

1. Je, kanisa ni nini?
2. Je, kanisa ni la muhimu?
3. Je, kanisa linapaswa liwe na umoja?

JE, KANISA NI NINI?

Kwanza, tunapaswa kujiuliza, “Je, kanisa ni nini? Neno “kanisa” linaleta akilini vitu mbalimbali kwa watu mbalimbali. Neno la Kiyunani *ekklesia* kwa kawaida linatafsiriwa kama “kanisa” na lina matumizi ya muhimu katika sheria za Agano Jipya.

Katika akili za watu wengi, kanisa ni jengo. Neno la Kiyunani linalotafsiriwa “kanisa” katika lugha ya Kiswahili kwenye Agano Jipya linatokana na neno linalo maanisha “walioitwa kutoka” likizungumzia watu. Moja kati ya fafanzu bora ninazozifahamu za “kanisa” zinapatikana katika Mdo. 8:1 na Mdo. 9:1. Katika Mdo. 8:1, inasema kwamba Paulo aliliudhi “kanisa.” Katika Mdo. 9:1, tunasoma pale Paulo alipokuwa akiwaudhi/akiwatesa “wanafunzi wa Bwana.” Hivyo basi, “kanisa” na “wanafunzi wa Bwana” ni kitu kimoja.

Keith Mosher Sr.
Mkufunzi na mhudumu wa Biblia

Ndani ya Agano Jipya, neno “kanisa” lina maana ya muhimu na limefafanuliwa kwa mapana zaidi. Limetajwa

kwanza katika injili ya Mathayo, ambapo kwenye sura ya 16 tunamuona Petro akimtangaza Yesu kama Kristo na Mwana wa Mungu. Katika kuitikia kwenye uthibitisho wa Petro, hebu tuangalie kile Yesu alichotuambia:

Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda. Nami nitakupa wewe funguo za ufalme; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni. (Mathayo 16:18-19).

Kadiri tunavyojitahidi kuelewa maana ya neno “kanisa,” tunapaswa kuangalia mambo matatu kuhusiana na kile Yesu alichokisema:

1. Kristo angelikuwa na kanisa.
2. Yesu angelikuwa mjenzi wa kanisa lake.
3. Petro (pamoja na mitume wengine – Mathayo 18:18) wangelipewa funguo za ufalme.

Kulingana na hili jambo la tatu, ni muhimu kugundua kwamba *funguo* ni alama/ishara ya mamlaka. Takribani mwaka mmoja tangu Yesu alipotoa ahadi ya kulijenga kanisa lake, tunamwona Petro na mitume wengine wakizitumia hizi funguo za *mamlaka* kufungua milango ya ufalme kwenye kuanzishwa kwa kanisa.

Hili tukio lilitokea siku ile ile Wayahudi walipokuwa wakisherehekea Pentekoste, na limeandikwa na mwandishi aliyevuviwa, Luka katika Mdo. 2. Kama tunavyosoma katika sura hii, tunaona kwamba mitume kumi na wawili walipokea nguvu kutoka juu wakati walipomwagiwa Roho Mtakatifu walipokuwa wakisubiri katika ile nyumba kule Yerusalemu. Huku kumwagiwa Roho kwa mitume kuliko tabiriwa na nabii Yoeli kulikuwa ni miongoni mwa vitu vingine, ishara kwamba Mungu yu karibu kuanzisha ufalme wake (Yoeli 2). Wakiwa hata hawajajifunza baadhi ya lugha zilizotajwa katika Mdo. 2:9-11, hata hivyo mitume walikuwa na uwezo wa kuhubiri Injili ya Kristo katika lugha mbalimbali za wanadamu kwa watu waliowakilishwa na baadhi ya haya makundi ya kikabila na kitaifa. Huu ujumbe wa Injili ulikuwa na yafuatayo: (a) rejea ya unabii wa Agano la Kale uliotabiri kuhusu Roho Mtakatifu (ambao ulitamilika katika siku ile); (b) ufupisho wa sifa za Bwana; (c) ujumbe kuhusu maana na umuhimu wa kifo, maziko na ufufuo wa Kristo; na (d) ufunuo kuhusu kukwezwa kwa Kristo katika kiti cha enzi cha Daudi. Kutokana na kuisikia hii hotuba,

Kuhusu Kanisa

mioyo minyofu na nafsi zilizoguswa ambazo zilikuwa katika hitaji la wokovu zilipaza sauti kwa imani, zikisema: “Tutendeje, ndugu zetu?” (Mdo. 2:37). Hiki ndicho kile Petro alichowaagiza wakifanye ili kupokea msamaha wa dhambi zao:

...Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie (Mdo. 2:38-39).

Mungu aliwaita na bado anawaita wenye dhambi leo watubu na kubatizwa. Lakini soma kile Luka mwandishi wa kitabu cha Mdo anachosema kuhusu kile kilichotokea kadiri Petro alivyoendelea na hotuba yake.

Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya, akisema, jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi. Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu (Mdo. 2:40-41).

Angalia tena kwamba wenye dhambi waliambiwa wabatizwe na kwamba ubatizo ungelikuwa “kwa ajili ya ondoleo la dhambi.” Wale waliolipokea lile Petro alilolisema walibatizwa, na muda huo huo walisamehewa dhambi zao – kama vile Mungu alivyoahidi. Waliokolewa. Lakini kutokana na kubatizwa, walifanyika kuwa sehemu ya nini? Je, walijiunga na dhehebu fulani? Soma tena kile Luka anachokisema kadiri anavyofunua kupitia Roho Mtakatifu, kile kilichotokea siku ile takribani miaka elfu mbili iliyopita:

Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu. Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa (Mdo. 2:41,46-47).

Je, umegundua kile Luka anachosema kilitokea? Wale waliokuwa wakibatizwa walizidishwa kwenye idadi ya wale waliokolewa, na wale waliokolewa walizidishwa katika kanisa. “Hawakujiunga na kanisa walilolichagua wenyewe.” Wala hawakufanyika kuwa sehemu ya dhehebu, kwa sababu, hata hivyo hapakuwa na dhehebu lolote wakati huo. Badala yake, kama wenye dhambi walibatizwa, waliokolewa. Na wakati huo huo Kristo alikuwa akiwazidisha pamoja na wale aliokwisha kuwaokoa. Kwa pamoja, wale wote waliokolewa waliunda kile kilichofahamika kama “kanisa” (Mdo. 2:47). Kwa kuweka wazi zaidi, “kanisa” ni muunganiko wa wale wote waliokolewa, na “waliokolewa” wanaunda kile kinachofahamika kama “kanisa.” Kwa ufupi,

“kanisa = “waliokolewa”

Katika kitabu chote cha Matendo ya Mitume (na sehemu iliyobaki ya Agano Jipya) utaona kwamba hawa watu waliokolewa wanatambuliwa hasa katika njia hii – nayo ni, kama “kanisa.” Neno “kanisa” limetumika likiwarejea hawa watu waliokolewa katika moja kati ya njia tatu. Kwanza, “kanisa” limetumika katika dhana ya *mahali fulani* (kama katika “kanisa lililoko Yerusalemu”). Pili, limetumika katika dhana ya *mahali kote/popote* likirejea watu waliokolewa ulimwenguni kote (kama katika “Kristo alilipenda kanisa”). Tatu, limetumika katika dhana *maalum* (kama katika dhana ambayo Biblia inazungumzia waliokolewa wakikutanika pamoja kwa ajili ya ibada). Katika dhana zote tatu, neno “kanisa” linazungumzia wale waliokolewa.

- **Mahali fulani (“kanisa lililoko Yerusalemu” - Mdo 11:22)**
- **Mahali kote/popote (“Kristo pia alilipenda kanisa” - Waefeso 5:25)**
- **Maalumu (“katikati ya kanisa nitakuambia sifa” – Waebrania 2:12)**

Walioliunda kundi walifahamika kama “Waliokolewa” wanatambulishwa katika maandiko kwa maelezo na maana mbalimbali, ambazo kila moja wapo inatusaidia kuelewa asili na kazi za waliokolewa. Baadhi ya maelezo yametumika kuelezea neno “waliokolewa” kama ifuatavyo:

Kanisa (“walioitwa” Mathayo 16:18)

Kama vile neno la Kiyunani kwa ajili ya kanisa linavyojieleza, waliokolewa ni wale “walioitwa watoke” – wameitwa kutoka katika ulimwengu wa giza, na kuingia katika nuru ya kiroho ya Mungu (1 Petro 2:9; Wakolosai 1:13; Warumi 13:12).

Ufalme (Wakolosai 1:13)

Tunapofikiria kuhusu ufalme, kwa hakika tunafikiria

Waliokolewa:

**Kanisa
Ufalme
Hekalu
Nyumba ya Mungu
Mwili**

Sura ya 4

kuhusu mfalme na wananchi waatiifu ambao ni watumishi ndani ya ufalme. Kama watu waliookolewa, wakristo wanaishi chini ya utawala wa kifalme wa Yesu. Wapo chini ya sheria na utawala wa Mfalme Kristo (1 Timotheo 6:15; Ufunuo 17:14).

Hekalu (1 Wakorintho 3:16)

Katika tamaduni za kipagani, hekalu liko katika dhana za kawaida kama maskani au nyumba kwa ajili ya mungu. Katika Biblia, tunajifunza kwamba Mungu pekee wa kweli na anayeishi hukaa ndani ya kanisa. Roho wake Mtakatifu hufanya makao ndani ya kila mkristo (2 Wakorintho 6:16).

Nyumba ya Mungu (Waefeso 2:19)

Katika Agano Jipya, neno “nyumba” mara kwa mara linarejea umoja wa kifamilia ulio na baba, mama, dada na kaka. Katika hali hiyo hiyo, kanisa linapaswa kufikiriwa kama familia – tukiwa na Mungu kama Baba yetu wa mbinguni, Kristo kama kaka yetu mkubwa, na waliookolewa kama ndugu na dada zetu (Mathayo 12:48-50; Yohana 20:17; Waebrania 2:10-13).

Mwili (Wakolosai 1:24)

Kama vile mwili wa mwanadamu ulivyo na kichwa kimoja lakini viungo vingi, hivyo hao waliookolewa wanaye ambaye ndiye kichwa chao Yesu Kristo, pamoja na viungo mbalimbali vya mwili kama wakristo binafsi. Kama vile mwili wa mwanadamu unavyofanya kazi kwa ufanisi pale viungo vyote vinapofanya kazi kwa pamoja kama kiungo kimoja, Hivyo basi kanisa ni mwili mmoja unaodhihirisha umoja (Waefeso 4:4; Warumi 12:1-5; 1 Wakorintho 12:12-26).

Kwa hakika, ni kudhihirika huku, mwili, unaoanishwa na rejea kutoka 1 Wakorintho 12:27, kwa hiyo hilo linaweka wazi kabisa kwamba *kanisa ni waliookolewa – watu waliotakaswa ambao ni mali ya Kristo*.

Sikiliza kile Paulo alichokiandika kwa waliookolewa walioko Kolosai na Korintho:

Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja pekee yeye. (1 Wakorintho 12:27)

...tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake (Wakolosai 1:24).

Mwili na kanisa ni kitu kimoja. Na kwa sababu hili ni la kweli, Paulo alikuwa na uwezo wa kuwataja wakristo waliopo Korintho kama “mwili wa Kristo.” Wale wakristo katika mji ule walifahamika kama “kanisa.”

Walikuwa ni kanisa la Kristo katika jamii ile. Hivyo basi, katika kulijibu swali linalosema, “Je, Kanisa ni nini?” tunapaswa kuhitimisha kwamba kanisa si jengo au mahali

fulani kwa ajili ya ibada. Bali, *kanisa ni kundi la watu waliookolewa ambao ni mali ya Mungu*.

Kwa kufafanua kwa undani asili na umuhimu wa kanisa, hebu tuangalie kifungu cha ziada kilichopo ndani ya waraka ulioandikwa na mtume Paulo kwa muinjilisti kijana ajulikanaye kama Timotheo.

Nakuandika hayo nikitaraji kuja kwako hivi karibu. Lakini nikikawia, upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli (1 Timotheo 3:14-15).

Wakati Paulo anapotaja neno “nyumba ya Mungu,” je, alikuwa akizungumzia nyumba *halisi*? Hapana! Alikuwa akizungumzia nyumba ya *kiroho* nayo ni kanisa.

Kanisa, nyumba ya Mungu, ilijengwa juu ya mwamba imara wa uungu wa Bwana (Mathayo 16:13-19). Baada ya Petro kutoa ukiri wake mkuu kuhusu uungu wa Kristo, Yesu alisema, “juu ya mwamba huu, nitalijenga kanisa langu...” Kulingana na Waefeso 2:20, Yesu ni jiwe kuu la pembeni, na mitume na manabii wake watakatifu ndiyo msingi. Kutoka 1 Petro 2:5, tunajifunza kwamba wakristo ni *mawe yaliyo hai* ambao katika wao nyumba ya kiroho hujengwa. Kulingana na 1 Timotheo 3:15, kanisa ni “nguzo na msingi wa kweli.” Kama hivyo, kanisa linabeba wajibu wa kwenda ulimwenguni kote kuhubiri ukweli – habari njema za Kristo, ambaye ndiye mlango ambao kwao wanadamu wanapaswa kuingia ili wapate uzima wa milele. Kuuelekea mlango huo kuna hatua za wokovu, ambazo kila mwenye dhambi ni lazima azipitie ili aweze kuingia kanisani.

Huu sasa, ndio muundo wa nyumba ya Mungu – jumla ya wakristo waliojengwa juu ya Yesu kama jiwe kuu la pembeni, na juu ya msingi wa mitume na manabii. Sasa tunauliza tena, “Je, kanisa ni nini?” Kanisa ni:

Kanisa ni:
Waliookolewa
Mwili wa waumini
waliobatizwa
Mwili wa Kristo
Ufalme wa Mungu
Nyumba ya Mungu
Hekalu la Mungu

Nyumba ya Mungu ya Kiro “KANISA”

Mitume na Manabii

Msingi

Waefeso 2:20

Juu ya Mwamba Huu Nitajenga Kanisa Langu

Uungu wa Kristo

Mathayo 16:13-18

Yesu, Jiwe Kuu

la Pembeni

Waefeso 2:20


oho

Wakristo
Mawe Yaliyo Hai
1 Petro 2:5

Ukweli
1 Timotheo 3:15

Yesu
Ndiye Mlango
Yohana 10:9

Ubatizo (Marko 16:16)
Kukiri (Warumi 10:9-10)
Tubu (Luka 13:3)
Amini (Yohana 8:24)
Sikia (Yohana 6:45)



Kuhusu Kanisa

SEHEMU YA MARUDIO: JE, KANISA NI NINI?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Neno la Kiswahili “kanisa” limetafsiriwa kutoka katika lugha ya Kiyunani linalomaanisha “_____.”
2. Kulingana na mstari hapo chini, je, maneno “kanisa” na “wanafunzi wa Bwana” yanafanana na ni kitu kimoja? NDIYO/HAPANA
Siku ile kukatukia adha kuu ya kanisa lililokuwa katika Yerusalemu, wote wakatawanyika katika nchi ya Uyahudi na Samaria, isipokuwa hao mitume (Mdo 8:1)
Lakini Sauli, akizidi kutisha na kuwaza kuwaua wanafunzi wa Bwana, akamwendea kuhani mkuu (Mdo 9:1)
3. Kulingana na Mathayo 16:18, Je, Yesu aliahidi kulijenga kanisa lake? NDIYO/HAPANA
4. Kulingana na Mdo 2:41 na 46-47, Je, kanisa la Kristo lilianza siku ya Pentekoste kufuatia ufuko wake? NDIYO/HAPANA
5. Je, ujumbe wa injili uliohubiriwa siku ya Pentekoste ulijumuisha maelekezo yanayohusu maana na umuhimu wa kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Kristo? NDIYO/HAPANA
6. Kulingana na Mdo 2:38, kwenye siku ile ambayo Yesu alilianzisha kanisa lake mtume Petro alisema yafuatayo, “Tubuni _____ kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate _____” (Mdo 2:38).
7. Kulingana na Mdo 2:47, Bwana “akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa _____” (Mdo 2:47).
8. Neno “kanisa” linazungumzia mjumuiko watu wote _____.
9. Je, misemo kama vile “ufalme,” “nyumba ya Mungu,” na “mwili,” ni maneno ambayo yanayozungumzia “kanisa”? NDIYO/HAPANA
10. Kulingana na 1 Timotheo 3:14-15, Paulo alisema, “Nakuandikia ili kwamba upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika _____, iliyo _____ la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli.”
11. Kulingana na mistari hapo chini, Je, kanisa limejengwa juu ya msingi wa uungu wa Kristo (ukweli kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu)? NDIYO/HAPANA

Sura ya 4

Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria-Filipi, akawauliza wanafunzi wake akisema, "Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?" Wakasema, "Wengine hunena u Yohana Mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yereimia au mmojawapo wa manabii." Akawaambia, "Ninyi mwaninena mimi kuwa ni nani?" Simoni Petro akajibu akasema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai." Yesu akajibu, akamwambia, "Heri wewe Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda. Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni" (Mathayo 16:13-19).

12. Kulingana na mstari hapo chini, akizungumzia nyumba ya Mungu ya Kiroho, kanisa, mtume Petro alisema yafuatayo, "Ninyi nanyi, kama _____, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu."

Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo (1 Petro 2:5).

13. Angalia mchoro/picha iliyopewa jina la *Nyumba ya Mungu ya Kiroho: Kanisa*, na ujibu maswali yafuatayo:
- Je, ni nani ambaye ndiye jiwe kuu la pembeni la nyumba ya Mungu, kanisa? _____
 - Je, ni nani ambaye ndiye mlango ambao wenye dhambi wanapaswa kuingia ili waweze kuingia kanisani? _____
 - Kabla ya kuingia mlangoni, je, ni hatua gani ambazo zinaelekeza wokovuni/kanisani? _____, _____, _____, _____.

Sehemu ya MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA inapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAZUNGUMZO

- A. Kulingana na Mdo 2:38 na mistari hapo chini, mtu anapaswa kubatizwa ili aweze kuokoka. Je, wewe umeshawahi kubatizwa kwa ajili ya msamaha wa dhambi zako? NDIYO/HAPANA
- Aminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa (Marko 16:16).*
- Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo (1 Petro 3:21).*
- B. "Kanisa" linaundwa na "waliookolewa." Je, wewe ni mshiriki wa kanisa la Kristo, na kwa hiyo umeokoka? NDIYO/HAPANA

Kuhusu Kanisa

- C. Je, unataka kufanyika kuwa sehemu ya mwili wa Kristo, kanisa, na kwa hilo uweze kuokolewa kutoka katika madhara ya dhambi? NDIYO/HAPANA

MASUALA YA KUZUNGUMZA

- A. Je, ni kwa nini ni muhimu kwa watu wanaotaka kwenda mbinguni kuwa washiriki wa kanisa la Kristo?
- B. Je, Paulo anamaanisha nini alipoandika kwamba kanisa ni “nguzo na msingi wa kweli” (1 Timotheo 3:14-15)?
- C. Je, ni kwa nini wengi wanaamini hili wazo la uongo kwamba kanisa ni jengo tu?



JE, KANISA NI LA LAZIMA NA MUHIMU?

Hebu sasa tujiulize, “Je, kanisa ni la lazima na muhimu?” Je, mtu anapaswa awe mshiriki wa kanisa ili aweze kuokolewa? Je, mtu anaweza “kuwa tu na uhusiano binafsi na Yesu,” na pasiwe na umuhimu wa yeye kujihusika katika kanisa? Mara kadhaa, unaweza ukamsikia mtu akisema, “Nipe Yesu, lakini usinipe kanisa,” au “Nipe mwanadamu, lakini usinipe mpango.” Unaweza pia ukasikia mtu fulani akisema hakuna ulazima wa mtu kuwa mshiriki wa kanisa ili aweze kwenda mbinguni. Lakini je, maelezo hayo ni sahihi/ya kweli?

Katika waraka ulioandikiwa kanisa lililoko Efeso, mtume Paulo alifunua ni jinsi gani kanisa lilivyo la lazima (na la thamani) kuhusiana na uhusiano wako na Mungu.

Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu ya Yesu Kristo. Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani. Akawapataniha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa ule msalaba (Waefeso 2:13-16).

Kulingana na Paulo, mgawanyiko na utengano ambao ulikuwepo kati ya Mungu na mwanadamu (pamoja na ule ulikuwepo kati ya Wayahudi na Mataifa) umeondolewa kupitia kanisa. Kutoka katika Isaya 59:1-2 na Warumi 6:23, tunajifunza kwamba dhambi ilileta utengano kati ya Mungu na mwenye dhambi. Pia Biblia inafundisha kwamba kwa

sababu ya dhambi, tunafanyika kuwa maadui wa Mungu. Lakini kwa sababu ya habari njema za Yesu na kifo chake msalabani, sisi sote tunafanyika kuwa *marafiki wa Mungu na kupatanishwa na upendeleo wa upendo wake.*

Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake. Wala si hivyo tu, ila pia twajifurahisha katika Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye sasa tumeupokea huo upatanisho (Warumi 5:10-11).

TUKI inafafanua neno “upatanisho” kama: “kurejeza kuunganisha na urafiki baada ya usuluhishi.” Kwa hiyo, upatanisho, ni neno linalotumika kuelezea sehemu mbili zilizotengana au vikundi viwili vilivyogombana vinaletwa pamoja na kuunganishwa, na kufanywa kuwa kimoja. Kutoka katika Waefeso 2:16, tunajifunza kwamba upatanisho unapatikana “katika mwili mmoja” wa Kristo. “Mwili” huo ulielezewa na Paulo kama “kanisa” aliposema kwamba Mungu alimweka Kristo “awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa, ambalo ndilo mwili wake” (Waefeso 1:22-23).

“Mwili wa Kristo” (wa waumini) na “kanisa” ni kitu kimoja na kinafanana. Hivyo basi, kama unataka kuokoka kwa kupatanishwa na Mungu, unapaswa kuwa “ndani ya mwili”- ambayo hata hivyo, ni sawa na kusema ni lazima uwe “ndani ya kanisa.” Kwa hiyo, ndiyo, kama unataka kupatanishwa na Mungu, unapaswa kuwa ndani ya mwili wa Bwana, kanisa. Ili uweze kuokolewa, unapaswa kuwa ndani ya Kanisa.

Kama ukiendelea kuchunguza katika kitabu cha Waefeso, utagundua sababu nyingine zinazohusiana na ni kwa nini

Sura ya 4

kanisa ni la lazima na muhimu. Paulo aliandika:

Mimi, niliye mdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote, nalipewa neema hii ya kuwahuribiri Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika; na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote; ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho; kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu (Waefeso 3:8-11).

Kutoka katika kifungu hiki, tunaweza kuangalia mambo mawili muhimu. Kwanza, angalia kwamba *kanisa ni mfano (au lina akisi) wa hekima ya Mungu*. Kutoka katika mpangilio wake mpaka kwenye mfumo wake wa kipekee wa kuabudu, *kanisa ndilo taasisi kuu kuliko zote iliyowahi kuanzishwa*. Moja kati ya vitu ambavyo linalifanya liwe la kipekee ni muingiliano wake wa kitamaduni na muingiliano wake wa ushirika wa kitaifa. Katika Waefeso, Paulo alifunua kwamba utengano umetokea miongoni mwa wanadamu – utengano kati ya Wayahudi na Mataifa. Paulo aliutaja huu utengano mwanzo kabisa katika Waefeso 2:14 alipozungumzia uwepo wa “kiambaza cha kati kilichotutenga.”

Kiambaza ambacho Paulo anakizungumzia katika Waefeso 2:14 kilikuwa, katika mtazamo mmoja, kiambaza halisi. Kiambaza kilijengwa ndani ya himaya

ya Herodea. Kilikuwa kimewekwa ili kuwazuia Mataifa kuingia katika sehemu ya ndani ya hekalu na sehemu zake za ndani. Kile tunachopaswa kukielewa ni kwamba mataifa hawakupewa, hawakuwa na ushirika wa kweli na Wayahudi kama matokeo ya kizuizi hiki. Si hivyo tu, bali ilikuwa ni ishara ya ukweli kwamba Mataifa hawakupewa uwezo wa kumfikia Mungu sawa na baraka zake za rohani pamoja na ahadi zilizopo chini ya Agano la Kale.

Alfred Washington
Mhudumu

Kuondolewa kwa kile kizuizi au “kiambaza cha kati kilichotutenga” kilitabiriwa na manabii wawili wa Agano la Kale, Isaya na Danieli. Wote wametabiri kuhusu mpango wa Mungu wa kukiondoa kiambaza ili kuondoa utengano kati ya Wayahudi na Mataifa kwa kupitia kifo cha Kristo msalabani, na kwa kupitia ufalme wa Mungu, kanisa.

Paulo, katika Waefeso 2, alielezea wazo kwamba kupitia kazi ya ukombozi ya Yesu Kristo, hiki “kiambaza cha kati kilichotutenga” kimeondolewa. Sasa, Wayahudi na Mataifa wanafursa sawa ya kupata baraka za rohani na ahadi za Mungu. Bila kujali utaifa, matabaka ya kijamii, au uhusiano wa kisiasa, kiwango cha elimu, au jinsia, sote tunapata fursa ya kumwendea Mungu kupitia mwili wa Kristo, ambao ndiyo kanisa lake.

Alfred Washington
Mhudumu



Kuhusu Kanisa

Kanisa hili, linajumuisha jumla ya watu wote ambao watazidi utaifa na ukabila. Kanisa, kama ufalme wa Mungu, utaundwa na watu kutoka ulimwenguni kote. Au, kama Isaya alivyoliweka, “na mataifa yote watauendea” (Isaya 2:2).

Katika kanisa la Kristo haijalishi rangi ya ngozi yako ni ya aina gani au ulizaliwa wapi. Haijalishi ama wewe ni wakiume au wakike, tajiri au maskini, msomi au si msomi. Kanisa ni familia. Kanisa – kama linafuata mpango wa Mungu - ni mfano wa jinsi watu wote wa mataifa na tamaduni mbalimbali wanavyoweza kukaa pamoja kwa amani na kupatana.

Leo, wakati mtu (kupitia imani kwa Yesu) anapobatizwa katika Kristo, pale ndipo anapomvaa Kristo, na kufanyika kuwa sehemu ya familia ambapo mipaka ya utaifa au ujamaa vinaondolewa:

Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu (Wagalatia 3:27-28).

Kanisa ni mfano ung’ao wa jinsi ya kuwaleta watu pamoja. Kupitia kubatizwa katika Kristo, watu wa mataifa na tamaduni zote wanafanywa kuwa wamoja. Wanafanyika kuwa sehemu ya ndugu ambao umeondoa kabisa tofauti za kiuchumi au za kisiasa. Kama familia, kanisa huonesha kuwajali kwa dhati washiriki wake wote.

Kulingana na Biblia, kanisa ndipo mahali uwepo wa umoja, ukarimu na roho ya upendo vilipo (Mdo. 2:44-46; 4:32-35). Kanisa ni mbingu ya furaha na mapenzi mema – hasa kwa wale waliotelekezwa au kutendewa vibaya na familia zao za kimwili – wakiwa na ndugu wengi, dada, baba na mama wanaosaidia kulea na kutunza wale walio wachanga kiroho.

Kanisa kwa hakika linaakisi hekima ya Mungu iliyodhihirishwa. Na tunapaswa kumshukuru Mungu kwa ajili hiyo! Lakini kanisa halioneshi hekima ya Mungu tu. Tunajifunza kutoka katika Waefeso 3:11 *kwamba kanisa ni la lazima kwa sababu wakati wote limekuwa ndani ya mpango wa Mungu wa milele*. Lilikuwepo ndani ya nia yake kabla hata ya kuumbwa kwa ulimwengu. Kanisa si kama wengine wanavyokosea kwa kufundisha kwamba lilikuwa ni “wazo la baadaye” au “uamuzi wa mwisho” uliofanywa na Bwana wakati aliposhindwa kuanzisha ufalme wa kidunia.

Badala yake tunajua kutoka katika maandiko kwamba kanisa:

Kanisa na ufalme, kama tulivyojifunza hapo mwanzo, ni kitu kimoja na vinafanana. Ufalme umepangwa na Uungu,



lilitabiriwa na manabii, lilibashiriwa na Yesu na lilianzishwa na Mungu. Haya yote yalitokea kulingana na mpango kamili ambao tumeuona ukamilifu wake katika karne ya kwanza, na ambao bado unatambuliwa hata leo.

Ufalme, kama ulivyofunuliwa katika Biblia, ulitokea katika karne ya kwanza (Wakolosai 1:13; 2 Wathesalonike 1:5; Ufunuo 1:9). Kulingana na nabii Danieli, ulipaswa kuanzishwa wakati wa siku za dola ya Kirumi.

Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele (Danieli 2:44).

Kutoka katika mazingira ya kifungu hiki, tunajifunza kwamba kishazi “katika siku za wafalme hao” kwa uwazi kabisa kinazungumzia dola ya Kirumi. Danieli ametabiri kwamba dola nne za ulimwengu zitakazokuwa na mafanikio (Babeli, Waajemi-Waamedi, Wayunani na Warumi) ambao watautawala upande wa Palestina. Ili kuwa ni wakati wa dola ya nne – ambayo historia inaielezea kama dola ya Kirumi pamoja na watawala au wafalme wake – kwamba kanisa la Kristo (“ufalme wa Mungu”) utanzishwa.

Wakati wa karne ya kwanza, ndipo mpando wa Mungu ulipodhihirishwa. Ufalme wa Kristo ulianzishwa. Na kwa kulisoma Agano Jipya, tunaona kwamba wanaume na wanawake wa mataifa yote walikaribishwa ili waingie, na kufanyika kuwa sehemu yake. Hivyo, kwa hakika, kanisa ni la muhimu. Ni sehemu ya muhimu ya mpango wa kumkomboa mwanadamu.

Lakini hebu tuangalie kwa undani zaidi katika kitabu cha Waefeso ili tuweze kujifunza zaidi kuhusu umuhimu na ulazima wa kanisa:

Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe; kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili enyi waume, wapendeni wake zenu,

Kitabu cha Danieli na Ufalme wa Mungu (Kanisa)

DOLA ZA ZAMANI ZA MESOPOTOMIA
NA MEDITERENIA

UNABII WA DANIELI
NA TAFSIRI

DHAHABU

Babeli

(625 K.K – 539 B.K)

"Na sanamu hii kichwa chake kilikuwa cha dhahabu safi ... na Mungu wa mbinguni amekupa ufalme ... Wewe (Nebukadreza wa Babeli) u kichwa kile cha dhahabu."
(Danieli 2:32, 37, 38, pia 1:1)

FEDHA

Umedi–Uajemi

(539 K.K – 331 B.K)

"Kifua chake na mikono yake ni ya fedha ... na baada ya zamani zako (Nebukadreza) utainuka ufalme mwingine mdogo kuliko wewe."
(Danieli 2:32, 39, pia 8:20)

SHABA

Uyunani

(331 K.K – 63 B.K)

"tumbo lake na viuno vyake ni vya shaba ... na ufalme mwingine wa tatu wa shaba, utaitawala dunia yote."
(Danieli 2:32, 39, pia 8:21)

CHUMA NA
UDONGO

Rumi


(146 K.K – B.K 476)

"miguu yake ni ya chuma; na nyayo za miguu yake nusu ya chuma na nusu ya udongo ... na ufalme wanne utakuwa na nguvu mfano wa chuma; ...bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu."
(Danieli 2:33, 40, 42, 43)

Ufalme wa Mungu Ulianzishwa (takribani 33 B.K)

"Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele; wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele." (Danieli 2:44).

Agano Jipya linafunua kwamba Yesu na Yohana Mbatizaji walihubiri kuhusu kuanzishwa kwa ufalme wa Mungu kwa kusema "umekaribia" (Mathayo 3:2; 4:17, 23). Kutokana na kwamba kanisa na ufalme ni kitu kimoja (Mathayo 16:18-19; Marko 9:1; Mdo 1:3; 2:38, 47; 8:12; Wakolosai 1:13), na kanisa lilianzishwa katika karne ya kwanza katika siku za utawala wa dola ya Kirumi, maana yake ni kwamba ufalme wa Mungu ulianzishwa katika karne ya kwanza kutokana na huduma ya duniani ya Yesu. Kanisa/ufalme linaundwa na watu kutoka mataifa yote (Isaya 2:1-2) na hivyo kuziangamiza "falme hizi zote" (Danieli 2:44) na linazungumziwa katika Agano Jipya kwamba lilianzishwa kwenye karne ya kwanza B.K (Wakolosai 1:13, 2 Wathesalonike 1:5; Ufunuo 1:9). Ufalme huu bado upo leo, na wenye dhambi wote waliotubu wanaweza kuchagua kufanyika sehemu yake kwa kuzamishwa ndani ya Kristo. Yesu, akiwa kichwa cha kanisa lake na Mfalme wa wafalme wote (Wakolosai 1:18; 1 Timotheo 6:15), sasa anatawala katika ufalme wake – watu wake (Mdo. 2:36; Luka 17:21).



Kuhusu Kanisa

kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake (Waefeso 5:23,25)



Kuna ukweli wa muhimu wa aina mbalimbali unaofunuliwa katika kifungu hiki. Lakini katika dhana hii ya swali letu kuhusu umuhimu wa kanisa, hebu tuangalie kwa makini katika ukweli wa muhimu wa aina mbili: Kristo analipenda kanisa, naye ndiye Mwokozi wa mwili. Kama Kristo (mfano wetu mkuu) alilipenda kanisa, Je, sisi pia, hatupaswi kulipenda kanisa? Ama kwa hakika! Kanisa la Kristo linapaswa kuwa kitu cha muhimu kuliko vyote katika maisha yetu!

Kwa sababu Kristo alilipenda kanisa kiasi cha kuimwaga damu yake na kulifia, Je, sisi hatupaswi kutaka kuwa sehemu yake? Kwa hakika tunapaswa, kwa sababu Paulo aliandika katika 2 Timotheo 2:10, “wokovu ...ulio katika Kristo.”

Kutokana na kwamba “mwili wa Kristo” ni kitu kimoja na “kanisa la Kristo,” Je, kwa hiyo hatuhitaji kuwa “ndani ya kanisa” (mwili wa Kristo) ili tuweze kuokolewa? Kwa hakika tunahitajika! Tunapaswa kuwa ndani ya mwili wa Kristo ili tuweze kuokolewa.

Ni wazi kabisa kwamba, si tu kwamba kanisa ni la muhimu na la thamani, bali pia linahitajika na ni la lazima.

Hata hivyo sasa, hebu tuangalie kipengele cha mwisho kutoka katika waraka wa Waefeso, ambao utatufikisha katika swali letu kuu la mwisho.

Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja (Waefeso 4:4-5)

Baada ya kumsikiliza Paulo, tunapaswa kuhitimisha kwamba, kama vile kulivyo na Mungu mmoja, Roho mmoja, na imani moja, pia kuna mwili mmoja. Na kutokana na kwamba mwili na kanisa ni kitu kimoja (kama ilivyodhihirishwa katika Waefeso 1:22-23), ni wazi kwamba kuna kanisa moja tu. Yesu aliuzungumzia ukweli huu wakati aliposema, “Juu ya mwamba huu, Nitalijenga kanisa langu, na milango ya kuzimu haitalishinda” (Mathayo 16:18).

Je, Yesu alisema kwamba atayajenga makanisa (wingi) au kanisa (umoja)? Yesu alisema kwamba atalijenga kanisa lake (umoja). Lakini bado, leo kuna makanisa mengi mbalimbali. Mengi kati yake yana majina ambayo ni tofauti na mengine. Pia, yanatofautiana katika kile wanachoamini kuhusu masuala ya maadili, katika kile wanachofundisha kuhusu jinsi ya kufanyika kuwa mkristo, katika kile wanachoamini kuhusu namna ya uongozi wa kanisa, na katika kile wanachofundisha kuhusu jinsi ya kumwabudu Mungu.

Kama ungelichunguza orodha ya makanisa katika eneo lako, ungeligundua kwamba kuna majina na aina nyingi tofauti tofauti za makanisa. Pia, utagundua kwamba miongoni mwa wale wanaodai kuwa ni wakristo, kuna mtengano mkubwa. Je, unafikiri hili linampendeza Mungu? Je, inakubalika kwa Mungu kwa kuwa na makanisa mengi tofauti, pamoja na majina mengi tofauti, wakifundisha vitu vingi tofauti, na kuleta utengano mkubwa?

Je, kanisa ambalo Yesu alilijenga linapaswa kuuvumilia mgawanyiko wa aina hiyo? Je, ina kubalika kuugawanya “mwili mmoja” wa Kristo ili kuanzisha makanisa yaliyoundwa na wanadamu au madhehebu? Je, wakristo wanapaswa kujitenga wenyewe kwa majina tofauti tofauti, mafundisho, au vitabu vya muongozo? Jiulize maswali yafuatayo:

Je, mwili wa Kristo unapaswa kugawanywa?

Je, kanisa linapaswa kuwa na mgawanyiko wa majina mengi?

Je, Kanisa linapaswa kuwa na vitabu vingi vya muongozo?

Je, kanisa linapaswa kufundisha mafundisho yasiyopatikana katika Biblia?

Katika sehemu inayofuata, hebu tujaribu kuyajibu hayo maswali, na haswa swali, “Je, kanisa linapaswa kuwa na umoja?”

KANISA NI LA LAZIMA NA LA MUHIMU:

- Kwa ajili ya wokovu
- Kama mfano wa hekima ya Mungu
- Ndani ya mpango wa Mungu wa milele
- Kwa sababu Kristo alilipenda kanisa
- Kwa sababu lipo limoja tu

SEHEMU YA MARUDIO: JE, KANISA NI LA LAZIMA NA LA MUHIMU?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na Waefeso 3:8-11 na mstari hapo chini, Je, inawezekana mtu akampendeza Mungu kwa kujaribu “kuwa na ushirika binafsi na Yesu,” lakini asijihusishe katika kanisa? NDIYO/HAPANA
Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote. (Waefeso 1:22-23).
Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani. Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba (Waefeso 2:14-16).
2. Kulingana na Waefeso 2:16, Je, wanadamu wenye dhambi wanapatanishwa na Mungu (wanarudishwa tena baada ya kuwa wametengana) katika mwili wa Kristo, kanisa? NDIYO/HAPANA
3. Kulingana na Waefeso 3:8-11, Paulo anaandika, “ili sasa, _____, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho, kwa kadiri ya _____ alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu.”
4. Je, inakubalika kwa Mungu kuwa na ubaguzi au mtu kuleta mawazo yake na kuyalazimisha ya kubaliwe ndani ya kanisa la Kristo? NDIYO/HAPANA.
5. Je, Biblia inafundisha kwamba kanisa lilipangiliwa na Uungu, lilitabiriwa na manabii, lilibashiriwa na Yesu na lilianzishwa na Mungu? NDIYO/HAPANA
6. Wakati wa karne ya kwanza, mpango wa Mungu wa milele ulidhihirishwa. _____ la Kristo lilianzishwa.
7. Kulingana na Waefeso 5:23 na 25, Je, Kristo analipenda kanisa naye ndiye Mwokozi wa mwili? NDIYO/HAPANA.
8. Kulingana na Waefeso 1:22-23, “Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa, ambalo ndilo _____.”
9. Je, ni lazima mtu awe ndani ya kanisa, mwili wa Kristo, ili aweze kuokolewa? NDIYO/HAPANA.
10. Kulingana na Waefeso 4:4-5, kuna mwili zaidi ya mmoja (kanisa)? NDIYO/HAPANA.
11. Kulingana na Mathayo 16:18, Je, Yesu alisema kwamba atajenga kanisa moja (umoja) au makanisa mengi (wingi)? _____.

Kuhusu Kanisa

12. Kulingana na Mathayo 16:18 na Waefeso 4:4, Je, inakubalika kwa Mungu kuwepo kwa madhehebu mbalimbali? NDIYO/HAPANA

MAJIBU kwa ajili ya **MASWALI YA KUJIFUNZIA** yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Je, kanisa ni la lazima na la muhimu? NDIYO/HAPANA
- B. Je, unalipenda kanisa kama Kristo alivyolipenda kanisa? NDIYO/HAPANA
- C. Je, unaamini kwamba Kristo alianzisha kanisa moja tu, na kwamba yeye ndiye kichwa chake? NDIYO/HAPANA
- D. Je, wewe ni mshiriki wa kanisa la Kristo, au mshiriki wa madhehebu yaliyoanzishwa na wanadamu?

MASUALA YA MAZUNGUMZO

- A. Kulingana na Waefeso 2:14, chini ya Sheria ya Kale, “kiambaza cha kati kilichotutenga” kilikuwepo kati ya Wayahudi na Wayunani. Je, ni kwa jinsi gani Kristo alikivunja kiambaza hicho?
- B. Kulingana na Danieli 2:44, nabii Danieli alitabiri “ufalme ambao hautaangamizwa milele,” nao “utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu.” Je, falme hizo zingine ni zipi, na “ufalme ambao hautaangamizwa milele” ambao ulitamiliza kile Danieli alichotabiri ni upi?



JE, NI LAZIMA KANISA LIWE NA UMOJA?

Katika ulimwengu wa leo, kuna utengano miongoni mwa wale wanaodai kuwa wanamfuata Yesu. Kukubali na kuvumilia mgawanyiko huu mara kwa mara unatambuliwa chini ya msingi wa dhana ijulikanayo kama “udhehebu.” Lakini, Je, udhehebu ni nini hasa?

“Udhehebu” kwa kifupi ni kukipa jina kitu fulani. Wakati unapojitenga wewe binafsi na kuingia katika kikundi chochote, basi wewe “umekuwa dhehebu.” Kama ungelimuuliza mtu fulani swali kwamba yeye ni mkristo wa aina gani, angeweza kukuambia, “Mimi ni mkristo wa aina hii.” Atakuonesha kikundi ambacho yeye yupo ndani yake. Kinachotokea hapa ni kwamba udhehebu unaugawanya ukristo katika miili mingi ambayo haiwezekani hata kuitaja yote kwa majina. Mtu fulani alikadiria kwamba kuna makundi zaidi ya 600 katika nchi hii pekee yanayodai kuwa ni “wakristo,” lakini bado yanajiita kwa majina tofauti

kwa sababu yanafuata vitabu mbalimbali vya miongozo, mafundisho mbalimbali, au imani mbalimbali. Kuwa dhehebu ni kujitenga au kulivunja kanisa ambalo Yesu alikufa kwa ajili yake na kulilipia kwa damu yake (Mdo. 20:28).

Keith Mosher Sr.
Mkufunzi na mhudumu wa Biblia

Dhana ya udhehebu – ambayo inazungumzia kujitenga kutoka katika sehemu nzima (kanisa kwa ujumla) kwa kujitambulisha kwa majina fulani au aina fulani ya mafundisho – kwa kuchezea utengano na makundi. Kitu cha kuvutia ni kwamba dhana ya udhehebu haijatajwa mahali popote katika Biblia. Kwa hakika, hata dokezo la utengano unaosababishwa na mafundisho yaliyoundwa na wanadamu, au majina na sifa mbaya za wanadamu, zinakemewa. Angalia kwa mfano, kile kilichokuwa kikitokea katika kanisa la Bwana lililoko Korintho.

Sura ya 4

Katika Mdo. 18, Luka anatueleza kwamba wakati Paulo alipokuwa katika moja ya safari zake za kiumisheni, alisaidia kuanzisha kanisa katika mji wa Korintho. Kulingana na kitabu cha Matendo ya Mitume, Paulo alitumia miezi kumi na nane akifundisha neno la Mungu, likifuatiwa na ubatizo wa wakorintho wengi ambao waliisikia, wakaiamini na kuitii Injili. Kutoka Korintho, punde Paulo akaondoka kuelekea Asia ndogo, ambako alifanya kazi ya kuanzisha kanisa katika mji wa Efeso. Ili hali akiwa katika mji wa Efeso, Paulo alipokea maneno kwamba kulikuwa na matatizo yaliyokuwa yakiendelea katika mwili wa Kristo uliopo Korintho. Moja kati ya matatizo hayo linahusiana na mgawanyiko miongoni mwa washiriki, kuhusiana na watu binafsi kuwainua wahubiri fulani.

Kwa maana, ndugu zangu, nimeharifiwa habari zenu na wale walio wa nyumbani mwa Kloe, ya kwamba iko fitina kwenu. Basi, maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu kusema, “Mimi ni wa Apolo”, na, “mimi ni wa Kefa,” na, “mimi ni wa Kristo.” Je! Kristo amegawanyika? Je! Paulo alisulubiwa kwa ajili yenu? Au je! Mlibatizwa kwa jina la Paulo? (1 Wakorintho 1:11-13).

Paulo aliposikia kuhusu matatizo haya, aliandika (kupitia uvuvio wa Roho Mtakatifu) kitabu cha Wakorintho wa Kwanza. Katika waraka huo, alipinga kwa ukali utengano.

Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mama; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja (1 Wakorintho 1:10).

Kwa bahati mbaya, baadhi ndani ya kanisa lililoko Korintho walishaanza kujitenga dhidi ya kuwainua wahubiri fulani. Baada ya kubatizwa, mtu fulani akaanza kusema, “Mimi ni wa Paulo,” au “Mimi ni wa Kefa,” au “Mimi ni wa Kristo.” Hata hivyo, Paulo, anaukataa mgawanyiko wao kwa kuwauliza maswali matatu muhimu: Je, Kristo amegawanyika? Je, Paulo alisulubiwa kwa ajili yenu? Au Je, mlibatizwa kwa jina la Paulo? (1 Wakorintho 1:13).

Majibu ya maswali haya yako wazi. Kwanza, *Kristo hajagawanyika*. Katika Marko 3:22-26, Kristo alitilia mkazo umuhimu wa asili yake. Pili, Paulo hakusulubiwa kwa ajili yao. Na tatu, hawakubatizwa kwa jina la Paulo. Kulingana na Mathayo 28:19, wenye dhambi walibatizwa katika jina la Kristo.

Kulingana na sifa hii, Je, hawa wakristo wa Korintho walikosea kwa kujiita “wa Paulo?” Je, wangelitenda dhambi kwa kuliita kanisa kwa jina la Paulo (“kanisa la Paulo”)? Ndiyo, wangelikuwa wamekosea. Na ndiyo, wangelikuwa wametenda dhambi dhidi ya Mungu.

Vipi kama leo kungelikuwa na mhubiri katika kanisa anayeitwa Alex Campbell, ambaye yeye mwenyewe



Kuhusu Kanisa

alikuwa mhubiri mwenye uwezo na nguvu? Hebu tuseme kwamba alikuwa ni maarufu na msomi mwenye elimu ya juu ya Biblia ambaye alisaidia kuwaongoa maelfu kuja kwa Kristo. Kama sisi, tungetaka kumheshimu yeye, tungelianza kuvaa jina la kidini, “Wakempbell,” Je, hiyo ingelikubaliwa na Mungu? Hapana kulingana na mafundisho ya Paulo katika 1 Wakorintho 1! Ili kwamba mtu aweze kujiita wa “Wakempbell,” vitu vitatu vingelipaswa kuwa ni vya kweli:

1. **Kristo angelipaswa kugawanyika.**
2. **Mtu angelipaswa kubatizwa “katika jina la Alex Kempbell.”**
3. **Alex Kempbell angelipaswa kusulubiwa kwa ajili ya huyo mtu.**

Kwa kujiita Mkempbell, utakuwa unaugawanya mwili wa Kristo, na ungeleta utukufu kwa Alex Kempbell badala ya kuleta utukufu kwa Kristo. Katika 1 Wakorintho 1:31, Paulo alisema, “Yeye aonaye fahari na aone fahari juu ya Bwana.” Petro aliandika: “Lakini ikiwa kwa sababu ni mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo.” (1 Petro 4:16, *The Holy Bible in Kiswahili-Union Version*). Je, Petro alikuwa anamaanisha nini wakati aliposema kwamba tunapaswa kumtukiza Mungu “katika jina hilo”? Je, ni jina gani? Jibu kwa hakika ni, jina la Kristo!

Kama ni makosa kuugawanya mwili wa Kristo dhidi ya kuwainua wahubiri, Je, hiyo haitakuwa sawa na kuugawanya mwili wa Kristo dhidi ya mafundisho au vitabu vya miongozo vilivyotengenezwa na wanadamu? Je, itakuwa ni makosa kuugawanya mwili wa Kristo kwa kuyafuata majina ya kidini ambayo hayaajaamriwa, ama kwa ajili ya nafsi zetu au kwa ajili ya kusanyiko ambalo sisi ni washiriki?

Kanisa moja linaweza lisifundishe kitu kinachofanana na kanisa lingine, lakini kulingana na udhehebu, wote ni “kanisa la Kristo.” Hata hivyo, maandiko yanatufundisha kwamba kuna mwili mmoja, kanisa moja, na kwamba kanisa hilo linafundisha kitu kinachofanana kila mahali. Hicho ndicho tunachohitajika kujitahidi kukifanya leo – kunena “kama mahusia ya Mungu,” na si kutofautisha au kujitenga katika makundi mbalimbali, ambayo yote yanadai kuwa yanatokana na mwili mmoja.

**B.J. Clarke
Mhudumu**

Umoja wa kanisa unasisitizwa mara kwa mara katika Agano Jipya. Hivyo basi, hatupaswi kuwa na hatia ya kuugawanya mwili wa Kristo! Ama kwa hakika! Yesu mwenyewe aliomba kwa ajili ya umoja kwa waumini wote:

Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani

yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma (Yohana 17:20-21).

Hasa Paulo aliliagiza kanisa kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani:

Kwa hiyo nawasihi, mimi niliyemfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyostahili wito wenu mlioitwa; kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo; na kujitahidi kuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote (Waefeso 4:1-6).

Angalia sio tu kwamba umoja ni wa lazima, lakini pia mgawanyiko na kujitenga vinakataliwa. Makosa kama hayo yanawekwa katika kundi la matendo ya mwili ambayo hayapaswi kufanywa au kuvumiliwa.

Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu (Wagalatia 5:19-21).

Ndugu zangu, nawasihi, waangalieni wale wafanyao fitina na mambo ya kukwaza kinyume cha mafundisho mliyojifunza; mkajiepushe nao. Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini na ya kujipendekeza waidanganya moyo ya watu wanyofu (Warumi 16:17-18).

Mgawanyiko unakemewa, ambao ndiyo sababu wakristo wanapaswa kujitahidi kwa bidii kuuhifadhi umoja katika mwili wa Kristo (Waefeso 4:1-6). Ili kuweza kuunganishwa kikamilifu katika nia moja na katika hukumu moja, kila mmoja wetu ni lazima awe tayari kuacha kitu chochote ambacho hakijaamriwa katika Biblia. Umoja unatuhitaji sisi kuabudu na kuishi kulingana na neno la Mungu – na ni neno la Mungu pekee! Ili kuuhifadhi umoja wa roho na kifungo cha amani ni lazima tutumie maneno kama, “kama asemavyo Bwana” kwa kila tukifanyacho na tukisemacho. Paulo alilielezea kwa maneno yafuatayo: “Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.” (Wakolosai 3:17).

Sura ya 4

MARUDIO YA SURA: JE, NI LAZIMA KANISA LIWE NA UMOJA?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na mstari hapo chini, Yesu alilinunua kanisa kwa damu yake. Leo, kuna madhehebu mengi ya kidini. Kuwa dhehebu ni kujitenga au kulimega kanisa ambalo Kristo alilifia, na alilinunua kwa damu yake. Je, hili linakubalika kwa Mungu? NDIYO/HAPANA

Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe (Mdo. 20:28).

2. Je, Biblia inaikubali dhana ya udhehebu? NDIYO/HAPANA
3. Kulingana na 1 Wakorintho 1:10, mtume analiandikia kanisa lililopo Korintho “kwamba nyote _____; wala pasiwe kwenu _____, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja.”
4. Kulingana na 1 Wakorintho 1:10-13, Je, itakuwa ni makosa pia kwa wakristo kuanza kujiita Wapaulo (wakijiita kwa jina la mtume Paulo). NDIYO/HAPANA.
5. Kulingana na mstari hapo chini, _____ litu-pasalo sisi kuokolewa kwalo.

Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo (Mdo. 4:12).

6. Kulingana na Yohana 17:20-21, Yesu alisema, “Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na _____; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako.”
7. Kulingana na Waefeso 4:1-6, Je, Paulo anasisitiza umoja wa wakristo na kanisa? NDIYO/HAPANA
8. Kulingana na Wagalatia 5:19-21, Je, kuna migongano, migawanyiko, makundi na machafuko katika kanisa? NDIYO/HAPANA
9. Kulingana na Wakolosai 3:17, Je, kila tunachokisema au kukifanya ni lazima kifanyike katika jina la Bwana Yesu? NDIYO/HAPANA.

Sehemu ya MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA inapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Kama wewe ni mshiriki wa kanisa ambalo si kanisa la Kristo, lakini badala yake ni moja kati ya migawanyiko mingi katika dini iliyoletwa leo na wanadamu, Je, uko *sahihi* kuendelea kubaki katika kanisa hilo? NDIYO/HAPANA.

Kuhusu Kanisa

- B. Kulingana na Wakolosai 3:17, Paulo ameandika: “Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu.” Je, kanisa ambalo wewe unashiriki linaitii hii amri ya Paulo iliyovuviwa? NDIYO/HAPANA.

MASUALA YA MAZUNGUMZO

- A. Je, “ufuasi wa madhehebu ni nini,” na ni kwa nini unakataliwa na Mungu?
- B. Je, ni kwa nini si sahihi kutumia majina mengine kwa ajili ya kanisa au kwa ajili ya wakristo binafsi, ambayo hayajaruhusiwa na Mungu katika neno lake?
- C. Kama ni makosa kumuita mkristo (au kanisa) kwa jina la Paulo (wa Paulo), Je, ni majina yapi mengine ambayo yapo leo na hayatakubaliwa?



HITIMISHO

Kufanya kitu “katika jina la Bwana Yesu” ni kufanya kupitia ruhusa na uthibitisho wake. Jiulize mwenyewe: Je, mimi nautafuta uthibitisho wa Bwana? Je, mimi niko ndani ya kanisa lake? Je, ninavaa jina la kidini linaloleta utukufu kwa Kristo? Je, mimi ninaishi na kuabudu katika njia ambayo imeruhusiwa (na hivyo inakubalika) na Kristo? Je, ninajitahidi kuchochea umoja katika mwili wa Kristo kwa kuliendea neno la Mungu na kufanya yale tu ambayo Biblia inaniruhusu?

Je, itakuwa si ajabu kama wanaoutafuta ukweli kwa unyofu kila mahali wakikataa kuvaa/kutumia majina ya kidini yaliyoletwa na wanadamu, wakaacha vitabu vyao mbalimbali vya miongozo, “ukiri wa imani,” na matendo yote yasiyo ya kibiblia – na kufanyika kuwa tu washiriki wa kanisa la Kristo lililofunuliwa katika Biblia? Mambo hayo hayatakuwa tu ni ya “ajabu,” bali kwa hakika, tunapaswa kufanya kila jitihada ili hilo litokee. Hivyo, katika kulijibu swali, “Je, ni lazima kanisa liwe na umoja?” Tunapaswa kujibu kwa sauti kuu “NDIYO!”

Kama tulivyojifunza katika somo hili kwamba

Kanisa ni mwili wa Kristo, na linaundwa na wale waliokolewa

Na

Kanisa ni la muhimu, la lazima na linahitajika,

Pia tumejifunza kwamba

Kanisa ni lazima liwe na umoja.

Huu ukweli wa aina tatu ni msingi wa Imani. Ni sehemu ya baraka za injili ya Kristo. Ni sehemu ya Kweli – neno

la Mungu – ambalo linaweza kutuweka huru kutoka katika pingu za majina, mafundisho na matendo yaliyoagizwa na wanadamu.

Je, utaukubali na kuutii ukweli kutokana na kile Biblia inachofundisha kuhusu kanisa la Kristo? *Utaiifahamu* kweli, na kweli *itakuweka* huru (Yohana 8:32). Nakusihi uukumbatie ukweli kuhusu kanisa kama ulivyofunuliwa ndani ya kurasa za neno la Mungu.

MARUDIO YA SURA

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana ndani ya sura hii.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na Mathayo 16:18, Yesu alisema, “Juu ya mwamba huu nitali-jenga kanisa _____, wala mi-lango ya kuzimu haitalishinda.”
2. Kulingana na Mdo. 2: 41, 46-47, “Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa _____.”

Sura ya 4

3. Katika 1 Wakorintho 1:13, Paulo aliuliza: "Je, Kristo amegawanyika?" Jibu sahihi ni lipi? NDIYO/HAPANA

MASWALI YA KUTILIA MAKAZO

1. Kulingana na Mdo 2:47, Mungu huwazidisha waliookolewa katika kanisa. Je, inawezekana kuokolewa, na bado ukawa haupo ndani ya kanisa? NDIYO/HAPANA
2. Kulingana na Wakolosai 1:24, kanisa ni mwili wa Kristo. Kulingana na Waefeso 4:4, kuna mwili mmoja. Hata hivyo, Je, Yesu alianzisha makanisa mangapi?
3. Somo hili limejadili njia tatu tofauti ambazo neno "kanisa" limetumika katika kuwazungumzia waliookolewa; moja ya njia hizo ni mahali fulani, kama ilivyo kwa "kanisa lililopo Yerusalemu" (Mdo. 11:22). Je, njia nyingine mbili ni zipi? (a) _____ (b) _____

Sehemu ya MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZA na MASWALI YA KUTILIA MAKAZO inapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MAMBO UNAYOPASWA KUJUA

- Kanisa ni mwili wa Kristo, na linaundwa na wale waliookoka.
- Kanisa ni la lazima, la muhimu na linahitajika.
- Kanisa ni lazima liwe na umoja.
- Yesu alianzisha kanisa; yeye ndiye Bwana Harusi wake; lenyewe ni bibi harusi wake; ni lazima livae/litumie jina lake.
- Kanisa ni: waliookolewa, kundi la waumi ni waliobatizwa, mwili wa Kristo; ufalme wa Mungu; nyumba ya Mungu; hekalu la Mungu.
- Mtu ni lazima awe ndani ya kanisa ili aweze kuokolewa.
- Mgawanyiko wa kanisa ni dhambi.

CHIMBA ZAIDI ...

Masomo hapo chini yamebuniwa kwa ajili ya watu ambao wangelipenda kujifunza somo hili zaidi. Kuna taarifa ambazo hazikujadiliwa kimsingi ndani ya somo hili.



KRISTO NA KANISA KATIKA UNABILAHADI NA UTIMILIFU

Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa BWANA wa majeshi ndio utakaotenda hayo (Isaya 9:6-7).

Kwa ajili ya hayo Bwana, MUNGU, asema hivi, "Tazama, naweka jiwe katika Sayuni, liwe msingi, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembeni lenye thamani, msingi ulio imara; yeye aaminiye hatafanya haraka" (Isaya 28:16).

Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono; tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile, nitamimina roho yangu (Yoeli 2:28-29).

Akawaambia, "Amini, nawaambia, Pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapouona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu" (Marko 9:1).



Kuhusu Kanisa

Lakini Petro akasimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapaza sauti yake, akawaambia, “Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, makasikilize maneno yangu. Sivyo mnavyodhani; watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana; lakini jambo hili ni lile lililolenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli, ‘Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto. Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake Roho yangu, nao watatabiri’” (Mdo 2:14-18).

Wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa (Mdo.2:47).

Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo. Naye amejulikana kweli tangu zamani, kabla haijawekwa misingi ya dunia; lakini alifunuliwa mwisho wa zamani kwa ajili yenu (1 Petro 1:18-20).

Mmwendee yeye, jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule Basi, heshima hii ni kwenu ninyi mnaoamini. Bali kwao wasioamini, “Jiwe walilolikataa waashi, limekuwe jiwe kuu la pembeni,” (1 Petro 2:4,7).

MAMBO YA KUFIKIRIA WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

1. Je, Isaya alikuwa anatabiri kumhusu nani katika Isaya 9:6-7? _____
2. Je, ni nani ndiye “jiwe kuu la pembeni” na “msingi ulio imara” ambao Isaya anautabiri katika Isaya 28:16? _____
3. Katika Marko 9:1, Je, Yesu anafundisha kwamba ufalme wa Mungu (kanisa) utakuja katika kipindi cha wale waliokuwa hai katika karne ya kwanza? NDIYO/HAPANA
4. Kulingana na Mdo. 2:47, Je, ni taasisi gani ya muhimu ilianzishwa kwenye siku ya Pentekoste baada ya kufufuka kwa Yesu? _____
5. Je, Yoeli 2:28-29 na Mdo. 2:14-18 zinafundisha kwamba Mungu alilipagilia kanisa muda mrefu hata kabla halijaanza? NDIYO/HAPANA

6 Naye _____ kweli tangu zamani, kabla haijawekwa misingi ya dunia; lakini _____ mwisho wa zamani kwa ajili yenu” (1 Petro 1:18-20).

7 Petro alikuwa anamzungumzia nani katika 1 Petro 2:7 wakati aliposema, “Jiwe walilolikataa waashi, limekuwa jiwe kuu la pembeni?” _____



HITAJI LA UKWELI NA AHADI KUTOKA KWA KRISTO NA KANISA

Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mkajifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzungu wangu ni mwepesi (Mathayo 11:28-30).

...Mtu ye yote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike na msalaba wake, anifuata (Marko 8:34).

Wala hakuna wokovu katika mwingine aweye yote, kwa maana hapana jina jingene chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo (Mdo. 4:12).

Kisha akatoka akaenda Tarso kumtafuta Sauli; hata alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia. (Mdo. 11:25-26).

Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; (Warumi 3:23).

Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu (Warumi 6:23).

Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo (Waefeso 1:3)

Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake (Waefeso 1:7).

Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili (Waefeso 5:23).

Kwa ajili ya hilo nastahimili mambo yote, kwa ajili ya wateule, ili wao nao waupate wokovu ule ulio katika Kristo Yesu, pamoja na utukufu wa milele. (2 Timotheo 2:10).

Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi

Sura ya 4

atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima (Ufunuo 2:10)

Nao waimba wimbo mpya wakisema, “Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa,” (Ufunuo 5:9).

MAMBO YA KUFIKIRIA WAKATI WA KUCHIMBA ZAI

8. Kulingana na Mathayo 11:28-30, kama tukimwendea Yesu, atatupa _____.
9. Je, Marko 8:34 inafundisha kwamba ili kumwendea Yesu tunapaswa kujikana sisi wenyewe, tujitwike msalaba na kumuata? NDIYO/HAPANA.
10. Je, Mdo 4:12 inafundisha kwamba kuna majina mbalimbali ambayo tunayahitaji ili tuweze kuokolewa? NDIYO/HAPANA

11. Kulingana na Mdo. 11:26, washiriki wa kanisa, wanafunzi, waliitwa _____.

12. “Kwa maana mshahara wa dhambi ni _____ bali karama ya Mungu ni _____ katika Kristo Yesu Bwana wetu” (Warumi 6:23).

13. Kulingana na Waefeso 1:3 na 7 na 2 Timotheo 2:10, Baraka zote za rohoni, ukombozi, msamaha, na wokovu unapatikana kwa _____.

14. Kulingana na Waefeso 5:23, Yesu alisema kwamba kama tukiwa waaminifu, atatupa _____

MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUCHIMBA ZAI yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.



Tafuta Ukweli

NYUMBA YA MUNGU



Sura ya 5

Watu wengi ulimwenguni huishi katika aina fulani ya nyumba au makazi. Nyumba hizo huwa na maumbo na ukumbwa mbalimbali – zikiwa na sakafu na mpangilio tofauti na hupambwa katika njia nyingi tofauti. Lakini bado kila nyumba ni ya thamani na ya kipekee kwa mmiliki wake. Lakini, Je, umeshawahi kujiuliza kama Mungu ana nyumba au la? Na kama anayo, Je tunawezaje kuitambua nyumba hiyo kama leo tutatoka na kuitafuta?

UTANGULIZI

Akiwa amevuviwa na Roho Mtakatifu, mtume Paul alimwandikia mwinjilisti kijana aliyeitwa Timotheo yafuatayo:

Nakuandikia hayo nikitaraji kuja kwako hivi karibu. Lakini nikikawia, upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli (1 Timotheo 3:14-15).

Kutoka katika kifungu hiki, tunajifunza kwamba Mungu ana nyumba – maskani. Nyumba hiyo hufahamika kama “kanisa.” Kanisa kama tulivyojifunza katika somo lililopita, linaundwa na “waliookolewa” na Kristo. Kama “waliookolewa,” wanatambulika kama mwili, ufalme, hekalu la Mungu, na kama tulivyokwisha kuona linatambulika pia kama nyumba ya Mungu.

Mungu, aliye na nguvu dhidi ya ulimwengu wote, anakaa katika dunia yote. Kwa hakika yeye anajua mambo yote, anaona vitu vyote na yupo sehemu zote wakati wote. Lakini bado Mungu hukaa katika njia maalumu ndani ya watu wake, ambao ni kanisa.

Jengo la kanisa si kanisa. Bali, jengo hilo ni sehemu tu ambayo washiriki wa nyumba ya Mungu hukutana mara kwa mara ili kuabudu na kujifunza. Kulingana na 1 Wakorintho 3:16, kanisa – kama maskani ya Mungu – inafahamika kama nyumba au hekalu la Mungu. Nyumba hiyo kama unavyoweza kutarajia ni ya kipekee. Ina mbunifu na mjenzi wa kipekee. Ilikuwa wakati uliopita na hata sasa na mpangilio wa kipekee wa uongozi na dhumuni lake. Pia lina sifa kadha wa kadha ambazo kama leo tungelitoka ili tuitafute zitatusaidia kutambua uwepo wake.

Hebu tuitafute hiyo nyumba. Hebu tutafute ukweli kuhusu nyumba ya Mungu. Kama tunavyofanya, tunahitaji kujiuliza maswali matatu ya muhimu:

1. Je, ni nani aliyeijenga nyumba ya Mungu?
2. Je, ni zipi sifa za kipekee za nyumba ya Mungu?
3. Je, leo tunaweza kuianzisha nyumba ya Mungu?

Hebu tuanze kwa kutafuta jibu la swali la kwanza: “Je, ni nani aliyeijenga nyumba ya Mungu?”

JE, NI NANI ALIYEIJENGA NYUMBA YA MUNGU?

Haipaswi kutuchukua muda mrefu kulijibu hili swali. Ukweli ni kwamba, kuna uwezekano kwamba wewe tayari unalifahamu jibu lake. Lakini ili kuwa na uhakika, hebu tusome maneno ya Yesu ili tuweze kugundua wenyewe kile anachotaka sisi tujue kuhusu kanisa lake.

Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria – Filipi, akawauliza wanafunzi wake akasema, “Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?” Wakasema, “wengine hunena u Yohana Mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeria au mmojawapo wa manabii.” Akawaambia, “Ninyi mwaninena mimi kuwa ni nani?” Simoni Petro akajibu akasema, “wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.” Yesu akajibu, akamwambia, “Heri wewe Simoni Baryona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.” (Mathayo 16:13-18).

Katika mstari wa 18 wa kifungu hiki, tunaona wazi kabisa kwamba Yesu ndiye Mjenzi wa kanisa. Pia tunaweza kugundua kwamba, yeye ndiye Mmiliki wa kanisa lake, kama anavyotilia msisitizo katika maelezo yake, “Nitalijenga kanisa Langu.” Kihusishi hiki “Langu” kinamwelekea Yesu kwa uwazi kabisa. Hivyo basi, yeye ndiye Mjenzi na Mmiliki wa kanisa lake.

Soma kile mwandishi wa kitabu cha Waebrania alichosema kuhusu suala hili, na uangalie ni nani ambaye yupo “juu” (au “msimamizi”) ya nyumba ya Mungu:

Kwa hiyo, ndugu watakatifu, wenye kushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu, aliyekuwa mwaminifu kwake yeye aliyemweka, kama Musa naye alivyokuwa, katika nyumba yote ya Mungu. Kwa maana huyo amehesabiwa kuwa amestahili utukufu zaidi kuliko Musa, kama vile yeye aitengenezaye nyumba alivyo na heshima zaidi ya hiyo nyumba. Maana kila nyumba imetengenezwa na mtu; ila yeye aliyevitengeneza vitu vyote ni

Nyumba ya Mungu

Mungu. Na Musa kweli alikuwa mwaminifu katika nyumba yote ya Mungu kama mtumishi, awe ushuhuda wa mambo yatakayonenwa baadaye; bali Kristo, kama mwana, juu ya nyumba ya Mungu; ambaye nyumba yake ni sisi, kama tukishikamana sana na ujasiri wetu na fahari ya taraja letu mpaka mwisho (Waebrania 3:1-6).

Kutoka katika kifungu hiki (na mambo tulijojifunza kutoka katika somo lililopita kuhusu kanisa) tunaweza tukahitimisha kwamba:

- **Jesu Kristo, ambaye ni Mungu, amejenga nyumba.**
- **Wakristo (waliookolewa) ndiyo nyumba hiyo.**
- **Yesu yupo juu ya nyumba yake.**

Hivyo, ni kweli kwamba Kristo ndiye Mjenzi na Mmiliki Lakini, Je, kishazi “juu ya nyumba yake” kinazungumzia nini?

Kirai “juu ya nyumba yake” kinazungumzia ukuu wa kipindi cha kanisa ukilinganishwa na kipindi cha zamani cha Musa. Katika siku zile na kipindi kile, Musa, kama mtumishi, alikuwa ndiye kichwa cha nyumba. Lakini Yesu, aliye Kristo, kama mwana wa Mungu, na kama Mrithi, ndiye Mtawala juu ya nyumba yake, ambayo ni kanisa. Mtume Paulo aliandika, “Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye. Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote” (Wakolosai 1:17-18). Angalia kifungu kinaeleza kwamba Yesu pekee ndiye mwenye mamlaka haya. Hakuna mwanadamu, hakuna kikundi cha watu na hakuna baraza lililo na mamlaka haya. Ni rahisi tu kiasi hicho.

**Chuck Homer
Mkufunzi wa Biblia na Mhudumu**

Kulingana na Wakolosai 1:17-18, Kristo ndiye kichwa cha kanisa. Hiyo inamaanisha, kwamba yeye pekee ndiye mwenye haki ya kutunga na kutoa sheria kulingana na asili yake, ibada yake, mpangilio wake, kazi yake na mengine mengi. Hivyo basi, hakuna mwanadamu anayeweza kudai kwamba yeye ndiye “kichwa cha kanisa,” kutokana na kwamba Yesu pekee ndiye kichwa. Zaidi sana, hapana mtu awaye yeyote anaye stahili kudai kwamba yeye ndiye mmiliki wa kanisa lililojengwa na Yesu, kutokana na kwamba Yesu ndiye Mmiliki, Mjenzi na Kichwa.

Ama kwa hakika Kristo yupo “juu” ya nyumba yake. Lakini Je, ni kiwango gani cha mamlaka alichonacho Kristo? Yesu alisema, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani” (Mathayo 28:18).

Je, ni kiwango gani cha mamlaka alichonacho Kristo? Ana mamlaka yote. Hiyo haitoi nafasi kwa mtu yeyote yule. Yote maana yake ni yote. Kama ninataka kufahamu kitu fulani kuhusu nyumba ya Mungu (kanisa), basi ninapaswa

kumwendea Yesu na ni Yesu pekee, kutokana na kwamba yeye ndiye Mjenzi na Mmiliki wa kanisa.

Lakini sasa hebu tujiulize, “Kutokana na kwamba Kristo ndiye Mjenzi, Mmiliki na Kichwa cha kanisa, Je, wewe au mimi tuna haki ya kuboresha na/au kuongeza katika nyumba yake? Je, tunaweza tukaamua wenyewe kubadilisha au kuiboresha nyumba ambayo Yesu tayari amekwisha kuijenga?”

Fikiri kama unataka kujenga nyumba ya kuishi. Na una pesa za kutosha kununua ardhi, vitu vya kujengea na umeamua kujenga nyumba hiyo kwa mikono yako mwenyewe. Fikiri zaidi, kwamba umeajiri vibarua wa kukusaidia katika ujenzi wa nyumba yako. Na ndipo ukawaamuru waijenge nyumba kulingana na maelekezo yako – kukiwa na idadi kamili ya vyumba unavyovihitaji, kwa hakika ukubwa wa sakafu unaohitajika n.k. Fikiria kwamba, baada ya nyumba yako kukamilika, unawakaribisha baadhi ya marafiki au ndugu ili wakae nyumbani kwako. Je, hao rafiki au ndugu wanahaki ya kuibadilisha nyumba yako iwe kama wanavyotaka wao? Je, wanaweza kuanza kufanya mabadiliko katika nyumba yako bila maagizo yako? Vipi kama siku moja utagundua kwamba rafiki au ndugu zako wamefanya kitu hicho, na wameamua wenyewe kuibadilisha nyumba kwa kuongeza ukuta hapa au mlango pale? Je, utajisikiaje? Je, utakubaliana na hilo? Ama kwa hakika jibu ni hapana! Je, ni kwa nini jibu ni hapana? Ni kwa sababu nyumba ni mali yako! Uliijenga kwa mikono yako mwenyewe na kwa pesa zako mwenyewe. Hivyo basi, ni wewe na ni wewe pekee uliye na haki ya kuamua siyo tu aina na mpangilio wa nyumba, bali pia jinsi nyumba itakavyokuwa inatunzwa.

Katika njia kama hiyo hiyo, Kristo aliye Mjenzi wa nyumba yake (Kanisa), aliyewanunua kwa damu yake mwenyewe watu wanaoliunda kanisa (Mdo. 20:28; 1 Petro 1:18-19). Na ndipo akawaamuru mitume kujenga msingi wa kanisa na kumsaidia kulijenga kulingana na maelekezo aliyoyatoa Mungu (Waefeso 2:19-22; 1 Wakorintho 3:10-11). Kama wakazi ambao tunaishi katika nyumba inayomilikiwa na kujengwa na Yesu, Je, tuna mamlaka ya kuboresha au kubadilisha vitu kama tupendavyo? Je, tuna haki ya kupangilia nyumba yake kulingana na maoni yetu wenyewe, au kuweka jina tofauti kwenye nyumba, hata kama si mali yetu? Hapana. Sisi sote tunatambua kwamba kama wakazi, tunapaswa kuiacha nyumba kama tulivyoikuta, na tunapaswa kuishi katika nyumba kulingana na kanuni za Mungu ambazo zinapatikana katika neno la Mungu. Hatuna haki wala mamlaka ya kubadilisha maelekezo yanayopatikana kwenye Biblia.

Sasa, Je, ni nani aliye mjenzi wa nyumba ya Mungu? Yesu ndiye Mjenzi – na kama Mjenzi na Mmiliki, yeye ana mamlaka yote dhidi ya nyumba yake.

SEHEMU YA MARUDIO: JE, NI NANI ALIYEIJENGA NYUMBA YA MUNGU?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZIA

1. Kulingana na 1 Timotheo 3: 14-15, "nyumba ya Mungu" ni sawa na "_____ Mungu aliye hai."
2. Je, Agano Jipya linafundisha kwamba vishazi kama "mwili", "ufalme," "waliookolewa," "hekalu la Mungu," na "nyumba ya Mungu" vyote vinalielezea kanisa? NDIYO/HAPANA
3. Kulingana na Mathayo 16: 13-18:
 - a. Je, ni nani aliyelijenga kanisa? _____
 - b. Je, kanisa ni mali ya nani? _____
4. Kulingana na Wakolosai 1: 17-18, Yesu yuko "kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye. Naye ndiye _____ cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika _____."
5. Kulingana na Mathayo 28: 18, Je, Yesu _____ mamlaka _____ na _____.
6. Kulingana na mistari hapo chini, Je, Yesu (Mungu) alilininua kanisa kwa damu yake mwenyewe? NDIYO/HAPANA

Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinua kwa damu yake mwenyewe (Mdo. 20:28).

Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana – kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo (1 Petro 1:18-19).
7. Kutokana na kwamba Kristo alilininua kanisa, naye ndiye mjenzi na kichwa cha nyumba yake (kanisa), Je, wewe au mimi tuna haki ya kufanya mabadiliko na/au kuongeza chochote katika nyumba yake? NDIYO/HAPANA
8. Kulingana na mistari hapo chini, Je, kanisa limejengwa juu ya msingi wa mitume na Yesu Kristo mwenyewe akiwa ndiye jiwe kuu la pembeni? NDIYO/HAPANA

Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye

Nyumba ya Mungu

Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. Katika yeye jengo lote linaunganishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho (Waefeso 2:19-22).

9. Je, wakazi (wakristo) wa nyumba ya Mungu (kanisa) wanapaswa kuishi katika nyumba hiyo kulingana na kanuni za Mungu zinazopatikana katika neno lake? NDIYO/HAPANA

MAJIBU kwa ajili ya **MASWALI YA KUJIFUNZIA** yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Je, unakubali kwamba Kristo ana mamlaka yote ya kuamua maamuzi yote yanayohusiana na nyumba yake, kanisa, na kwamba wanadamu hawana haki yoyote ya kubadilisha au kuyapuuzia maamuzi ya Kristo? NDIYO/HAPANA
- B. Je, wewe ni mshiriki wa kanisa linaloelezewa katika Biblia, ambalo Kristo alilunua kwa damu yake? NDIYO/HAPANA

MASUALA YA MAZUNGUMZO

- A. Je, ina maanisha nini kwa Kristo kuwa “Mwana juu ya nyumba yake mwenyewe” (Waebrania 3:6)?
- B. Je, kuna tofauti gani kati ya Musa mtumishi na Kristo ambaye ni Mwana?
- C. Je, ni wajibu gani waliokuwa nao mitume katika kujenga nyumba ya Mungu?



JE, NI ZIPI SIFA ZA KIPEKEE ZA NYUMBA YA MUNGU?

Kwa kadiri tunavyoichunguza Biblia, Je, ni kitu gani tutakachogundua kuhusu aina na ujenzi wa nyumba ya Mungu? Je, imepangiliwaje? Je, washiriki wake huabudu katika njia gani? Je, ni fundisho gani linalofundishwa katika nyumba ya Mungu? Na Je, ni jina (au majina) gani linalotumika katika kuitambulisha nyumba ya Mungu?

Kila kikundi cha kidini (au “nyumba za kidini”) kitakuwa na sifa/alama kadhaa wa kadha ambazo hukitofautisha na kikundi kingine cha kidini. Kama vile unavyoweza kuitofautisha nyumba yako na nyumba nyingine, nyumba ya Bwana inaweza kutofautishwa na zile zinazojiita nyumba kwa kupitia sifa za kipekee. Hebu tuitafute nyumba ya Mungu. Tunavyofanya hivi, nina kuomba ufikirie kuhusu kanisa ambalo unahudhuria sasa. Je, linafanana na nyumba ya Mungu kama inavyoonekana katika Agano Jipya?

Kristo ndiye Msingi

Kwanza, kama vile nyumba unayoishi leo, nyumba ya Bwana, kanisa, lina msingi.

.....msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo (1 Wakorintho 3:11 pia Waefeso 2:19-22).

Nyumba ya Mungu ni lazima ijengwe juu ya Yesu Kristo, na si kwa kupitia ushawishi wa watu, au juu ya mafundisho ya wanadamu, miongozo, au mafundisho ya kitaaluma. Kamwe haiwezi kujengwa juu ya “kinachokubalika au kisichokubalika kitamaduni” au “kilicho sahihi kisiasa.” Bali, ni lazima ijengwe juu ya Yesu Kristo, ambaye ni “yeye yule, jana, leo na hata milele” (Waebrania 13:8). Je, kanisa ambalo wewe ni mshiriki wake limejengwa juu ya Yesu?

Kristo ndiye Mjenzi

Pili, kama tulivyojifunza hapo awali, nyumba ya Bwana ina Mjenzi.

.... Nitalijenga kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda (Mathayo 16:18).

Sura ya 5

Je, mjenzi wa kanisa unalohudhuria ni nani? Je, wewe ni sehemu ya kanisa lililojengwa na kuanzishwa na Yesu?

Kristo ndiye Jina

Tatu, alama nyingine ya nyumba ya Bwana ni jina. Kanisa linaelezwa kama kanisa la Mungu (Mdo. 20:28; 1 Wakorintho 1:2; Wagalatia 1:13; 1 Timotheo 3:5). Lakini kwa sababu Kristo ni Mungu (Yohana 20:27-28), pia inazungumziwa kama kanisa la Kristo (Warumi 16:16 – “makanisa ya Kristo yawasalimu”). Kuliita kanisa kwa jina la Kristo huleta utukufu kwa yule aliyelinunua. Mdo. 20:28, Mtume Paulo alisema kwamba Kristo alilinunua kanisa “kwa damu yake mwenyewe.”

Fikiria kama unataka kununua shamba. Na ikawa una fedha zote zinazohitajika ili uweze kununua ardhi hiyo. Je, ungelipenda jina la nani liandikwe katika mikataba au hati ya shamba hilo? Kwa nini, jina lako ni lazima litumike! Wewe umekinunua, na wewe unakimiliki. Hivyo basi, jina lako linapaswa kuonekana katika hati. Katika njia kama hiyo hiyo, kwa sababu Kristo amelinunua kanisa, Je, jina lake halipaswi kuwepo katika hati ya umiliki? Ama kwa hakika linapaswa kuwepo! Ni mali ya Kristo, na linapaswa kubeba jina lake, na si majina ya watu wengine au kikundi.

Angalia pia kanisa katika Agano Jipya linaitwa “bibu harusi wa Kristo” (Waefeso 5:22-23; Warumi 7:1-4; 2 Wakorintho 11:2). Je, ni mume gani (pamoja na Kristo ambaye ni Bwana Harusi wa kanisa) atakayemtaka mke wake kutumia jina la mwanamume mwingine? Je, bibu harusi wa Kristo hapaswi kutumia jina la Kristo? Katika wakati wa Agano Jipya, kanisa lilifanya kitu kama hiki. Lilibeba jina la yule ambaye

alikuwa kwa ajili ya washiriki wake.

Salimianeni kwa busu takatifu, Makanisa ya Kristo yawasalimu (Warumi 16:16).

Ndiyo, nyumba ya Mungu wa kipekee, Mjenzi wa kipekee na Jina la kipekee. Je, kanisa unalohudhuria wewe hutumia jina la Kristo?

Kristo ndiye Mpangaji

Nne, sifa nyingine ya nyumba na kanisa ni mpangilio wake. Ndani ya nyumba ya Bwana, Kristo “ndiye kichwa cha kanisa” (Wakolosai 1:18). Katika kifungu hiki, neno “kanisa” limetumika katika dhana ya ujumla. Katika Agano Jipya, tunasoma pia kwamba mwili huo unazungumziwa katika dhana ya mahali fulani. Kama vile “kanisa lililopo Korintho,” “kanisa lililopo Efeso,” au “kanisa lililopo Filipi.” Baada tu ya kuanzishwa, makanisa haya yalipangiliwa chini ya uongozi na maelekezo ya wanaume waitwao wazee, ambao walipaswa kulilisha na kulichunga kundi katika kila kusanyiko au kikundi cha watu wa Mungu.

Na walipokwisha kuwachagua wazee katika kila kanisa, na kuomba pamoja na kufunga, wakawaweka katika mikono ya Bwana waliyemwamini (Mdo. 14:23).

Tunapozungumzia mpangilio wa kimaandiko wa kanisa la Kristo, tunapaswa kuelewa kwamba makanisa ya Kristo (Warumi 16:16) ni makusanyiko ya mahali fulani. Wale ambao ni washiriki wa makusanyiko hayo ni sehemu ya mwili wa Kristo kwa ujumla (ulimwengu kote), ambapo yeye ndiye Kichwa na ndiye mwenye mamlaka. Kristo ametoa maelekezo yanayohusu mpangilio wa kila kanisa la mahali



Nyumba ya Mungu

husika. Kunapaswa kuwa na wanaume, wanaofahamika kama wazee, ambao wataisimamia kazi hiyo ya mahali hapo.

**Bobbly Liddell
Mkufunzi wa Biblia na Mhudumu**

Neno “mzee” linamzungumzia mtu ambaye, pamoja na wazee wengine katika kusanyiko husika, ana jukumu la kulichunga kundi ambalo ni kusanyiko moja. Katika lugha ya Agano Jipya, watu hawa wanatajwa kwa maneno matatu tofauti ya kiyunani. Kila neno limetumiwa kwa kubadilika badilika, na yanaweza kupatikana kwenye vifungu kama vile 1 Petro 5:1 na Mdo. 20:17,28. Yametafsiriwa kwa kutumia maneno manne ya Kiswahili.

**Presbuteros
Episkopos
Poimen**

**Mzee
Askofu au Msimamizi
Mchungaji**

Maneno yote haya yanamzungumzia mtu ambaye – ametimiza sifa zilizoordheshwa katika 1 Timotheo 3:1-7 na Tito 1:7-9. Katika vifungu hivyo, tunajifunza kwamba mzee ni lazima atimize sifa fulani, kama vile kuwa mkarimu, wa haki, mtakatifu n.k Hivi ndivyo vinavyohitajika ili mtu aweze kuwa mzee.

Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha; si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wa kujadiliana, wala asiwe mwenye kupenda fedha; mwenye kuisimamia nyumba yake vyema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu (1 Timotheo 3:2-4).

Siyo tu kwamba watu hawa wanapaswa kuwa na sifa hizi, bali pia tunajifunza kutokana na kusoma Agano Jipya kwamba hawa maaskofu au wazee wamepewa majukumu maalumu ya kulichunga kundi moja ambalo wao nao ni sehemu yake. Mtume Petro, ambaye yeye mwenyewe alikuwa ni mzee, anaelezea kazi na mipaka ya usimamizi wa mzee wakati anapoandika:

Nawasihi wazee walio kwenu, mimi niliye mzee, mwenzi wao, na shahidi wa mateso ya Kristo, na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye; lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo (1 Petro 5:1-2).

Hakuna kabisa ushahidi au ruhusa katika Biblia kwa kikundi cha wazee au askofu mmoja kuwa na mamlaka nje ya kusanyiko lake la mahali fulani. Ndiyo maana, kanisa la Filipi halikuwa na wazee ambao wangelisimamia masuala ya kusanyiko la Efeso au kinyume chake. Hapakuwa na uongozi wa kikasisi katika kanisa, tofauti na Kristo kuwa ndiye kichwa. Manabii na mitume walisaidia katika kujenga


msingi. Katika Agano Jipya, makusanyiko yalipangiliwa chini ya uongozi wa wazee, na kila kikundi cha wazee kikisimamia kazi ya kundi lao wenyewe.

Ili kanisa la Kristo liwe limepangiliwa kulingana na maandiko, linapaswa kuendana na kielelezo cha Maandiko Matakatifu. Katika Agano Jipya, tunayaona makanisa yenye wingi wa wazee(zaidi ya mmoja) (Mdo. 14:23) katika kusanyiko moja, ambalo walilichunga (1 Petro 5:2 -). Kuna hekima katika mpango wa Mungu, kwa sababu alihakikisha kwamba kwa kuwa na wingi wa wazee, kama mtu mmoja ataharibika kimaadili au kimaandiko, haitakuwa rahisi kuuharibu uongozi mzima. Kuna mfumo wa kuchunguza na kurekebisha ambao Mungu ameujiunga katika hili. Kulikuwa na mashemasi katika Agano la Kale, lakini tunaweza kusema si “bodi ya mashemasi.” Mashemasi katika Agano Jipya walitumika chini ya watu ambao walikuwa ni wazee – watu ambao walipaswa kuwa na sifa fulani, kulingana na 1 Timotheo 3:1-7, Mashemasi pia wanapaswa kutimiza sifa fulani, kama zinavyopatikana katika 1 Timotheo 3:8-13. Wahubiri hawajawahi kuwa wasimamizi wa kanisa katika karne ya kwanza. Katika kielelezo cha Mungu, wahubiri wanapaswa kuhudumu chini ya usimamizi wa wazee. Wao si viongozi wa kanisa, kwa maana kwamba wao ndiyo wanaotoa maamuzi ya mwisho. Wafilipi 1 inazungumzia maaskofu (Wazee na maaskofu ni neno lenye maana moja na hutumiwa kwa kubadililabadili) na mashemasi. Hivyo basi, unakuwa na wazee wanaolisimamia kusanyiko husika, pamoja na mashemasi wakitumika chini ya mamlaka yao. Wahubiri na washiriki hufanya kitu hicho hicho, na kufuata usimamizi wa wazee wawatawalao (Waebrania 13:17). Huo ndiyo mpango wa Mungu, na ndiyo tunaopaswa kuufuata.

**B.J.Clarke
Mhudumu**

Nyumba ya Mungu ina Msingi, Mjenzi, Jina na mpangilio wa kipekee. Je, dini uliyopo imepangiliwa kulingana na maelekezo ya Bwana?

Nyumba ya Mungu ina _____ wa/la/ya kipekee:



Sura ya 5

Hebu sasa tuangalie kwamba, pia ina ibada ya kipekee

Kristo Mwanzilishi wa Ibada yenye Maana

Tano, kama ilivyoelekezwa na Yesu, waabuduo halisi imewapasa kumwabudu Mungu “katika roho na kweli,”

Mungu ni Roho, nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika roho na kweli (Yohana 4:24).

Yesu alisema kwamba, tunapaswa kumwabudu Mungu katika kweli. Kama tulivyojifunza katika somo la pili, “Kweli” ni kitu kimoja sawa na “neni la Mungu.” Hivyo basi, kumwabudu Mungu “katika kweli” ni kumwabudu yeye kulingana na neno lake. Kulingana na neno hilo, inawezekana kumwabudu Mungu bure. Yesu alifundisha kwamba ibada huwa ya bure pale ambapo amri za wanadamu zinafundishwa badala ya mafundisho yenye uzima au kweli.

Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu (Mathayo 15:9).

Hivyo, tunaona kwamba katika nyumba ya Mungu, si tu kwamba kila aina ya ibada inakubalika kwake, bali ibada yetu ni lazima iamuriwe na Mungu. Nini basi, Je, kuna viashiria vya ibada yenye maana? Je, wakristo waliabudu katika njia gani kwenye karne ya kwanza? Na Je leo, wakristo wanapaswa kuabudu katika njia gani?

Wakristo wanapokutanika...

Wanaomba

Kulingana na Biblia, wakristo walipokutanika ili kuabudu, waliomba (Mdo. 2:42; 4:31; 1 Timotheo 2:1-6; 1 Wathesalonike 5:17; Mdo. 12:5). Waliomba kupitia (“katika jina la”) Yesu ambaye ndiye Mpatanishi pekee kati ya Mungu na mwanadamu. Kuomba kulikuwa ni jambo la msingi sana katika ibada ya kanisa wakati wa karne ya kwanza, na bado ni muhimu sana hata leo.

Lakini wakristo, kama sehemu ya ibada yao, pia wanapaswa:

Kulitangaza Neno la Mungu

Wakati washiriki wa nyumba ya Mungu wanapokutanika, neno la Mungu huhubiriwa (Mdo. 20:7, 20; 1 Wakorintho 14). Mahubiri yamewekwa kwa ajili ya kuelekeza na kujenga. Yamewekwa ili kuwalea na kuwaimarisha wakazi wa ufalme wa utukufu, pamoja na kuziongoa roho zilizopotea ili zimjie Yesu. Kufundishwa kwa neno la Mungu ni jambo la msingi sana katika maisha na kazi ya kanisa. Ndicho chanzo cha chakula ambacho wakristo wanakihitaji ili kuendelea kuimarika kiroho.

Lakini, hebu tuangalie pia kwamba, katika nyumba ya Bwana, wakristo:



Huchangia katika hazina ya pamoja (katika siku ya kwanza ya kila juma)

Kanisa lilipoanzishwa katika karne ya kwanza, yalitokea mahitaji ya kufadhili kazi za kanisa, palikuwapo wajane ambao walihitaji msaada wa kifedha, wahubiri ambao walihitaji posho na familia zilizokuwa na hali mbaya. Katika kukabiliana na hili, makusanyiko yalijitolea kusaidia, mara kwa mara walilifanya hilo kwa njia ya matoleo ya hiari kutoka kwa washiriki kila siku ya kwanza ya juma (1 Wakorintho 16:1-2; 2 Wakorintho 9:6-7). Chini ya Agano la Kale, Wayahudi waliamriwa kutoa sehemu ya kumi ya kila walichokipata au kuzalisha (inafahamika kama “fungu la kumi”). Lakini katika nyumba ya Mungu, kanisa, fungu la kumi halijatiliwa mkazo. Badala yake, wakristo wanahitajika kutoa kadiri Mungu alivyowafanikisha, na kufanya hivyo kwa moyo wa ukunjufu:

Lakini ninasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu (2 Wakorintho 9:6-7).

Pamoja na suala la kutoa kila siku ya kwanza ya juma, wale walio katika nyumba ya Mungu:

Hushiriki meza ya Bwana (siku ya kwanza ya kila juma)

Siku ya kwanza ya juma ni ya muhimu sana kwa maisha ya kanisa, kwa maana ni siku kama hii ambapo kanisa lilianza. Ni katika siku hii ambapo Yesu alifufuka kutoka katika wafu, na ni katika siku hii ambapo kanisa la Agano Jipya lilikutana ili kushiriki Meza ya Bwana (Mdo. 20:7; Mathayo

Nyumba ya Mungu

26:26-28; Mdo. 2:42). Meza ya Bwana ni kumbukumbu maalumu ambayo hutufanya kukumbuka mwili na damu ya Yesu. Sio tu kwamba mlo huu huwakumbusha wakristo kile ambacho Kristo amefanya kwa ajili yao, bali pia hutumika kama ushuhuda kwa wale wasio wakristo kuhusu upendo wa Kristo kwa wenye dhambi. Kama vile kuimba, kutoa, kuhubiri na kuomba havifanyiki kuwa vitu vya kuzoeleka (hata kama vinafanyika kila juma) vivyo hivyo Meza ya Bwana haipotezi umuhimu wake inaposherehekewa kila juma. Katika karne ya kwanza, Meza ya Bwana ilikuwa ni sehemu ya muhimu ya ibada ya kanisa, na kumbukumbu yake ya kila juma inaendelea kuwa alama ya utambulisho wa nyumba ya Bwana leo.

Hatimaye, nyumba ya Mungu inapokutana kwa ajili ya ibada, washiriki:

Humsifu Mungu na Kujengana wao kwa wao kupitia nyimbo

Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu (Wakolosai 3:16; pia Waefeso 5:19; 1 Wakorintho 14:15).

Muziki ni sehemu ya muhimu ya ibada ya kanisa lakini muziki wa kanisa la Agano Jipya ulikuwa unatofauti kidogo na ule unaosikika mara kwa mara miongoni mwa madhehebu siku hizi. Muziki unaopatikana katika nyumba ya Mungu ni ule usiokuwa na vyombo vya muziki, ambao ni kusema kwamba ni uimbaji usiohusishwa na aina yeyote ya chombo cha muziki.

Inapofikia hatua ya kuamua ni kitu gani tunapaswa kufanya katika ibada, mpango wa wokovu ni upi, au ni kwa jinsi gani kanisa linapaswa kupangiliwa, masuala kama hayo yanapaswa yaamuliwe si kwa wingi wa kura za watu wasiovuviwa, bali kwa kuuliza, “Je, Yesu amesema nini kuhusu hili kupitia mitume wake na kupitia maneno yake mwenyewe wakati wa huduma yake ya hapa duniani?” Hivyo basi, kutokana na kwamba sasa tunafahamu kile

alichosema, Je, tupo tayari kukubali mamlaka yake na kufanya kwa hakika kile alichotuambia tufanye, katika njia ile ile aliyotuagiza tufanye?

B.J Clarke
Mhudumu

Vyombo vya muziki havikuwepo kwenye ibada mpaka ilipofika kame ya saba B.K. Hakuna kiashiria chochote katika maandishi ya wale walioitwa “mababa wa kanisa” katika kame tatu au nne za kwanza za uwepo wa kanisa lililotumia vyombo vya muziki, kamwe havikuwahi kutumika katika ibada ya wakristo. Kuna uwezekano kwamba watu wachache wamelizungumzia hili, lakini matumizi ya vyombo vya muziki katika kumwabudu Mungu kamwe haikuwa tendo linalokubalika katika kame nne au tano za kwanza za uwepo wa kanisa. Katika miaka ya 900, ndipo hatimaye viliingizwa na kukubaliwa kuwa sehemu ya ibada ya wakristo. Wakati huo jambo hili lilisababisha kanisa kugawanyika, wakati huo kanisa la Kiothidoksi la upande wa Mashariki kamwe halikuwahi kukubaliana na suala hili, na halikubaliani na suala hilo hata leo. Wakati Waprotestanti wa Maboresho/Matengenezo walipoingia katika miaka ya 1500, hata miongoni mwa baadhi ya Waboreshaji wakuu (kama vile John Calvin, John Wesley, na Martin Luther) walipinga vikali matumizi ya vyombo vya Muziki katika ibada.

Ben Moseley
Profesa wa Chuo Kikuu na Mhudumu


Wakati matumizi ya vyombo vya muziki yalipoanza kuingizwa mara kwa mara katika ibada za madhehebu mbalimbali, kulikuwa na baadhi ya wahubiri imara miongoni mwa madhehebu hayo ambao walipinga vikali matumizi hayo.

Muziki, kama sayansi, Ninauheshimu sana na kuupenda. Lakini vyombo vya muziki kwenye nyumba ya Mungu ninauchukia mno na kukereka. Haya ni matumizi mabaya ya muziki; na hapa naandika pingamizi langu dhidi ya aina zote za uharibifu wa ibada ya Mwanziilishi wa Ukristo (Adam Clark's Commentary, ya kitabu cha Amosi 6:5).

Sikatai vyombo vya muziki katika ibada zetu, kwa sababu havitasikika wala kuonekana (John Wesley, alivyonukuu katika Adam Clarke's Commentary, ya kitabu cha Amos 6:5).

Ilihali ukweli kwamba wasomi wengi wa Biblia wa zamani walilaumu sana matumizi ya vyombo vya muziki katika ibada ni hakika kweli havistahili, ni muhimu sana kuonesha kwamba hakuna mahali popote katika Agano Jipya tunapopata mamlaka ya kuvitumia leo.

Amri ya Agano Jipya kwa wakristo ya kumwimbia Mungu sifa, haitaji vyombo vya muziki. Ukweli ni kwamba, kulingana na kamusi ya kiyunani ya Bauer (Bauer's Greek Dictionary), matumizi ya neno psallo – lililotafsiriwa kama “zaburi” katika



Sura ya 5

Waefeso 5:19 – linamaanisha “kuimba,” pekee.”

Mungu aliposema kwamba tunapaswa “kuimba” amri hiyo inaondoa kila aina nyingine ya muziki.

Sababu ya sisi kutokutumia vyombo vya muziki ni kutokana na kwamba havijaruhusiwa. Mara kwa mara watu wanaweza wakasema, “Lakini haisemi usitumie.” Hilo halihusiki kabisa. Hebu fikiria kwamba umeamka asubuhi, unajisikia vibaya na unamwendea daktari. Daktari anakwambia una virusi, na anakuandikia kwenye karatasi maelekezo ya kutumia dawa ya salfa. Unaenda kwenye duka la dawa, mfamasia anaiangalia, na kusema nafsini mwake, “hii inaonesha kwamba anahitaji salfa, lakini pia, nitamwongezea penisilini kidogo” Baadaye kidogo, unagundua kile alichokifanya yule mfamasia, na unamwendea tena na kumuuliza, “Ni kwa nini ulifanya vile?” Naye anasema, “Maelezo hayakuwa yanasema kwamba sipaswi kukuongezea.” Hilo halihusiani na chochote, kile alichopaswa kufanya ni kutoa kile daktari alichoelekeza. Njia pekee ya sisi kujua kile kimpendezacho Mungu ni kwa kujiuliza, “Je, neno lake linasemaje?” Kila mstari kwenye Agano Jipya unaongelea kuhusu muziki katika ibada, au aina ya muziki Mungu anayoihitaji, yote huzungumzia kuhusu nyimbo za kutumia sauti za midomo/ulimi. Hivyo basi, hicho ndicho kilichoamriwa katika Agano Jipya na si vinginevyo. Kwa mfano, wakati Mungu alipomwambia Nuhu achonge safina, hakusema, “usitumie mpingo” au “usitumie mkalatusi.” Mungu alipomwambia Nuhu atumie mbao ya mvinje hilo liliondoa aina nyingine zote za mbao.

James Meadows
Mkufunzi wa Biblia na Mhudumu

Uimbaji ambao ni wa kipekee kwa Mungu kwa uhakika kabisa ni ule wa kutumia mdomo (bila kutumia vyombo vya muziki). Lakini vipi kuhusu kabla ya kuanzishwa kwa kanisa la Bwana? Je, vyombo vya muziki havijatajwa kwenye Agano la Kale?

Ndiyo, vilikuwepo, lakini Agano Jipya liliakisi mpangilio wa vitu vya msingi sana vya kimwili (angalia Waebrania 9:10). Agano la Kale limejaa dhahibu za damu. Agano la Kale lilikuwa na uchomaji wa uvumba. Agano la Kale lilikuwa na ukuhani wa kikabila na wa kimwili ambao kwao hali na taarifa za watu zilimfikia Mungu. Lakini mpango huo wa kimwili uliwekwa kando, kama mwandishi wa kitabu cha Waebrania anavyoeleza katika sura ya tisa ya kitabu hicho. Mamlaka ya Agano la Kale yalizidiwa na mpango wa kiroho.

Hakuna budi basi, kwa mtu anayetafuta ukweli leo kutokupita yale yaliyoandikwa kwenye neno la Mungu. Kama vile Mungu alivyoweka wazi matumizi ya mzao wa mzabibu na mkate katika kumbukumbu ya meza ya Bwana, vivyo hivyo ameweka wazi kabisa uimbaji tofauti na upigaji wa vyombo vya muziki. Nina uhakika kwamba hakuna hata mmoja wetu anayeweza kuongeza wahi au Coca – Cola kwenye meza ya Bwana, hata kama tunavipenda vitu hivyo, na pia Mungu hajavikataa. Vyema, vipi kuhusu kuongeza wahi, Coca – Cola na vyombo vya muziki kwenye ibada? Je, hili litakubalika?

Wakristo wa kame ya kwanza walikuwa na uwezo wa kutumia vyombo vya muziki, lakini walichagua kutokutumia kama sehemu ya ibada yao. Ilikuwa ni sifa inayolitofautisha kanisa la Bwana.

Ben Moseley
Profesa wa Chuo Kikuu na Mhudumu

Je, kanisa unalohudhuria lina sifa hizi za kipekee? Je, kanisa unalohudhuria linaabudu kulingana na Biblia? Alama za kipekee za uimbaji wa kutumia mdomo, na alama nyingine za kipekee za ibada (pamoja na msingi, mpangilio, jina, Mwanzilishi na Mjenzi wa kipekee), vyote ni sehemu ya muhimu ya kile kinachounda nyumba ya Mungu ya Agano Jipya. Sifa hizi za kipekee ni baadhi tu ya mifano inayopatikana kwenye Agano Jipya inayodhihirisha upekee wa asili ya kanisa la Bwana. Sifa nyingine za kipekee za nyumba ya Mungu zinaweza zikajumuisha:

Mafundisho yake (Neno la Mungu)

Mafundisho ya kipekee ya nyumba ya Mungu (kanisa) ni Biblia, neno la Mungu (2 Timotheo 3:16-17).

Kazi zake (Uinjilisti, Uelimishaji, Huruma)

Kama nyumba ya Mungu, kanisa pia limejumuisha mtazamo wa kipekee wa kazi (Mathayo 28:18-20; 1 Wakorintho 16:1-2) unaohusisha uinjilisti, uelimishaji/uimarishaji wa washiriki wake na huruma (kuwasaidia wale wenye mahitaji).

Ushirika wake

Nyumba ya Mungu ina ushiriki wa kipekee unaoundwa na watu ambao wamejitoa kuwa wanafunzi wa Kristo (Mdo. 6:7), na ambao wanaitwa tu “Wakristo” (Mdo. 11:26; 1 Petro 4:16). Majina mengi ya kidini yanayotumika leo hayakuwepo kwenye karne ya kwanza. Badala yake, waumini waliobatizwa katika Biblia walilitumia jina la yule aliyeyatoa maisha yake pale Kalvari – Kristo.

Ukuhani wake

Kujifunza Agano Jipya kunaonesha kwamba kila mkristo binafsi ni sehemu ya ukuhani (1 Petro 2:9; Ufunuo 1:5-

Alama za pekee za kanisa:

Mafundisho
Kazi
Ushiriki
Ukuhani
Watumishi



Nyumba ya Mungu

6; pia Wagalatia 3:27). Kulingana na Biblia, madaraja ya makasisi/watu wa kawaida hayapaswi kuwepo. Machoni pa Mungu, kila muumini aliyebatizwa ni kuhani, na kwa njia hiyo, ana uwezo (anatarajiwa) kuhudumu ndani ya nyumba/hekalu la Mungu.

Watumishi wake

Hatimaye, nyumba ya Bwana ina watumishi kama vile mashemasi na wahubiri (au wainjilisti) ambao wanahitajika kuwa na sifa fulani fulani kama zilivyotajwa katika 1 Timotheo 3:8-13 na 2 Timotheo 4:5. Watu hawa ni watumishi tu katika mwili wa Kristo ambao pamoja na washiriki wengine wa kanisa, wanakatazwa kutumia majina

ya kidini kama vile “baba” au “mtukufu”

Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni (Mathayo 23:9).

Amewapelekea watu wake ukombozi, Ameamuru agano lake liwe la milele, Jina lake ni takatifu la kuogopwa (Zaburi 111:9, Kiswahili - Union Version).

Katika kujibu swali letu kuu la pili, tunaweza tukaona wazi kabisa kwamba nyumba ya Mungu ina sifa nyingi tofauti za kipekee. Katika kila sifa, tunaweza tukaona jinsi kanisa la Yesu Kristo linavyopaswa kupangiliwa, namna ambayo ibada yake inapaswa kuwa na kitu gani cha kufundisha.

SEHEMU YA MARUDIO: JE, NI ZIPI SIFA ZA KIPEKEE ZA NYUMBA YA MUNGU?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu

MASWALI YA KUJIFUNZA

- Kulingana na Waebrania 13:8, nyumba ya Mungu inapaswa kujengwa juu ya Yesu Kristo, yeye ambaye ni “yule yule jana, leo na _____.”
- Kulingana na Warumi 16: 16:
 - Je, tunasoma kuhusu kanisa la Kristo katika Biblia? NDIYO/HAPANA
 - Je, itakuwa ni makosa kuiita nyumba ya Mungu (kanisa) kwa jina hili? NDIYO/HAPANA
 - Je, jina hili linampa utukufu yeye aliyelijenga kanisa na kulinunua kwa damu yake mwenyewe? NDIYO/HAPANA
- Kulingana na Mdo. 14:23 na mistari hapo chini:
 - Je, ni cheo au uongozi gani katika kanisa unaojadiliwa katika vifungu hivi? _____
 - Je, neno mzee na askofu linazungumzia cheo kimoja? NDIYO/HAPANA
 - Je, mzee ni lazima awe ameo? NDIYO/HAPANA
 - Je, mzee ni lazima awe na watoto? NDIYO/HAPANA
 - Je, mtu aliyeongoka hivi karibuni (mchanga) anaweza akatumika kama mzee? NDIYO/HAPANA
 - Mtu aliyeongoka hivi karibuni anaweza akatumika kama mzee? NDIYO/HAPANA

Ni neno la kuaminiwa; mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema. Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu,

Sura ya 5

mkaribishaji, ajuaye kufundisha; si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wa kujadiliana, wala asiwe mwenye kupenda fedha; mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu; (yaani, mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje Kanisa la Mungu?) Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya ibilisi. Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje; ili asianguke katika lawama na mtego wa ibilisi (1 Timotheo 3:1-7).

Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru; ikiwa mtu hakushitakiwa neno, naye ni mume wa mke mmoja, ana watoto waaminio, wasioshitakiwa kuwa ni wafisadi wala wasiotii. Maana imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno, kwa kuwa ni wakili wa Mungu; asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake, asiwe mwepesi wa hasira, asiwe mlevi wala mgomvi, asiwe mpenda mapato ya aibu; bali awe mkaribishaji, mpenda wema, mwenye kiasi, mwenye haki, mtakatifu, mwenye kudhibiti nafsi yake; akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga (Tito 1:5-9).

4. Kulingana na Mdo. 14:23, 1 Petro 5:1, na mistari hapo chini, Je, maneno kama "mzee," "mchungaji," "msimamizi," na "askofu" ni maneno yanayotumika kwa kubadilishana ambayo huelezea cheo kimoja? NDIYO/HAPANA

Toka Mileto Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa (Mdo. 20:17).

Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe (Mdo. 20:28).

5. Je, kuna mamlaka yeyote ya kibiblia, kwa kikundi cha wazee, au askofu mmoja, kuwa na mamlaka nje ya kusanyiko la mahali pamoja (lake)? NDIYO/HAPANA
6. Kulingana na Yohana 4:24, Je, tunapaswa kumwabudu Mungu kulingana na kweli? NDIYO/HAPANA
7. Kulingana na mistari hapo chini:

a. Je, ukweli ni nini? _____

b. Kutokana na kwamba tunapaswa kumwabudu Mungu katika kweli (Yohana 4:24), Je, tunapaswa kumwabudu Mungu kama alivyoelekeza katika Biblia? NDIYO/HAPANA

Maneno haya aliyasema Yesu; akainua macho yake kuelekea mbinguni, akasema: "Baba, ... uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli" (Yohana 17:1,17).

8. Kulingana na Mathayo 15:9, Je, inawezekana kumwabudu Mungu bure? NDIYO/HAPANA
9. Kulingana na mistari hapo chini, wakristo wakutanikapo, wanapaswa _____ kwa Mungu.

Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali (Mdo. 2:42).

Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri (Mdo. 4:31).

Nyumba ya Mungu

10. Kulingana na mistari hapo chini, "Paulo _____" wanafunzi ambao walikutana ili kumega mkate siku ya kwanza ya juma.

Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutanika ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafululiza maneno yake hata usiku wa manane (Mdo. 20:7).

11. Kulingana na 2 Wakorintho 9:6-9 na mistari hapo chini, Wakristo wanafundishwa kwamba wanapokutana pamoja katika siku ya kwanza ya juma, wanapaswa _____ kwenye hazina ya kawaida.

Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja (Wakorintho 16:1-2).

12. Kulingana na Mdo. 20:7 na Mdo. 2:42, wakristo wanapokutana siku ya kwanza ya juma, wanapaswa _____ (mf. Kushiriki Meza ya Bwana).

13. Kulingana na Wakolosai 3:16 na mistari hapo chini, Wakristo wanapokutana ili kuabudu, wanapaswa _____ Mungu.

Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu (Waefeso 5:19).

Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia; nitaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia (1 Wakorintho 14:15).

14. Kulingana na Wakolosai 3:16, Waefeso 5:19 na 1 Wakorintho 14:15, Je, maandiko yanatoa mamlaka yeyote kwa ajili ya matumizi ya vyombo vya muziki katika kumwabudu Mungu? NDIYO/HAPANA

15. Mungu aliposema kwamba tunapaswa "kuimba," amri hiyo inaondoa aina nyingine zote za _____.

16. Je, itakuwa ni makosa kuongeza mchele, Coka – Cola, na vyombo vya muziki kwenye ibada ya kanisa? NDIYO/HAPANA

17. Kulingana na mistari hapo chini, Je, kila mkristo binafsi ni sehemu ya ukuhani? NDIYO/HAPANA

Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu (1 Petro 2:9).

Tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake, na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una yeye hata milele na milele. Amina (Ufunuo 1:5-6).

MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

Sura ya 5

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Je, mjenzi wa kanisa unalohudhuria ni nani? _____
- B. Je, wewe ni sehemu ya kanisa lililojengwa na kuanzishwa na Yesu? NDIYO/HAPANA
- C. Je, sifa za kipekee za nyumba ya Mungu, kama zilivyotajwa katika sehemu hii, zinapatikana kwenye kanisa unalohudhuria? NDIYO/HAPANA
- D. Kama kanisa unalohudhuria haliabudu kulingana na Biblia, Je, inakubalika kwa wewe kuendelea kulishikilia kanisa kama hilo? NDIYO/HAPANA

MASUALA YA MAZUNGUMZO

- A. Kulingana na 2 Timotheo 3: 16-17, mafundisho ya kipekee ya nyumba ya Mungu (kanisa) ni Biblia, neno la Mungu. Je, kuna sehemu yeyote katika Biblia inayoruhusu miongozo na mafundisho ya wanadamu?
- B. Kulingana na 1 Petro 2: 9, Ufunuo 1: 5-6, na Wagalatia 3: 27, kila mkristo binafsi ni sehemu ya ukuhani. Je, kuna mahali popote ndani ya kanisa la Kristo penye mfumo wa kikasisi/ushiriki wa kawaida?
- C. Kulingana na mistari hapo chini, Biblia inalichukulia kanisa kama bibi harusi wa Kristo. Je, hili linahusiana vipi na jina la kanisa, na uhusiano lililokuwa nao na bwana harusi wake?

Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa. Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe. Maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake po pote; bali huulisha na kuutunza, kama Kristo naye alivyolitendea kanisa. Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake. Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa. Lakini kila mtu ampende mke wake kama nafsi yake mwenyewe; wala mke asikose kumstahi mumewe (Waefeso 5:22-33).

Ndugu zangu, hamjui (maana nasema na hao waijuao sheria) ya kuwa torati humtawala mtu wakati anapokuwa yu hai? Kwa maana mwanamke aliye na mume amefungwa na sheria kwa yule mume wakati anapokuwa yu hai; bali akifa yule mume, amefunguliwa ile sheria ya mume. Basi wakati awapo hai mumewe, kama akiwa na mume mwingine huitwa mzinzi. Ila mumewe akifa, amekuwa huru, hafungwi na sheria hiyo, hata yeye si mzinzi, ajapoolewa na mume mwingine. Kadhalika, ndugu zangu, ninyi pia mmeifia torati, kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya mwingine, yeye aliyefufuka katika wafu, kusudi tumzalie Mungu matunda. (Warumi 7:1-4).

Maana nawaonea wivu, wivu wa Mungu; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi (2 Wakorintho 11:2)



Nyumba ya Mungu

JE, LEO TUNaweza KUIANZI SHA NYUMBA YA MUNGU?

Sasa, hebu tujiulize swali letu la tatu: “Je, tunaweza kuanzisha nyumba hii leo?” kwa maneno mengine, Je, nyumba ambayo ilijengwa na kuanzishwa na Yesu katika karne ya kwanza – kanisa ambalo tunalisoma kwenye Biblia – inaweza kuanzishwa au kujengwa leo katika jamii yako au jirani yako? Hebu tumuulize mtu ambaye aliwahi kuwa fundi mwashi na muhubiri pia.

Makanisa yanafanana sana na nyumba. Nyumba zina ubunifu, na hivyo basi ni lazima ziwe na mbunifu. Nyumba zina misingi na miundo. Zina sifa za kipekee ambazo huzifanya ziwe za kipekee kwa wale wanaozimiliki. Na kitu kingine ambacho kila nyumba inayo ni ramani. Katika kujenga nyumba, siwezi kujua wapi pa kuanzia bila kuwa na ramani. Kwa kufuata ramani, ninaweza kujenga nyumba vile vile kama mbunifu au mkandarasi alivyokusudia. Lakini cha msingi ni kama ningelichukua ramani, ningeliweza kujenga nyuma kama hiyo hiyo Amerika ya Kaskazini au Kusini, Australia, Afrika, Ulaya au Asia. Ilimradi tu vifaa vya ujenzi vipatikane, wakati huu ninaweza kujenga nyumba inayofanana katika kila moja wapo ya maeneo hayo, au miaka hamsini kutoka sasa, kwa kufuata tu ile ramani.

Inapokuja katika suala la kujenga nyumba ya Bwana, Ninaweza kufanya kitu hicho hicho. Ninaweza kuchukua Biblia na kuitumia kama kielelezo au ramani, na nikajenga kanisa upande wa Amerika ya Kaskazini au Kusini, Afrika, au mahali pengine popote. Kama nikifuata maelekezo yake hasa katika maeneo kama ya mpangilio wake, jina lake na ibada yake, na kama nikifundisha kile tu kilichofunuliwa katika Biblia kuhusu jinsi ya kuingia na kuwa mshiriki, Je, hiyo haitakuwa nyumba ya Mungu? Kama nikichukua kitabu cha mwongozo cha kimadhehebu, nikakisoma na kuanzisha dhehebu kupitia sheria zake ndogo ndogo, Je, ni kwa nini nisisome tu Agano Jipya la Kristo na nikalitumia kuanzisha kanisa la Kristo? Ama kwa hakika, “Kanisa la Kristo” na “nyuma ya Mungu” ni kitu kimoja kinachofanana. Kama ninataka kuanzisha nyumba ya Mungu kwenye jamii ye yote, basi ni bora nifuate ramani inayopatikana kwenye Agano Jipya.

Thomas Moore
Mhudumu na Fundi Mwashi

Ni ukweli kwamba Biblia inapaswa (na ni lazima) itumiwe kama ramani yetu kwa kuanzisha kanisa na kwa ajili ya kuishi maisha ya ukristo. Kwa mfano, angalia kile mtume Paulo alichosema kuhusu neno la Mungu kuwa ndilo ramani au kielelezo.

Shika kielelezo cha maneno yenye uzima uliyoyasikia kwangu, katika imani na upendo ulio katika Kristo Yesu (2 Timotheo 1:13).

Soma pia, kile Paulo alichosema kuhusu kufuata mapokeo yaliyoanzishwa na mitume katika neno lililoandikwa.

Basi, ndugu, simameni imara, mkayashike mapokeo mliyofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa waraka wetu (2 Wathesalonike 2:15).

Kulingana na Waefeso 2:19-22, mitume walioteuliwa na Mungu walimsaidia Yesu katika kuuweka msingi wa kanisa. Tunajifunza kutoka katika kitabu cha Mathayo 16:19 kwamba chochote watakacho fungua au kufunga hapa duniani (kulingana na nguvu ya neno la Kiyunani lililotumika katika kifungu hiki) kitakuwa kimefungwa au kufunguliwa mbinguni. Kama mabalozi wa Bwana (2 Wakorintho 5:20), mitume walianzisha kanisa wakitarajia kwamba wafuasi wote wa Yesu walifuata. Amri za mitume na matendo yote yameelezewa kwa undani katika kurasa za Agano Jipya. Agano Jipya ndilo ramani ya kanisa, na ndiyo ramani ambayo sisi tunapaswa kuifuata leo. Kama tunataka kuuendeleza ushirika wetu katika mwili wa Kristo, basi, tunapaswa



Sura ya 5

kuyatii mapokeo yaliyowekwa na mitume kwenye Agano Jipya.

Na ikiwa mtu awaye yote halishiki neno letu la waraka huu, jihadharini na mtu huyo, wala msizungumze naye, apate kutahayari (2 Wathesalonike 3:14).

Hivyo basi, katika kulijibu swali letu kuu la tatu, “Je, leo tunaweza kuijenga nyumba ya Mungu?” Tunapaswa kujibu kwa sauti kubwa kabisa, “Ndiyo!” Kwa hakika, si tu kwamba tunaweza kuijenga nyumba ya Mungu leo, lakini la muhimu zaidi sana, tunapaswa kuijenga kulingana na maelekezo ya Mungu kama yalivyofunuliwa katika kile mitume walichoandika kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Kufuata mamlaka ya mitume yaliyofunuliwa katika

maandiko ya Agano Jipya si suala la uchaguzi. Hivyo basi, kile kilichoandikwa, ni lazima tukifuata na tukitii. Na kulingana na Kumbukumbu 4:2, hatupaswi kuongeza katika neno la Mungu. Onyo hilo hilo limetolewa pia katika Agano Jipya.

Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki (Ufunuo 22:18-19).

SEHEMU YA MARUDIO: JE, LEO TUNAWENZA KUIANZISHA NYUMBA YA MUNGU?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na 2 Timotheo 1: 13 na 2 Wathesalonike 2: 15, Je, Biblia ndiyo ramani au kielelezo chetu kwa ajili ya kuijenga nyumba ya Mungu? NDIYO/HAPANA
2. Kulingana na 2 Wathesalonike 2:15 na 2 Wathesalonike 3:14, kanisa ni lazima liyatii na “kuyashika _____” yaliyowekwa na mitume kwenye Agano Jipya.
3. Kulingana na mistari hapo chini, kutokana na kwamba mitume walikuwa ni mabalozi wa Kristo, na walipewa mamlaka ya kuanzisha kanisa ambalo wafuasi wote wa Kristo wanapaswa kulifuata, wakristo leo wanapaswa _____ amri za mitume na kufuata matendo yao yaliyoelezewa ndani ya kurasa za Agano Jipya.

Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihii kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu (2 Wakorintho 5:20).

Nami nakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni (Mathayo 16:19).

4. Kulingana na 2 Wathesalonike 3:14, wakristo hawapaswi _____ na wale watu ambao hawayashiki maneno ya mitume kama yanavyopatikana katika maandishi yao (au nyaraka).

Nyumba ya Mungu

5. Je, leo tuna maelezo ya kutosha ndani ya Agano Jipya ya jinsi ya kujenga nyumba ya Mungu? NDIYO/HAPANA
6. Kulingana na Ufunuo 22:18-19 na mstari hapo chini, hatupaswi ama _____ wala _____ neno la Mungu.

Msiliongeze neno niwaamurulo wala msilipunguze, mpate kuzishika amri za BWANA, Mungu wenu, niwaamuruzo (Kumbukumbu 4:2).

MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Je, wewe ni mshiriki wa kanisa ambalo limeanzishwa kulingana na maelekezo ya Mungu kama yalivyofunuliwa katika kile mitume walichoandika kwa msaada wa Roho Mtakatifu? NDIYO/HAPANA
- B. Agano Jipya linatoa ramani ya kujenga nyumba ya Bwana. Je, kanisa ambalo wewe ni mshiriki wake limejengwa kulingana na ramani iliyotolewa na Mungu? NDIYO/HAPANA
- C. Kama sivyo, Je, uko tayari kuitafuta nyumba ya Bwana? NDIYO/HAPANA
- D. Kama kanisa la Kristo halipo katika jamii unayoishi, Je, wewe na/au wengine mkotayari kuichukua Biblia pekee na kuanzisha kanisa? NDIYO/HAPANA.

MASUALA YA MAZUNGUMZO.

- A. Eleza ni kwa nini kanisa la Kristo linapaswa kufanana ulimwengu mzima.
- B. Kulingana na 2 Timotheo 1:13, Wakristo wanapaswa "kukishika kielelezo cha maneno yenye uzima" kinachopatikana ndani ya ramani ambayo ni Biblia. Eleza ni nini kinaweza kutokea kama wakristo hawatafanya hili.
- C. Je, wengine kwa takribani miaka 2000 iliyopita wamejaribu kubadilisha na/au kuboresha nyumba ya Mungu? Kwa njia zipi?



Sura ya 5

HITIMISHO

Sasa hebu tujiulize: Je, wewe au wale ambao unaabudu pamoja nao, mmeongeza kitu fulani katika nyumba ya Bwana ambacho hakikukusudiwa au kuamriwa na Mungu? Je, kanisa unalohudhuria lina sifa ambazo zimefunuliwa katika Agano Jipya? Kama ungefanya ulinganifu kati ya kanisa la Agano Jipya na kanisa unalohudhuria, Je, ungegundua kama limejengwa juu ya Yesu? Je, kanisa ambalo wewe ni sehemu yake, linatumia jina la Kristo? Je, Yesu ndiye kichwa cha kanisa unalohudhuria? Je, limepangiliwa kwa kuwa na wazee na mashemasi wenye sifa? Je, linaabudu katika kweli? Na hatimaye, Je, kanisa unaloabudu sasa linafundisha kwamba kuna kanisa moja tu ambalo waumini waliobatizwa huzidishwa kwalo? Kama sivyo, basi tunakusihi, nenda leo ukatafute kanisa la kweli la Kristo.

Mpaka hapa katika kutafuta kwetu ukweli, tumeona kwamba kwa hakika Bwana anayo nyumba, na ya kwamba nyumba yake ni kanisa, ufalme. Pia tumejifunza kwamba, Yesu ni Mjenzi wa nyumba hiyo, na kwamba nyumba yake ina sifa mbalimbali za kipekee za utambulisho. Pia tumejifunza kwamba katika kuianzisha nyumba ya Mungu leo, tunapaswa kuifuata ramani iliyofunuliwa katika Agano Jipya, na ya kwamba hatupaswi kupindisha chochote kutoka katika mpango wake.

Je, wewe ni mshiriki wa nyumba ya Mungu? Kama ndivyo, Je, umewahi kuwa na hatia ya kukiharibu kielelezo cha kuanzisha nyumba ya Mungu? Bwana ana nyumba moja tu. Kama kanisa moja la kweli linapatikana katika jamii yako, sasa ni kwa nini usiende kulitafuta? Kama halipatikani, basi tunakusihi uiendee Biblia (ambayo ndiyo chanzo cha pekee cha ukweli cha kuanzisha kanisa hilo), na uanze leo kulirejeza kanisa kama lilivyobuniwa na Yesu.

Katika Yohana 4:24, tunajifunza kwamba wale wamwabuduo Mungu imewapasa kumwabudu katika Roho na Kweli. Kulingana na Yohana 17:17, Neno la Mungu ni kweli. Je, wewe unamwabudu Mungu kulingana na kweli? Je, wewe ni sehemu ya kanisa ambalo lilianzishwa juu ya kweli? Yesu alisema, "Mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru" (Yohana 8:32).

MARUDIO YA SURA

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana ndani ya sura.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na 1 Timotheo 3:15, "Nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa _____."

2. Kulingana na mstari hapo chini, kanisa ni _____ la Mungu, na Roho wake hukaa ndani yao.

Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? (1 Wakorintho 3:16).

3. Kulingana na mistari hapo chini, nyumba ya Mungu ina ushirika wa kipekee pia, unaoundwa na watu ambao wanatumia jina la _____ na wanatafuta jinsi ya kumtukuza Mungu kwa jina hili.

Hata alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia (Mdo. 11:26).

Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu kwa katika jina hilo (1 Petro 4:16, Union Version).

MASWALI YA KUTILIA MKAZO

1. Kulingana na Wakolosai 1:17-18, Je, kichwa cha kanisa ni nani?

Nyumba ya Mungu

2. Nyumba ya Bwana inaweza kutofautishwa na nyumba nyingine kwa kupitia _____ zake za kipekee.

3. Kama mtu akifuata ramani inayopatikana katika Agano Jipya, Je, nyumba ya Mungu (kanisa la Kristo) inaweza ikaanzishwa leo? NDIYO/HAPANA

MAJIBU kwa ajili ya **MASWALI YA KUJIFUNZIA** na **MASWALI YAKUTILIA MKAZO** yanapatikana nyuma ya kitabu.

MAMBO UNAYOPASWA KUJUA

- Kanisa ni nyumba ya Mungu.
- Yesu ndiye mjenzi wa kanisa.
- Yesu ana mamlaka yote dhidi ya kanisa lake.
- Kanisa lililojengwa na Kristo huvaa jina la Kristo.
- Kanisa lililojengwa na Kristo limepangiliwa kwa kuwa na wazee (pia hufahamika kama maaskofu, wachungaji na waangalizi).
- Kanisa lililojengwa na Kristo huabudu bila ya kutumia vyombo vya muziki.
- Kanisa lililojengwa na Kristo hushiriki meza ya Bwana kila siku ya kwanza ya juma.
- Kitabu pekee cha “mwongozo” kinachotumiwa katika nyumba ya Mungu ni Biblia.
- Kanisa lililojengwa na Yesu lina mafundisho, kazi, ushiriki na ukuhani wa kipekee.

CHIMBA ZAIDI

Masomo hapo chini yamekusudiwa kwa wale ambao wangependa kujifunza somo hili kwa undani zaidi. Kuna maelezo ambayo kimsingi hayakujadiliwa katika somo.



KUHUSU KANISA (AU UFALME)

... wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni na kuiamini Injili (Marko 1:15).

Akawaambia, “Amin, nawaambia, Pana watu kati ya hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapouona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu.” (Marko 9:1).

Akakaa muda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake aliyokuwa ameipanga, akawakaribisha watu wote waliokuwa wakimwendea, akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu (Mdo. 28:30-31).

Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakatifu (1 Wakorintho 1:2).

Hapo ndipo mwisho, atakapompa Mungu Baba ufalme wake; atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu. Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake (1 Wakorintho 15:24-25).

Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake (Wakolosai 1:13).

Nakuandikia hayo nikitaraji kuja kwako hivi karibu. Lakini nikikawia, upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli (1 Timotheo 3:14-15).

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

1. Je, Yesu alifundisha katika Marko 1:15 kwamba kanisa (ufalme) “ulikuwa mbali sana” kutoka kwa watu aliokuwa akizungumza nao? NDIYO/HAPANA
2. Katika Marko 9:1, Je, Yesu alisema kwamba baadhi ya watu ambao alizungumza nao watakuwa hai wakati ufalme utakapokuja? NDIYO/HAPANA
3. Kulingana na Mdo. 28:30-31, Je, ni kitu gani Paulo aliwahubiria wale watu waliokwenda kumtembelea wakati alipokuwa amefungiwa katika nyumba huko Rumi? _____

Sura ya 5

4. Mwisho wa wakati, Bwana atatoa kitu fulani kwa Baba yake (1 Wakorintho 15:24-25). Je, ni kitu gani hicho?

5. Je, Paulo alimwambia Timotheo (1 Timotheo 3:14-15) kwamba “nyumba ya Mungu” na “kanisa” ni kitu kimoja? NDIYO/HAPANA



KUHUSU WASHIRIKI WA KANISA

Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu. Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu (Mathayo 5:11-12).

Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka. (Mathayo 10:22).

Ulimwengu hauwezi kuwachukia ninyi; bali hunichukia mimi, kwa sababu mimi naushuhudia ya kuwa kazi zake ni mbovu (Yohana 7:7)

Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi (Yohana 15:18)

..... Na wanafunzi waliitwa wakristo kwanza hapo Antiokia (Mdo. 11:26).

Nami nikayafanya hayo Yerusalemu; niliwafunga wengi miongoni mwa watakatifu ndani ya gereza, nikiisha kupewa amri na wakuu wa makuhani; na walipouawa nilitoa idhini yangu. Na mara nyingi katika masinagogi yote naliwaadhibu, nikawashurutisha kukufuru; nikawaonea hasira kama mwenye wazimu, nikawaudhi hata katika miji ya ugenini (Mdo. 26:10-11).

Agripa akamwambia Paulo, “kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo” (Mdo. 26:28).

Maana mmesikia habari za mwenendo wangu zamani katika dini ya Kiyahudi, kwamba nililiudhi kanisa la Mungu kupita kiasi, nikaliharibu (Wagalatia 1:13).

Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo (1 Petro 4:16).

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

6. Katika vifungu kama Mathayo 5:11-12, Yohana 15:18 na Mathayo 10:22, Je, Yesu alisema kwamba wafuasi wake watachukuliwa na kutendewa kwa upendeleo na watu wengi wa ulimwengu? NDIYO/HAPANA

7. Je, wanafunzi wa Kristo waliitwaje “kwanza” katika mji wa Antiokia? _____

8. Kulingana na Mdo. 26:28, Je, jina “Mkristo” liliwahi kutumiwa na viongozi wakipagani wakiwazungumzia wanafunzi wa Kristo? NDIYO/HAPANA

9. Je, Petro, kama mtume wa Bwana, alilitumia jina “Mkristo” (1 Petro 4:16) akiwazungumzia wanafunzi wa Kristo? NDIYO/HAPANA

10. Katika Wagalatia 1:13, Paulo alisema kwamba aliliudhi “kanisa la Mungu.” Katika Mdo. 26:10-11, hata hivyo, alisema kwamba aliwaudhi “watakatifu.” Sasa basi, kanisa linaundwa na akina nani?

11. Kulingana na Mdo. 11:26, Je, jina lingine la hao “watakatifu” ni lipi? _____



KUHUSU VIONGOZI NA VYEO KATIKA KANISA

Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe (Mdo. 20:28).

Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu; si wenye kauli mbili, si watu wa kutumia mvinyo sana, si watu wanaotamani fedha ya aibu; wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi. Hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye waitende kazi ya shemasi, wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia. Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi, waaminifu katika mambo yote. Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja, wakiwasimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao. Kwa maana watendao vema kazi ya shemasi hujipatia daraja zuri, na ujasiri mwingi katika imani iliyo katika Kristo Yesu (1 Timotheo 3:8-13).

Wazee watawalao vema na wahesabiwe kustahili heshima maradufu; hasa wao wajitaabishao kwa kuhutubu na kufundisha (1 Timotheo 5:17).

Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru; ikiwa mtu hakushitakiwa neno, naye ni mume wa mke mmoja, ana watoto waaminio, wasioshitakiwa kuwa ni wafisadi wala wasiotii. Maana imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno, kwa kuwa ni wakili wa Mungu; asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake, asiwe mwepesi wa hasira, asiwe mlevi wala mgomvi, asiwe mpenda mapato

Nyumba ya Mungu

ya aibu; bali awe mkaribishaji, mpenda wema, mwenye kiasi, mwenye haki, mtakatifu, mwenye kudhibiti nafsi yake; akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga (Tito 1:5-9)

Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia neno la Mungu; tena, kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni imani yao (Waebrania 13:7).

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

12. Kulingana na Tito 1:5-9, Je, ni mapenzi ya Mungu kwamba kanisa liwe na wazee (wachungaji, waangalizi, maaskofu)? NDIYO/HAPANA
13. Je, Mdo. 20:28 inafundisha kwamba wachungaji wa kanisa la Mungu wanapaswa kuangalia mambo yote ya kiroho ya wakristo wanaoliunda kanisa? NDIYO/HAPANA
14. Kulingana na Tito 1:5-9, Je, wanaume wanaohudumu kama wazee (wachungaji, waangalizi, maaskofu) wanapaswa wawe na sifa fulani fulani kama zilivyotajwa na Mungu katika neno lake? NDIYO/HAPANA
15. Je, Paulo alimwambia Timotheo kwamba yalikuwa ni mapenzi ya Mungu kwa kanisa kuwa na watumishi waliofahamika kama “mashemasi” (1 Timotheo 3:8-13)? NDIYO/HAPANA
16. Kulingana na 1 Timotheo 3:8-13, Je, wanaume wanaotumika kama mashemasi (watumishi) wanapaswa wawe na sifa fulani fulani kama zilivyowekwa na Mungu katika neno lake? NDIYO/HAPANA
17. Kulingana na Waebrania 13:7, Je, wakristo wanapaswa kuwaheshimu na kuwatii hao wazee (waangalizi) “wanaolisimamia” kanisa? NDIYO/HAPANA



KUHUSU IBADA YA KANISA

Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli (Yohana 4:24).

Kuhubiri ...

Niwaambialo ninyi katika giza, lisemeni katika nuru; na msikialo kwa siri, lihubirini juu ya mimbari (Mathayo 10:27).

Akatuagiza tuwahubiri watu na kushuhudia ya kuwa huyu ndiye aliyeamriwa na Mungu awe Mhukumu wa walio hai na wafu (Mdo. 10:42).

Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikiaje pasipo mhubiri? Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema (Warumi 10:14-15).

Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana; na sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya Yesu (2 Wakorintho 4:5).

Lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaa na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho (2 Timotheo 4:2).

Kuomba...

Yesu akajibu, akawaambia, “Amin, nawaambia Mkiwa na imani, msipokuwa na shaka, mtafanya si hilo la mtini tu, lakini hata mkiuambia mlima huu, ‘ng’oka, ukatupwe baharini,’ litatendeka. Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea” (Mathayo 21:21-22).

Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko (Marko 1:35).

Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma (Yohana 17:20-21).

Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani (Wakolosai 4:2).

Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii (Yakobo 5:16).

Kutoa...

Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoyaamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kweni na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja (1 Wakorintho 16:1-2).

Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mtu na atenda kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu (2 Wakorintho 9:6-7).

Meza ya Bwana...

Hata saa ilipofika aliketi chakulani, yeye pamoja na wale mitume pamoja naye. Akawaambia, “Nimetamani

Sura ya 5

sana kuila pasaka hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu; kwa maana nawaambia ya kwamba siili tena hata itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu.” Akapokea kikombe, akashukuru, akasema, “Twaeni hiki, mgawanye ninyi kwa ninyi; Maana nawaambia ya kwamba tangu sasa sinywi mazao ya mzabibu hata ufalme wa Mungu utakapokuja.” Akatwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa, akisema, “[Huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yangu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.” Kikombe nacho vivyo hivyo baada ya kula; akasema, “Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, inayomwagika kwa ajili yenu.]” (Luka 22:14-20).

Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, “Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.” Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, “kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.” Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo (1 Wakorintho 11:23-26).

Kuimba...

Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia; nitaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia (1 Wakorintho 14:15).

.... Bali mjazwe Roho; mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu (Waefeso 5:18-19).

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

18. Kulingana na Yohana 4:24, watu wanapaswa wamwabudu Mungu katika _____ na _____.
19. Kulingana na Warumi 10:14-15, Je, kuhubiri ni jambo la msingi katika kuieneza Injili? NDIYO/HAPANA
20. Je, 2 Wakorintho 4:5 inafundisha kwamba wale wanaohubiri hawapaswi kuhubiri kuhusu nafsi zao, bali kuhusu Kristo? NDIYO/HAPANA
21. Kulingana na 2 Timotheo 4:2, Paulo alimwambia Timotheo awe tayari kuhubiri wakati _____ na wakati _____.
22. Kulingana na Marko 1:35 na Yohana 17:20-21, Je, sala ilikuwa ni jambo la msingi/muhimu kwa Yesu Kristo? NDIYO/HAPANA
23. Kulingana na Wakolosai 4:2, wakristo wanapaswa wa _____ katika maombi.
24. Je, Yakobo 5:16 inafundisha kwamba maombi ya

mkristo mwenye haki yafaa sana? NDIYO/HAPANA

25. Kulingana na 1 Wakorintho 16:1-2, Mkristo anatakiwa amtotee Bwana “ kwa kadiri ya _____.”
26. Katika 2 Wakorintho 9:6-7, Paulo amefundisha kwamba Mungu humpenda _____.
27. Kulingana na Luka 22:14-20, Je, Meza ya Bwana ilianzishwa na mwanadamu? NDIYO/HAPANA
28. Kulingana na 1 Wakorintho 11:23-26, Je, wakristo wanaposhiriki Meza ya Bwana, wanatangaza nini? _____.
29. Kulingana na 1 Wakorintho 14:15, wakristo wanapaswa kuimba kwa _____.
30. Katika Waefeso 5:18-19, “chombo” ambacho Paulo anamwamuru kila mkristo kufanyia “shangwe” ni _____.



KUHUSU KAZI ZA KANISA

Uinjilisti...

Ndipo alipomwambia mwanafunzi wake, “Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake” (Mathayo 9:37-38).

Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari (Mathayo 28:19-20).

Akawaambia, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” (Marko 16:15).

Basi usiuonee haya ushuhuda wa Bwana wetu ambaye alituokoa akatuia kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele, na sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake Mwokozi wetu Kristo Yesu; aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili (2 Timotheo 1:8-10).

Uimarishaji/ujengaji ...

Kwa kuwa yeye amtumikiaye Kristo katika mambo hayo humpendeza Mungu, tena hukubaliwa na wanadamu. Basi kama ni hivyo, na mfuate mambo ya amani na mambo yafaayo kwa kujengana (Warumi 14:18-19).

Nyumba ya Mungu

Basi, farijianeni na kujengana kila mtu na mwenzake, vile vile kama mnavyofanya. Lakini, ndugu, mwatambue wale wanaojitaabisha kwa ajili yenu, na kuwasimamia ninyi katika Bwana, na kuwaonyeni; mkawastahi sana katika upendo, kwa ajili ya kazi zao. Iweni na amani ninyi kwa ninyi (1 Wathesalonike 5:11-13).

Huruma...

Basi, yo yote mtakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo ... (Mathayo 7:12).

“Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote.” Na ya pili ndiyo hii, “Mpende jirani yako kama nafsi yako.” Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi (Marko 12:30-31).

Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio (Wagalatia 6:10).

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

31. Kila mwanafunzi wa Yesu anapaswa ajihusisha na uinjilisti kwa sababu “mavuno ni _____ bali watenda kazi ni _____” (Mathayo 9:37-38).
32. Katika Mathayo 28:19-20 na Marko 16:15, Je, Yesu amewaamuru wafuasi wake kuihubiri Injili ulimwenguni kote? NDIYO/HAPANA
33. Katika 2 Timotheo 1:8-10, Paulo anazungumza ukweli kwamba kupitia Injili, Yesu aliondoa _____ na kuleta _____.
34. “Basi kama ni hivyo, na mfuate mambo ya _____ na mambo yafaayo kwa _____” (Warumi 14:19).
35. Kulingana na 1 Wathesalonike 5:11-13, Je, wakristo wanaambiwa wawatambue na kuwastahi wazee (maaskofu, waangalizi) wao? NDIYO/HAPANA
36. Je, Mathayo 7:12 inafundisha kwamba tunapaswa kuwatendea wengine kile tunachotaka wao watutendee? NDIYO/HAPANA
37. Katika sehemu ya mwisho ya Marko 12:30-31, wakristo wanaambiwa wampende Mungu na majirani zao kwa sababu “hakuna amri nyingine iliyo _____ kuliko hizi.”
38. Je, Wagalatia 6:10 inafundisha kwamba wakristo wanapaswa kuwasaidia wale watu ambao ni wakristo tu? NDIYO/HAPANA



KUHUSU MAFUNDISHO YA KANISA

Basi Yesu akawajibu, akasema, “Mafunzo yangu si yangu mimi, ila ni yake yeye aliyenipeleka. Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu, au kwamba mimi nanena kwa nafsi yangu tu” (Yohana 7:16-17).

Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki (Warumi 6:17-18).

Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo (Waefeso 4:14-16).

Uwakumbushe ndugu mambo hayo, nawe utakuwa mtumishi mwema wa Kristo Yesu, na mzoovu wa maneno ya imani, na mafundisho mazuri yale uliyoyafuata (1 Timotheo 4:6)

Hata nitakapokuja, ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha (1 Timotheo 4:13)

Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo; maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia (1 Timotheo 4:16).

Mtu awaye yote akifundisha elemu nyingine, wala hayakubali maneno yenye uzima ya Bwana wetu Yesu Kristo, wala mafundisho yapatanyo na utauwa, amejivuna; wala hafahamu neno lo lote; bali ana wazimu wa kuwazia habari za maswali, na mashindano ya maneno, ambayo katika hayo hutoka husuda, na ugomvi, na matukano, na shuku mbaya (1 Timotheo 6:3-4).

Maana utakuja wakati watakapo yakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajipusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo (2 Timotheo 4:3-4).

Lakini wewe nena mambo yapasayo mafundisho yenye uzima (Tito 2:1).

Vivyo hivyo na vijana waume uwaonye kuwa na kiasi; katika mambo yote ukijionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema, na katika mafundisho yako ukionyesha usahihi na ustahivu, na maneno yeye uzima yasiyoweza

Sura ya 5

kuhukumiwa makosa, ili yule mwenye kupinga atahayarike, kwa kuwa hana neno baya la kunena juu yetu (Tito 2:6-8).

Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia. Mtu akija kwenu, naye haleti mafundisho hayo, msimkaribishe nyumbani mwenu, wala msimpe salamu. Maana yeye ampaye salamu azishiriki kazi zake mbovu (2 Yohana 9-11).

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

39. Kulingana na Yohana 7:16-17, mafundisho aliyofundisha Yesu yalitoka kwa _____.
40. Kulingana na Warumi 6:17-18, Je, ni muhimu kuyatii mafundisho ya Kristo? NDIYO/HAPANA
41. Katika Waefeso 4:14-16 sababu moja muhimu ya kuyajua na kudumu katika mafundisho ambayo yalifundishwa na Yesu ni ya kwamba yatatusaidia tusiweze kutupwa _____.
42. 1 Timotheo 4:6 inasema kwamba tunapaswa kuwa “wazoevu wa _____ ya imani.”
43. Katika 1 Timotheo 4:13, Timotheo aliambiwa afanye bidii katika kusoma, kuonya na _____.
44. Katika 1 Timotheo 4:16, Timotheo aliambiwa kwamba kujitunza katika maandiko lilikuwa ni jambo la muhimu kwa sababu hii ndiyo njia ambayo _____ nafsi yake na wale wamsikiao.
45. Kulingana na 1 Timotheo 6:3-4, mtu ambaye hafundishi mafundisho ya Kristo katika njia ya uaminifu _____ wala hafahamu _____.
46. “Nena mambo yapasayo _____” (Tito 2:1).
47. Kulingana na Tito 2:6-8. Mambo manne tunayopaswa kuonesha yanayohusiana na mafundisho ni _____ na _____.
48. Kulingana na 2 Yohana 9-11, kama hatudumu katika mafundisho ya Kristo, Je, tunaweza kuwa na uhusiano na Mungu Baba na Yesu? NDIYO/HAPANA



KUHUSU MPATANISHI NA MWOMBEZI WA WAKRISTO

Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu; ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote, utakaoshuhudiwa kwa majira yake (1 Timotheo 2:5-6).

Lakini sasa amepata huduma iliyo bora zaidi, kwa kadiri alivyo mjumbe wa agano lililo bora, lililoamriwa juu ya ahadi zilizobora (Waebrania 8:6).

Na kwa sababu hii ni mjumbe wa agano jipya, ili, mauti ikiisha kufanyika kwa kukomboa makosa yaliyokuwa chini ya agano la kwanza, hao walioitwa waipokee ahadi ya urithi wa milele (Waebrania 9:15).

Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote (1 Yohana 2:1-2).

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

49. Kulingana na 1 Timotheo 2:5-6, Je, kuna wapatanishi wangapi kati ya Mungu na mwanadamu? _____
50. Kulingana na 1 Timotheo 2:5-6, Je, ni nani aliye Mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu? _____
51. Kulingana na Waebrania 9:15, Je, ilimpasa Yesu afe kabla hajawa Mpatanishi wetu? NDIYO/HAPANA
52. Waebrania 9:15 inasema kwamba kama Mpatanishi, Kristo anatuwezesha sisi tuipokee ahadi ya _____.
53. Kulingana na 1 Yohana 2:1-2. Wakristo wana Mwombezi ambaye hutetea mashitaka yao mbele za Mungu. Je, Mwombezi huyo ni nani? _____
54. 1 Yohana 2:1-2 inatufundisha kwamba Yesu aliitoa nafsi yake kama dhabihu kwa ajili ya _____ za ulimwengu wote.

MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUCHIMBA ZAIDI yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

TAFUTA UKWELI

KUHUSU UBATIZO



Sura ya 6

Katika ulimwengu wa leo, kuna mitazamo mingi kuhusu ubatizo. Wengine wanasema kwamba wato-to wanapaswa kubatizwa, wakati wengine wanasema ubatizo unafanywa kwa watu wazima tu. Baa-dhi wanaamini kwamba ubatizo ni muhimu ili mtu apate wokovu, wakati wengine hawaamini. Je, ukweli ni upi kuhusu ubatizo? Je, umeshawahi kujiuliza kama unapaswa kubatizwa au la? Na, kama umebatizwa, Je, ulibatizwa kwa sababu sahihi zinazoelezwa katika Biblia?

UTANGULIZI

Maji! Ni moja kati ya rasilimali zetu za thamani. Bila hayo, ulimwengu kama tunavyoufahamu usingekuwapo. Tunapaswa kuwa nayo ili tuweze kuendesha maisha yetu. Hukata kiu zetu, yanaweza kutuweka safi na yanaweza kutufanya tujisikie kama watu wapya baada ya siku nzima ya kazi ngumu. Je, kuna la kushangaza kwamba katika Biblia, maji yanatumiwa na Mungu kama kitu cha muhimu sana na ishara ya utakaso na usafi?

Ama iwe ni kwenye gharika ya Nuhu ambayo iliisafisha dunia, tamaduni ya utakaso ya Uyahudi ama ubatizo wa maelfu ya watu katika Agano Jipya, maji yamekuwa ni sehemu ya muhimu sana ya mpango wa Mungu katika kuzio-koa roho(nafsi).

Lakini ni kwa jinsi gani, na ni kwa nini yamefanyika kuwa sehemu ya mpango wa Mungu? Je, ni kwa nini walioamini walibatizwa kwa maji? Na Je, ni muhimu kwa mtu kubatizwa leo kwa ajili ya wokovu? Kama ndivyo, mtu anapaswa afahamu nini kabla ya kubatizwa?

Kabla hatujaanza uchunguzi wetu, itasaidia sana kama utajibu maswali kadhaa ya muhimu sana. Andika majibu yako chini ya kila swali katika maswali yafuatayo.

- **Je, kwa sasa upo katika uhusiano wa kuokolewa na Mungu? Kwa maneno mengine, kama ungelikufa leo, Je, ungelikwenda mbinguni?**

- ☐ MBINGUNI
- ☐ JEHANAMU
- ☐ SIJUI

- **Kama kwa sasa haupo katika uhusiano wa kuokolewa na Mungu, Je, kuna wakati fulani ulikuwa katika uhusiano huo?**

- ☐ HAPANA
- ☐ WAKATI ULIOPIITA LAKINI SI SASA
- ☐ SIJUI

- **Kama umeokolewa sasa, au uliokolewa wakati fulani uliopita, Je, uliokolewa kwa njia gani? Kwa maneno mengine, Je, ulipaswa useme au ufanye nini ili uwe mkristo?**

- **Je, umeshawahi kubatizwa? Kama ndiyo, Je, ulifanya kwa njia ya kunyunyiza, kumimina au kuzamisha(kutosa)?**

- ☐ NDIYO, NIMEBATIZWA KWA
 - ☐ KUNYUNYIZIWA MAJI
 - ☐ KUMWAGIWA/KUMIMINIWA MAJI
 - ☐ KUZAMISHWA/KUTOSWA KATIKA MAJI
- ☐ HAPANA, SIJAWAHI KUBATIZWA

- **Kama ulibatizwa, ulibatizwa ukiwa mtoto au ukiwa mtu aliyekomaa? Kwa maneno mengine, Je, ulibatizwa ukiwa mtoto au mtu mzima?**

- ☐ NILIBATIZWA NIKIWA MTOTO
- ☐ NILIBATIZWA NIKIWA MTU MZIMA

- **Je, uliokolewa kabla ya ubatizo au baada ya ubatizo?**

- ☐ NILIOKOKA KABLA YA UBATIZO
- ☐ NILIOKOKA BAADA YA UBATIZO

- **Je, ulibatizwa kwa kusudi/dhumuni gani?**

Baada ya maswali hayo kujibiwa, hebu tuanze kutafuta ukweli kuhusu ubatizo. Kadiri tunavyojifunza Biblia, hebu ni-

Kuhusu Ubatizo

kutie moyo uufikirie kwa makini uhusiano wako na Mungu, kwa sababu kama bado hujaokolewa, katika eneo hili tunaangalia kipi unapaswa kufanya ili uweze kuokoka. Hata hivyo, kama unajisikia kwamba tayari umeshaokoka, hebu nikutie moyo ulinganishe majibu uliyoyatoa katika maswali sita hapo juu na taarifa zitakazopatikana katika somo hili ili uone kama kile ulichofundishwa kina uwiano na kinalingana na neno la Mungu.

Kumbuka, kama tulivyoona tena na tena, kweli ndiyo itakayokuweka huru (Yohana 8:32). Maagizo na mapokeo ya wanadamu hayawezi kukuweka huru; wala nia njema au tabia ya unyofu vyenyewe haviwezi kukuweka huru. Ni Yesu pekee na nguvu ya neno lake anayeweza kukuweka huru. Hivyo hebu twende katika kuutafuta ukweli ili tuone ni kitu gani tunachoweza kukigundua kuhusu ubatizo, na katika kufanya hivyo hebu tujibu maswali haya manne muhimu:

1. Je, ubatizo ni nini?
2. Je, dhumuni/lengo la ubatizo ni nini?
3. Je, ni nani anapaswa kubatizwa?
4. Je, wewe umebatizwa kulingana na maandiko?

Hebu tuanze na swali la kwanza: “Je, ubatizo ni nini?”

JE, UBATIZO NI NINI?

Ubatizo ni kutosi, ni neno ambalo lilitumika katika mazingira ya kawaida katika wakati wa Agano Jipya, na si tu katika mazingira ya kidini. Kwa mfano wakati meli ilipozama walisema “imebatizwa.” Maandiko yanazungumzia ubatizo zaidi ya mmoja, kama vile ubatizo wa Yohana, ubatizo wa moto na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hata hivyo kimsingi, tunapaswa kuyaelekeza mawazo yetu kwenye aina ya ubatizo ambao unatumika kwetu leo. Tunapoyaangalia maandiko, yatatueleza kitu fulani kuhusu asili ya ubatizo huo. Ni wazi kwamba ni kitu kinachofanyika majini. Biblia inanukuu vizuri sana watu “wakiingia majini” na “wakitoka majini.”

Kenneth Ratcliff
Mzee

Angalia kwa mfano, kile kilichotokea kwenye karne ile wakati mwinjilisti aliyeitwa Filipo alipomfundisha mtu kutoka Kushi/Ethiopia jinsi ya kufanyika kuwa mkristo. Habari hii imeandikwa katika kitabu cha Mdo. 8. Hapo tunajifunza kwamba Mkushi huyu alikuwa njiani akitokea Yerusalemu, akielekea Gaza. Alikuwa mekaa juu ya gari lake la kukokotwa na farasi, na alikuwa akisoma kutoka katika kitabu cha Agano la Kale cha Isaya. Ilikuwa ni katika wakati huu ambapo Filipo aliingia na kumsika akisoma kutoka katika kitabu cha Isaya 53, kuhusu mtumishi wa

Mungu ambaye angeteseka kwa niaba ya wenye dhambi. Ili hali akiendelea kujisomea kuhusu asili ya dhabihu ya mateso haya, Mkushi akamwambia Filipo: “Nakuomba, nabii huyu, asema; maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine?” (Mdo. 8:34). Angalia jinsi Filipo alivyojibu:

Filipo akafunua kinywa chake, naye, akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu (Mdo. 8:35).

Kutoka katika kifungu hiki, tunaona kwamba Filipo alimfundisha mkushi kuhusu Yesu. Kumfundisha mtu kuhusu Yesu kunahusisha kumfundisha kuhusu Uungu wa Bwana, nguvu zake, upendo wake, kifo, maziko na kufufuka kwake. Angalia mwitiko wa mafundisho kuhusu Yesu:

Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema, “Tazama, maji haya; ni nini kinachonizua nisibatizwe?” Filipo akasema, “ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana.” Akajibu, akanena, “Naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu.” Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza (Mdo. 8:36-38).

Katika tukio hili, tunajifunza kwamba ubatizo sio tu sehemu ya mafundisho kuhusu Yesu, bali pia tunajifunza kitu fulani kuhusu njia au jinsi ubatizo unavyofanywa. Katika tukio hili, iliwalazimu Filipo na Mkushi kuteremka wote wawili majini. Na ndipo walipokuwa kwenye maji, Filipo akambatiza Mkushi.

Hivyo basi, mtu anapotoswa majini, hutoswa/huzamishwa ndani ya maji na kufunikwa kabisa. Kwa hakika, mtu huzikwa – ambayo ni sawa kabisa na jinsi mtume Paulo alivyo-ouelezea ubatizo:

Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima (Warumi 6: 3-4).

Katika kukizungumzia kifungu hiki, Adam Clarke, msofi wa Biblia na mhubiri anayefahamika sana toka katika kanisa la Methodisti, anahitimisha pia kwamba ubatizo wa Agano Jipya ulifanywa kwa njia ya kutosi:

Kwa kugusia kitendo cha kutosi/kuzamisha katika suala la watu wazima, popote pale mtu anapozikwa ndani ya maji kama Kristo alivyozikwa ndani ya ardhi ya dunia, kufufuka kwake tena katika siku ya tatu, na kuibuka kwao kutoka majini ni kiashiria cha kufufuka kwa mwili. (Adam Clarke's Commentary on Colossians 2:12)

Sura ya 6

Angalia pia jinsi John Calvin, mwanzilishi wa kanisa la Presbyteriani alivyouelezea ubatizo:

Hata hivyo, neno hilo hilo “ubatizo” linaelezea kuza-misha, na kwa hakika kuzamisha huko kulifanywa na kanisa la zamani (Institutes, 3:343).

Leo, kuna makanisa mengi ambayo yananyunyiza au kumwagia maji na kitedo hicho hukiita ubatizo. Ili hali hakuna mahali popote katika Agano Jipya ambapo kitendo hiki cha kunyunyiza au kumwagia kinahusishwa na ubatizo.

Kumnyunyizia au kumwagia mtu maji kama aina ya ubatizo si sehemu ya ukristo wa kweli/halisi. Katika lugha ya Kiyunani, ambayo ndiyo lugha ambayo ilitumika kuan-dikia Agano Jipya, kulikkuwa na maneno yaliyotumika kwa kunyunyiza na kumwagia. Neno la kunyunyiza ni rhaino, kwa mfano neno hili lilitumika kwa ajili ya kunyunyiza damu. Neno kwa ajili kumwagia ni cheo. Ingawa maneno yote haya yalikuwepo wakati wa kuandikwa kwa Agano Jipya, hayakutumiwa kwa kuhusishwa na ubatizo. Badala yake neno lililotumika katika kwa kuhusishwa na ubatizo ni baptisma, ambalo lina mzizi wenye maana zamisha, tumbukiza au tosa.

**Rick Brumback
Mkufunzi wa Biblia na Mhudumu**

Unaweza ukajiuliza, kama watu wengine wanavyojiuliza, Je, kulikuwa na maji ya kutosha katika nchi ya Palestina


kwenye karne ya kwanza yaliyotosha kuwazamisha/kuwatosa idadi kubwa ya watu (kama ilivyoandikwa katika Mdo 2 na katika Yohana 3) waliobatizwa?

Kwanza kabisa, hebu niseme kwamba ubatizo hauhitaji kiwango kikubwa cha maji. Ubatizo wa kutosa umefanyika katika maeneo madogo sana, kama vile katika bafu(haya ni yale mabafu ya kisasa ambayo mtu anaweza kutumbukizwa na kuoga ndani yake) au visima.

Pili, ninaweza nikaongezea kwamba katika karne ya kwanza kulikuwepo na maji ya kutosha, katika mito na vijito vya Palestina pamoja na maeneno mengi ya kukusanyia maji yaliyotengenezwa na watu wa ulimwengu wa kale.

Tatu, kwa sababu ya msisitizo wa Wayahudi wa kujitakasa, mamia ya visima vya kubatizia (vilivyofahamika kama miqvehs) vilishajengwa ndani na maeneo yanayozunguka miji mikubwa na sehemu za kuabudia. Yerusalemu peke yake, Wanaakiolojia wamegudua takriban visima 150 viliyojengwa wakati wa Kristo.

Hivyo basi, katika kulijibu swali letu kuu la kwanza, “Je, ubatizo ni nini?” tunapaswa kuhitimisha kwamba ubatizo unaohitajika kwa wenye dhambi katika Agano Jipya ulifanywa kwa njia ya kutosa (kumzamisha mtu ndani ya maji). Haukufanywa kwa kunyunyiza au kumwagia.



Kuhusu Ubatizo

SEHEMU YA MARUDIO: JE, UBATIZO NI NINI?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Maji yanatumiwa na Mungu kama kitu muhimu sana na ishara ya _____ na usafi.
2. Kulingana na Mdo. 8:38, wakati Filipo alipombatiza towashi wa Kushi, yeye pamoja na towashi “_____ majini.”
3. Kulingana na Warumi 6:3-4, Je, ubatizo unaelezewa kama maziko? NDIYO/HAPANA.
4. Ni hakika kwamba kutosi (mfano. Ubatizo) kulikuwa ni tendo lililofanywa na kanisa la kwanza. NDIYO/HAPANA.
5. Neno la Kiyunani kwa ajili ya “kunyunyiza” ni rhaino. Je, neno hili limewahi kutumika mahali popote katika Agano Jipya likihusishwa na ubatizo? NDIYO/HAPANA.
6. Neno la Kiyunani kwa ajili ya “kumwagia” ni cheo. Je, neno hili limewahi kutumika mahali popote katika Agano Jipya likihusishwa na ubatizo? NDIYO/HAPANA.
7. Neno la Kiyunani baptismi lina mzizi wenye maana ya kuzamisha, kutumbukiza, au _____.
8. Kutokana na msisitizo wa Wayahudi wa kujitakasa, kulikuwa na mamia ya _____ (vili-vyofahamika kama miqvehs) vilishajengwa ndani na maeneo yanayozunguka miji mikubwa na maeneo ya kuabudia katika karne ya kwanza.

MAJIBU kwa ajili ya **MASWALI YA KUJIFUNZIA** yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Kama umebatizwa, Je, ulibatizwa ipasavyo, kulingana na kielelezo cha Agano Jipya? NDIYO/HAPANA
- B. Kama mtu “amebatizwa” kwa kunyunyuziwa au kumwagiwa maji, Je, mtu huyo amebatizwa ipasavyo, kulingana na Agano Jipya? NDIYO/HAPANA

MASUALA YA MAZUNGUMZO

- A. Jadili umuhimu wa ukweli kwamba ubatizo ni kuzamishwa kabisa kwa mwili kwenye maji, kulingana na maelezo ya Paulo katika Warumi 6:3-4.
- B. Kama mtu “amebatizwa” kwa kunyunyuziwa au kumwagiwa maji, na kama amefikia hatua ya kutambua kwamba ubatizo huo haukuwa wa kimaandiko, Je, anapaswa afanye nini?
- C. Je, John Calvin na Adam Clarke wanaamini nini kuhusu kielelezo cha ubatizo? Je, ni kwa nini mtazamo huu kuhusu kielelezo cha ubatizo umebadilishwa miongoni mwa madhehebu mbalimbali?



Sura ya 6

JE, DHUMUNI/LENGO LA UBATIZO NI NINI?

Hebu sasa tujibu swali, “Je, dhumuni la ubatizo ni nini?” Je, ni kwa nini wenye dhambi walibatizwa? Je, kulikuwa na kitu fulani cha kimazingara au maajabu kuhusu maji yaliyowaongoa wenye dhambi? Hebu tena tuangalie Biblia kama kiongozo wetu kwa ajili ya uhakika wa ukweli, na kadiri tunavyopekua kurasa zake, hebu tuangalie jinsi Mungu alivyotumia damu na maji kama njia ya utakaso na usafi wa kiroho kupitia vipindi vitatu tofauti vya nyakati na mipango ya kidini.

Vipindi hivyo vya wakati na mipango ya kidini vinafahamika kama kipindi cha Mababa (takriban miaka 4000 K.K), kipindi cha Musa (takriban miaka 1500 K.K), na kipindi cha Ukristo (takriban miaka 33 B.K). Katika kipindi cha Mababa, maji yalitumika kuisafisha dunia na kumuokoa Nuhu na familia yake ili wasiangamie. Mafuriko hayo ya maji yamezungumziwa na Petro kama ishara ya ubatizo katika zama za Ukristo.

Watu wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji. Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo (1 Petro 3:20-21).

Pia katika kipindi cha Mababa, damu ya wanyama ilitumika

kama ishara/alama ya kuhesabiwa haki na kuwa na agano, kama vile ilivyo katika suala la Habili, Nuhu na Ibrahim.

Wakati wa kipindi cha Musa, Mungu aliitumia damu kama ishara ya usafi na ukombozi - kama ilivyo katika hadithi ya Kutoka wakati Mungu alipowaokoa wazaliwa wa kwanza wa taifa la Israeli wasife kwa kuruka milango ya wale waliopaka damu katika miimo ya milango yao (Kutoka 12). Katika kitabu cha Walawi matumizi ya damu yanatiliwa mkazo sana, kinaonesha jinsi damu ilivyokuwa ikinyunyizwa madhabahuni, kwa kuhani na mara kadhaa kwa watu.

Kwa kuongezea, maji yalitumika kama ishara ya utakaso na usafi wakati wa kipindi cha Musa. Yalitumika kwa lengo la kumtakasa kuhani ambaye alipaswa kuingia hekaluni au hemani ili kutoa huduma (Walawi 8:6). Maji yalitumika pia kuwatakaswa wakoma ambao walikuwa wakitafuta tiba katika kambi ya Waisraeli. Matumizi ya hivi vitu viwili katika kila moja ya mifumo hii vilitumika kama vitu muhimu na vya msingi kwa matumizi yao katika kipindi cha Agano Jipya.

Katika kipindi cha Ukristo, Yesu alimwaga damu yake ya thamani kwa lengo la kutakasa na kusafisha. Alipigwa. Alidhihakiwa. Halafu akasulubiwa kwenye msalaba wa Kalvari. Ilikuwa ni pale msalabani ambapo alimwaga damu yake. Damu yake ilikuwa ni safi na isiyo na hatia, ilitolewa kama malipo ya kulipia uhuru wetu ili tutoke katika utumwa wa dhambi.

Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mliou-

Vipindi vya Kidini

Mababa
(Takriban) 4000 K.K



Musa
(Takriban) 1500 K.K



Ukristo
(Takriban) 33 B.K



Isaka

Wayahudi chini ya Sheria ya Musa

Leo

Ishmaeli

Mataifa bado wapo chini ya Sheria ya Mababa

Kuhusu Ubatizo

pokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo (1 Petro 1:18-19).

Siyo tu kwamba damu ya Yesu inakomboa, bali pia humhesabia mtu haki:

Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu; ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake, ili aonyeshe haki yake, kwa sababu ya kuziachilia katika ustahimili wa Mungu dhambi zote zilizotangulia kufanywa; apate kuonyesha haki yake wakati huu, ili awe mwenye haki na mwenye kumhesabu haki yeye amwaminiye Yesu (Warumi 3:23-26).

Neno “kuhesabiwa haki” kwa hakika ni neno la muhimu sana, na linaonesha kwa ujumla ni kwa kiasi gani Mungu huwapenda watu wote kila mahali. Neno “kuhesabiwa haki” katika lugha ya asili ilikuwa linabeba dhana ya “kutokuwa na hatia” au “kuachiliwa huru.” Hivyo basi, kunawakati fulani – tunapokutana na damu ya Kristo – wakati Mungu atakaposema kwamba mwanadamu hana hatia ya dhambi tena. “Amehesabiwa haki.”

**Norman Starling
Mwinjilisti**

Ama kwa hakika, damu ya Yesu huokoa. Lakini kama vile Mungu katika Agano la Kale alivyotumia damu na maji katika kutakasa na kusafisha, Hivyo ndivyo anavyovitumia leo pia, chini ya Agano Jipya damu na maji hutumika kumhesabia haki mwenye dhambi.

Ili kuelewa vizuri uhusiano huu kati ya maji na damu, hebu tugeuzie akili zetu katika kitabu cha Warumi, ambapo Roho Mtakatifu alifunua jinsi damu ya Yesu na maji ya ubatizo vinavyofanya kazi pamoja ili kuleta wokovu. Katika Warumi 1, Mtume Paulo anawakumbusha wasomaji wake kwamba Injili – ujumbe unaopatikana katika Biblia ni nguvu ya Mungu iletayo wokovu. Katika sura ya 2 na 3, anawakumbusha kwamba “wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu” (Warumi 3:23).

Neno “wote” katika kifungu hiki kinazungumzia matabaka yote ya watu na mataifa yote. Tunaendelea kujifunza katika sura hii, na sura ya 5, kwamba watu wote hawa wanaweza kuhesabiwa haki na kuokolewa kutoka katika ghadhabu ya Mungu kwa kupitia damu ya Kristo. Lakini tunapofika katika sura ya 6, tunajifunza jinsi wenye dhambi wanavyo-okolewa, na jinsi mkristo anavyopaswa kuishi maisha baada ya kuokolewa.

Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki (Warumi 6:17-18).

Hapa tunaona kwamba wale waliokuwa watumwa wa dhambi wamefanyika kuwa watumwa wa haki. Ni nini kimeleta utofauti hii? Je, ni kitu gani kilichowafanya wawe huru kutoka katika dhambi? Je, ni kwa jinsi gani waliweza kukutana na damu isafishayo ya Kristo? Kwa maneno mengine, Je, ni kitu gani walichokifanya kikasababisha wawe wakristo?

Kwanza kabisa, hebu tuangalie kwamba walikuwa watiifu. “Hawakuamini” tu jina la Yesu ili waweze kuwekwa huru kutoka katika dhambi zao zilizopita, kwa sababu imani pekee haiwezi kuokoa. Imani ya kweli iokoayo huhusisha matendo. Inahusisha kufanya mapenzi ya Mungu.

Wewe waamini yakuwa Mungu ni mmoja; wataenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka! Lakini wajua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai?..... Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani pekee yake. (Yakobo 2:19-20,24)

Angalia kile Yakobo alichosema. Anaanza kwa kusema kwamba mwanadamu huhesabiwa haki kwa matendo, na si kwa imani pekee yake. Yesu pia anathibitisha umuhimu wa utii.

Si kila mtu aniambiaye, “Bwana, Bwana”, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni (Mathayo 7:21).

Kumuita tu Bwana, au kujivunia kile tulichokifanya kwa jina la Kristo havitoshi. Yesu alisema ni lazima tuyafanye mapenzi ya Baba. Wakati matendo na amri za wanadamu haziwezi kuwaokoa, matendo ya Mungu yanaweza kuwaokoa!

Maana kila mtu atendaye mabaya huichukia nuru, wala haji kwenye nuru, matendo yake yasije yasije yakakemewa. Bali yeye aitendaye kweli huja kwenye nuru, ili matendo yake yaonekane wazi ya kuwa yametendwa katika Mungu (Yohana 3:20-21).

Tunapofanya yale yanayosemwa na kweli, tunakuja nuruni. Kuutii ukweli kunadhihirisha kwamba Mungu anawaokoa wenye dhambi. Hakuna hata mmoja wetu awezaye – kwa nafsi zetu wenyewe, au ndani ya nafsi zetu – kujiokoa wenyewe. Lakini tunapoutii ukweli, husababisha wenye dhambi kuokolewa na Mungu. Tena katika Warumi 6 tunaona kwamba hawa wenye dhambi walioko Rumi waliwekwa huru kutoka katika dhambi zao baada ya kuwa watiifu.

Sura ya 6

Sasa, hebu tuangalie ni kitu gani walichokitii. Je, walifanya nini ili wawe huru kutoka katika dhambi zao? Msikilize tena mtume Paulo:

Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mlitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake (Warumi 6:17).

Je, waliadini nini? Waliadini namna ya elimu ambayo walipewa. Lakini, Je, hayo mafundisho yalikuwa ni yapi? Je, walikuwa wamefundishwa nini? Paulo anatuambia:

Basi, ndugu zangu, nawaarifu ile injili niliyowahubiria; ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mnasimama, na kwa hiyo mnaokolewa; ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiri isipokuwa mliadini bure. Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko (1 Wakorintho 15:1-4).

Kama katika Warumi 6, hapa katika 1 Wakorintho 15 Paulo anazungumzia kitu fulani kilichotolewa (au kukabidhiwa) kwa wakristo. Je, ni kitu gani hicho? Ili kuwa ni mahubiri yake kuhusu kifo, maziko na ufufuko wa Kristo. Ukweli huu wa aina tatu ndiyo msingi wa kuelewa Injili ya Yesu. Ni vya muhimu katika kuhakikisha wokovu wa mwenye dhambi.

Ujumbe wa kifo, maziko na ufufuko ulikuwa ni msingi wa kile ambacho Paulo na wengine walichokihubiri kwenye karne ya kwanza. Kuhusu kifo cha Kristo, walizungumzia kupigwa kwake na kusulubishwa vibaya. Pia walisisitiza kuhusu damu ambayo aliimwaga.

Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa



ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye (Warumi 5:8-9).

Sheria inasema tulipaswa kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Lakini Yesu alisema, "Nitachukua nafasi ya mwanadamu mwenye dhambi." Alikidhi haki ya Mungu kwa mwanadamu ili kwamba watu wote ambao kwa imani, wataifikia damu ya Yesu na kuhesabiwa haki – na kutangazwa kuwa "hawana hatia" na "huru kutoka katika dhambi."

**Norman Starling
Mwinjilisti**

Sio tu kwamba ujumbe wa Injili unahusisha habari njema kuhusu kifo na damu ya Yesu, bali pia inahusisha maelezo ya kina kuhusu mazishi yake. Inazungumzia jinsi Yusufu wa Arimathaya na Nikodemu walivyouchukua mwili wa Yesu kutoka msalabani na kuuandaa kwa ajili ya maziko. Inazungumzia jinsi walivyoweka mwili wa Bwana kwenye kaburi, na jinsi mwili wa Bwana wetu ulivyolala pale kaburini mpaka siku ya Jumapili asubuhi alipofufuliwa kwa nguvu za Mungu. Kufufuka kwake kunamaanisha kwamba amekishinda kifo, na kwamba kwa hakika yeye ndiye Masihi. Injili inafunua jinsi Kristo alivyomshinda Shetani, dhambi na kaburi. Kwa njia ya mshindi huyu, Yesu aliliziba pengo lililokuwepo kati ya wenye Mungu na wenye dhambi kwa kujenga daraja.

Kulingana na Isaya 59:1-2, dhambi ndiyo inamtenga mtu na Mungu. Lakini kwa kupitia njia ya kifo, maziko na ufufuo wa Kristo, wenye dhambi sasa wanatumaini la kuvuka daraja na kuunganishwa tena na Mungu. Hata hivyo, wenye dhambi wanapotii namna ya mafundisho yanayopatikana katika Biblia – hiyo ndiyo kifo, maziko na ufufuo wa Kristo – Je, hiyo inamaanisha kwamba mwenye dhambi anapaswa kufa kihalisia, kuzikwa kihalisia, na kufufuka kihalisia ili awe mtiifu? Soma Warumi 6:17 kwa mara nyingine ili ujifunze hasa kile ambacho wenye dhambi wanachopaswa kukitii:



Injili yafanywa kuwa Sheria

1 Wakorintho 15:3-4

Yesu Kristo

Kifo, Maziko na Ufufuo wake
Kwa ajili ya Dhambi za Mwanadamu



Kifo



Maziko



Ufufuo

Injili yafanywa kuwa Sheria Tena

Katika Ubatizo

(Kuitii Injili—Warumi 6:3-4)

Katika Ubatizo

Tunazitubia na kuzifia dhambi

Tunazikwa katika maji kwa ajili ya Ondoleo la dhambi

Tunafufuliwa ili kuenenda katika Upya wa Uzima



Kuzifia
Dhambi



Kufufuliwa ili
kuenenda katika
Upya wa Uzima



Kuzikwa Katika Maji

Kuhusu Ubatizo



Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake (Warumi 6:17).

Kile walichokitii hakikuwa mafundisho (au mafunzo) kuhusu kifo, maziko na ufufuo wa Yesu, lakini kilikuwa ni namna (au kielelezo) cha mafundisho hayo. Walitii kitu fulani kinachofanana na hayo mafundisho. Je, kilikuwa ni kitu gani, na Je, kilihusisha maji? Soma kile Paulo alichokisema kuhusiana na jambo hili:

Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake (Warumi 6:3-5).

Ni hapa, katika kifungu hiki ambapo tunajifunza jinsi kuhesabiwa haki na msamaha vinavyopatikana, na jinsi kifo cha Kristo na damu yake vinavyounganishwa na maji ya ubatizo. Katika Warumi 6, tunajifunza jinsi wenye dhambi waliopo katika mji wa Rumi walivyofanyika kuwa Wakristo, kwa maana kama Kristo alivyokufa msalabani, hawa wakristo walichagua kuufia utu wao wa kale wa dhambi kwa kumkiri Yesu kuwa ndiye Bwana. Kama vile Yesu alivyozikwa katika kaburi, ndivyo hawa wenye dhambi walivyozikwa katika kaburi la maji ya ubatizo. Na kama vile Yesu alivyofufuliwa kwa nguvu za Mungu kuwa na maisha mapya, hawa wenye dhambi walitoka katika ubatizo kwa nguvu hizo hizo ili waenende katika upya wa uzima. Kabla ya ubatizo wao, walikuwa wamekufa kiroho, lakini baada ya ubatizo, walihuishwa katika Kristo; walikuwa katika hali ya ufufuo. Hivyo basi, ubatizo ni kwa ajili ya wale

waliokufa katika dhambi. Ili kufufuliwa kiroho na kuhuishwa katika Kristo, mwenye dhambi anapaswa kuunganishwa na Kristo katika ubatizo. Damu ya Yesu na maji ya ubatizo hutwa pamoja katika njia nzuri na iokoayo maisha. Kwa sababu ya hili, haipaswi kuwa kitu cha kushangaza kusikia kile Yesu alichomweleza huyu mtu aliyeitwa Nikodemu ambaye alikuwa ni Myahudi anayeamini.

Yesu akajibu, akamwambia, "Amin, amin na kuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu ...Nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuona ufalme wa Mungu" (Yohana 3:3,5).

Kuzaliwa mara ya pili, na kwa njia hiyo kufanyika kuwa mwana wa Mungu, kunahitaji mtu azaliwe kwa maji; hiyo ni kusema, ni lazima abatizwe. Kulingana na Warumi 6:17-18, ili kuwa huru kutoka katika dhambi – na kwa kupitia hilo kufanyika kuwa mtumwa wa haki – mtu anapaswa kuwa mtiifu katika ubatizo kwa namna ya mafundisho ambayo yanafuatisha/yanaakisi kifo, maziko na ufufuo wa Kristo. Katika Warumi 1:16, tunajifunza kwamba Injili ndiyo nguvu ya Mungu iletayo wokovu. Katika Warumi 6:17, tunajifunza kwamba namna ya Injili hiyo mtu anaweza kuitii. Kutokana na hilo kuwa ni la kweli, mimi na wewe tunapaswa kuelewa uzito wa maelezo yafuatayo:

Na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu (2 Wathesalonike 1:7-8).

Tunapaswa kuitii Injili! Mwenye dhambi hawezi kujio-koa mwenyewe au yeye mwenyewe kusulubiwa kihalisia, na kuzikwa kihalisia, na kufufuka kihalisia kutoka katika kaburi. Lakini kama tulivyoona, mwenye dhambi anaweza akafanya kitu kinachofanana na hiki. Mwenye dhambi anaweza akazikwa pamoja na Kristo kwa njia ya ubatizo kwa ajili ya ondoleo la dhambi (Mdo 2:38), na kufufuka ili kuenenda katika upya wa uzima (Wakolosai 2:12).

Katika hatua hii unaweza ukauliza, "Je, maji pekee yanaweza kuokoa?" Je, kuna kitu cha ajabu au cha kimazingara kuhusu maji – hasa maji yaliyopo kwenye kisima cha kubatizia? Hapana, hakuna kitu chochote kwenye Biblia kina-choongelea kwamba maji pekee yanaweza kuiokoa roho kutoka katika mauti. Hakuna mahali popote katika Biblia inapozungumzia kwamba maji pekee yanaweza kuokoa, lakini pia haifundishwa kwamba imani pekee inaweza kuokoa. Ni neema ya Mungu inayomwokoia mtu. Lakini pia ni neno la Mungu, kweli, ambalo linatueleza ni wakati gani mtu anaokolewa, na ni katika hatua gani mtu huyo anakuwa katika uhusiano sahihi na Mungu.

Njia pekee ya kujua kama ubatizo ni wa muhimu kwa ajili ya wakovu ni kwa kuangalia matukio yaliyoan-

Sura ya 6

dikwa katika Biblia. Kifungu cha 1 Petro 3:21 kinatuambia kwamba ubatizo hufanya kitu fulani. Je hufanya kitu gani? Petro anasema, “Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowakoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo.” Ubatizo si kuoga ambako huondoa uchafu wetu, lakini hutupa sisi dhamiri safi, Pamoja na kutuondoa dhambi zetu (Mdo 2:38) na huosha dhambi zetu (Ufunuo 1:5). Lakini, Je, ni wakati gani tunapokutana na damu hiyo? Ni pale kama watu tuliotubu, waumini tunaokiri, tunapobatizwa.

B.J. Clarke
Mtumishi

Hii kanuni ya kuoshwa na Mungu tunapofanya kama alivyo-tuagiza inaweza pia ikaonekana katika Agano la Kale katika habari ya jemedari wa jeshi la Shamu, Naamani, ambaye alikuwa akitafuta kutakaswa ukoma wake. Kulingana na 2 Wafalme 5:1-14, Naamani, akijaribu kuiondoa nafsi yake katika ugonjwa huu mbaya, alimwendea nabii Elisha, akitarajia kupokea masharti makubwa. Badala yake Elisha alimwambia Naamani ajitose mara saba katika mto Yordani. Mwanzoni Naamani alilipinga wazo hili kwamba mto Yordani unaweza ukamtakasa. Na ni kweli maji ya mto Yordani pekee yake yasingeweza kuutakasa ukoma wa mtu – iwe wakati ule au sasa. Lakini maji hayo yalipounganishwa na utii wa amri ya Mungu, jemedari wa Shamu ghafla akafanywa kuwa mpya. Ndipo pale na ni pale tu, ukoma wake ukatakaswa.

Leo, hakuna kiwango chochote cha maji pekee kinachoweza kuiokoa roho kutoka katika ukoma wa dhambi. Lakini ubatizo unapounganishwa na tumaini, imani yenye utii, ndipo Mungu anasema unaweza kuokolewa kwa damu ya Kristo. Kwa hakika ni suala la kutumaini katika kile Mungu alichosema kifanywe, Mungu anaposema fanya, na jinsi Mungu anavyotaka kifanyike, na kwa mtu Mungu aliyemwambia afanye.

Hivyo, katika kulijibu swali letu kuhusu dhumuni la ubatizo, tumejifunza kwamba ubatizo ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na pia ni njia ya mtu kumfanya mtu kuwa mtumwa wa haki, mwana wa Mungu na mkristo.

Ili mtu aokolewe na kupata nyumba ya milele mbinguni, ni lazima awe mshiriki wa mwili wa Kristo. Paulo anasema katika Waefeso 1:3 kwamba baraka zote za rohoni zinapatikana “katika Kristo.” Moja kati ya hizo Baraka za rohoni ni wokovu (2 Timotheo 2:10). Ili mtu apate wokovu – ambao upo “katika Kristo” – anapaswa kuingia katika Kristo. Paulo alisema katika 1 Wakorintho 12:13, “Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja.”

Alfred Washington
Mtumishi

Ubatizo humuingiza mwenye dhambi katika mwili wa Kristo (huku ni kusema, kanisa la Kristo), na ni njia ambayo kwayo mwenye dhambi anamvaa Kristo. Ni hatua katika mchakato wa uongofu ambapo mwenye dhambi anaweza akajiita mkristo. Basi ubatizo, una dhumuni la pekee na la muhimu ambalo tunapaswa kulielewa kikamilifu.

SEHEMU YA MARUDIO: JE, DHUMUNI LA UBATIZO NI NINI?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Katika kipindi cha mababa, _____ ilitumika kuisafisha dunia na Nuhu pamoja na familia yake walio-kolewa na maangamizi.
2. Kulingana na 1 Petro 3:20-21, mtume Petro anataja gharika ya kipindi cha Nuhu ambayo iliisafisha dunia na kusema yafuatayo: “.... Siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani watu wanane _____ kwa maji. Mfano wa mambo hayo ni _____ unaowaokoa ninyi pia siku hizi.
3. Katika kipindi cha Musa _____ ya wanyama ilitumiwa kama ishara ya utakaso na ukombozi.
4. Katika kipindi cha Musa, _____ ilitumika kama ishara ya utakaso kwa vitu kama kutakaswa kwa makuhani ambao walikuja kutumika katika hekalu, na katika kuwatakasa wakoma.

Kuhusu Ubatizo

5. Kulingana na 1 Petro 1:18-19 na Warumi 3:23-26, katika kipindi cha Ukristo, Yesu alimwaga _____ ya thamani kwa lengo la kutakasa na kusafisha.
6. Kulingana na Warumi 3:23-26, wenye dhambi _____ bure kwa neema yake kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu, ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa damu yake.”
7. Neno “kuheshabiwa haki” kama lilivyotumika katika Agano Jipya, lina maana ya “_____” au “kuachiliwa”
8. Kama vile Mungu katika Agano la Kale alivyotumia damu na maji katika kutakasa na kusafisha, Vivyo hivyo leo katika Agano Jipya anatumia _____ na _____ wenye dhambi.
9. Kulingana na Yakobo 2:24, Watu hawawezi kuokolewa kwa “_____.”
10. Kulingana na Mathayo 7:21, Yesu alisema, “Si kila mtu aniambiaye ‘Bwana, Bwana’ atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yeye _____ mapenzi ya Baba yangu aliyembinguni.”
11. Kulingana na Warumi 6:17-18, Biblia inafundisha: “Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini _____ kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki.”
12. Kulingana na mstari hapo chini, Je, nguvu ya Mungu iletayo wokovu ni ipi? _____

Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia (Warumi 1:16).

13. Kulingana na 1 Wakorintho 15: 1-4, Je, Injili iliyohubiriwa na Paulo na kutolewa kwa Wakorintho ilijumuisha mahubiri kuhusu kifo, maziko na ufufuo wa Kristo? NDIYO/HAPANA
14. Kulingana na 2 Wathesalonike 1:7-8, Bwana Yesu na malaika wake wakuu watawalipa kisasi wao wasiomjua _____, na wao _____.
15. Kulingana na Warumi 6:17 na 1 Wakorintho 15:1-4, Je, wenye dhambi wanapaswa kufa kihalisia, kuzikwa kihalisia na kufufuka kihalisia ili waitii Injili? NDIYO/HAPANA
16. Kulingana na Warumi 6:3, wenye dhambi wanoataka kuokolewa wanapaswa _____ katika kifo cha Kristo.
17. Kulingana na mstari hapo chini, ubatizo ni kwa ajili ya _____ la dhambi.
Petro akawaambia, “Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.”(Mdo. 2:38).
18. Kulingana na Yohana 3:3,5 Yesu alimwambia Nikodemu kwamba ili mtu aweze kuingia katika ufalme wa Mungu anapaswa “azaliwe kwa _____ na kwa Roho.”
19. Kulingana na mstari hapo chini, _____ huosha dhambi.

Sura ya 6

Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake (Mdo. 22:16).

20. Katika 1 Petro 3:21, Petro anauzungumzia ubatizo kama “ndio ambao _____ sisi.”
21. Kulingana na mistari hapo chini, Je, baraka zote za rohoni (pamoja na wokovu) zinapatikana katika Kristo? NDIYO/HAPANA

Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za Rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo (Waefeso 1:3).

Kwa ajili ya hilo nastahimili mambo yote, kwa ajili ya wateule, ili wao nao waupate wokovu ule ulio katika Kristo Yesu, pamoja na utukufu wa milele (2 Timotheo 2:10).

22. Kulingana na mstari hapo chini, mwenye dhambi huingia kwa Kristo kwa _____ katika Kristo.
- Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo (Wagalatia 3:27).*
23. Kulingana na 1 Wakorintho 12:13, Ubatizo humweka mwenye dhambi katika _____ wa Kristo (Hii ni kusema, kanisa la Kristo).

MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Je, umeshabatizwa kwa kuzamishwa majini ili dhambi zako zisamehewe? NDIYO/HAPANA
- B. Kama ulifundishwa kwamba uliokoka kabla ya ubatizo, Je, ungelibatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi (kuokolewa)? NDIYO/HAPANA
- C. Kama hukubatzwa katika njia ambayo Mungu ameagiza (kwa kutoswa majini) na kwa sababu sahihi (kwa ajili ya ondoleo la dhambi), Je, inawezekana wewe ukawa umekosea? NDIYO/HAPANA.
- D. Je, unataka kwenda mbinguni? NDIYO/HAPANA
- E. Je, uko tayari kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi katika mwili wa Kristo? NDIYO/HAPANA

MASUALA YA MAZUNGUMZO

- A. Kulingana na Warumi 6:3-5 na mistari hapo chini, Je, mwenye dhambi anakutanaje na damu ya Yesu iokoayo?
- Tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye sisi na kutuosha dhambi zetu katika damu yake (Ufunuo 1:5).*
- B. Kulingana na Yohana 3:3,5 ubatizo humweka mwenye dhambi katika “kitu fulani” Je, kitu hicho ni kipi?
- C. Je, ni kwa jinsi gani ukweli wa kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu huungana na kuunda msingi wa kugeuzwa kwa mwenye dhambi na kufanywa kuwa mkristo? Kwa maneno mengine, Je, kuna uhusiano gani kati ya kifo, maziko na ufufuo wa Kristo na amri inayowataka wenye dhambi kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi?



Kuhusu Ubatizo

JE, NI NANI ANAYEPASWA KUBATIZWA

Je, ni nani anayepaswa kubatizwa? Kwa maneno mengine, Je, mtu anahitaji kujua nini au afanye nini kabla ya ubatizo? Na ni vipi kuhusu watoto? Je, wanapaswa kubatizwa? Katika kuyajibu maswali haya, hebu tuanze kwa kusikiliza maneno ya Yesu:

Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu (Mathayo 28:19).

...Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka ... (Marko 16:15-16).

Kutoka katika maelezo haya yote, tunajifunza kwamba kitu fulani cha muhimu sana ni lazima kitokee kabla mtu haja batizwa kulingana na maandiko. Je, hicho “kitu fulani” ni kipi”? Rahisi sana, ni kuhubiri na kuamini. Ili mtu amwendee Mungu imempasa kwanza kusikia (au kufundishwa) neno la Mungu.

Imeandikwa katika manabii, na wote watakuwa wamefundishwa na Mungu. Basi kila aliyesikia na kujifunza kwa Baba huja kwangu (Yohana 6:45).



Kwa kuongezea katika kufundishwa, mtu anayetaka kubatizwa ni lazima aamini kile kinachofundishwa. Wakati Yesu aliposema, “Aaminiye na kubatizwa ataokoka,” ni lazima tujiulize, “Je, mtu anapaswa kuamini nini hasa?” Angalia tena Yesu alisema kwamba, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili. Aaminiye (huko ni kusema, aaminiye Injili) na kubatizwa ataokoka.” Wale wanaotamani kubatizwa ni lazima waiamini Injili.

Kuiamini Injili kunahitaji sisi tuamini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu na Mwokozi wa ulimwengu.

Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele (Yohana 3:16).

Kumwamini Yesu huja tunapolisikia neno la Mungu:

...imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo (Warumi 10:17).

Lakini hebu tuangalie kwamba kuiamini Injili kunatuhitaji sisi kuamini kile Yesu alichofundisha katika Agano lake Jipya. Hili Agano (au makubaliano) yanaonesha kwamba kabla mtu hajamwendea Mungu katika ubatizo, ni lazima atubu:

...Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu (Mdo. 2:38).

Toba si tu kujisikia huzuni kuhusu dhambi. Lakini badala yake, Biblia inatufundisha kwa huzuni ya namna ya Mungu huleta toba:

Sasa nafurahi, si kwa sababu ya ninyi kuhuzunishwa, bali kwa sababu mlihuzunishwa, hata mkatubu. Maana mlihuzunishwa kwa jinsi ya Mungu, ili msipate hasara kwa tendo letu katika neno lolote. Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti (2 Wakorintho 7:9-10).

Sasa je, ubatizo ni nini? Kutubu maana yake ni kubadilika – kutoka katika kuishi katika maisha ya dhambi na kuishi maisha ya haki. Toba pia inahitaji sisi tuache kuishi kulingana na mapenzi yetu na kuanza kuishi maisha ambayo yanafuata hatua za Yesu:

...mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuata (Luka 9:23).

Je, ni nani anayepaswa kubatizwa? Ni mtu yule ambaye ameiamini Injili na kuzitubia dhambi zake.

Sura ya 6

Lakini bado analakufanya zaidi, wale ambao wanapaswa kubatizwa ni wale ambao wamekiri.

Basi kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni (Mathayo 10:32).

Hebu sasa tuunganishe haya yote pamoja: Ubatizo ni lazima utanguliwe na mafundisho – halafu imani, toba na ukiri. Je, ni nani anayepaswa kubatizwa? Ni mwenye dhambi aliye nje ya Kristo, aliyefundishwa, aliyeamini, aliyetubu na aliyekiri.

Lakini sasa, Je, tunapaswa kufanya nini kuhusu kuwabatiza watoto? Je, ni sahihi au ni lazima kumbatiza mtoto? Jiulize wewe mwenyewe, “Je, mtoto anaweza akaamini, akatubu au akakiri?” Hapana. Tunajua kwamba mtoto hana uwezo wa kiakili wa kufanya haya mambo. Hivyo basi, mtoto hawezi kuitii amri ya Mungu ya kubatizwa.

Si lazima kumbatiza mtoto, wala si suala la kimaandiko. Ubatizo ni kwa wale wenye uwezo wa kusikia neno la Mungu, kulelewa, kuliadini na kutokana na uelewa huo, kulitii. Yesu alisema, “Aminiye na kubatizwa ataokoka” (Marko 16:16). Kwa kuongezea, watoto hawajapotea. Wako “salama,” kama Yesu alivyosema katika Mathayo 18:3, “Amin, nawaambia, Msipoongoka na kuwa kama

vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.” Tunapaswa kuwa na sifa za watoto wadogo, ambao wapo kwenye ufalme wa Mungu. Watoto hawajapotea, na wala hawahitaji kubatizwa. Hawalielewi hili. Ubatizo ni kwa ajili ya wale waliokomaa na wenye kujua mema na mabaya na walio na uwezo wa kutenda jambo kulingana na uchaguzi wao.

Bobby Liddell
Mkufunzi wa Biblia na Mtumishi

Sababu pekee ambayo inaweza kumfanya mtoto abatizwe ni kama mtoto atakuwa na dhambi ambayo inahitajika kuondolewa. Lakini kulingana na Ezekieli 18:20, “Mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe.” Kumbukumbu la Torati 24:16 lina weka kanuni kwamba kila mtu anapaswa kuuawa kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe. Mtoto hawawahi kuivunja sheria ya Mungu (I Yohana 3:4). Hivyo, mtoto hahitaji kubatizwa kwa sababu hajatenda dhambi, na hana sifa za kubatizwa kwa sababu hajaamini.

B.J Clarke
Mtumishi

Dhambi ni kitu kinachofanywa, na si kitu kinachorithiwa. Hivyo basi watoto na vijana wadogo hawahitaji kubatizwa.

SEHEMU YA MARUDIO: JE, NI NANI ANAYEPASWA KUBATIZWA?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na Marko 16:16, mtu anapaswa _____ na _____ ili aokoke.
2. Kulingana na Yohana 6:45, Je, ni lazima mtu asikie na kujifunza kabla hajamwendea Baba? NDIYO/HAPANA
3. Kulingana na Yohana 3:16, Ili mtu awe na uzima wa milele anapaswa aamini (awe na imani) kwamba Yesu ni _____ wa pekee (wa Mungu).
4. Kulingana na Warumi 10:17, imani chanzo chake ni _____ neno la Mungu.
5. Kulingana na Mdo. 2:38, mwenye dhambi anapaswa _____ dhambi zake ili apate wokovu.
6. Kulingana na 2 Wakorintho 7:9-10, Je, toba ni “kujisikia tu huzuni” kwa ajili ya dhambi zetu? NDIYO/HAPANA
7. Kutubu maana yake ni kubadilika kutoka katika maisha ya _____ na kuishi maisha ya haki.

Kuhusu Ubatizo

8. Kulingana na Mathayo 10:32, Ili mwenye dhambi apate kuokolewa anapaswa _____.
9. Kulingana na Mdo. 2:38 na mstari hapo chini, Je, Biblia inafundisha kwamba ili mwenye dhambi aokolewe ni lazima abatizwe? NDIYO/HAPANA

Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake (Mdo. 22:16).

Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo (I Petro 3:21).

10. Kulingana na mstari hapo chini, Je, dhambi inaweza kurithiwa, au Je, mtu anazaliwa katika dhambi? NDIYO/HAPANA

Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa; mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe, haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake. (Ezekieli 18:20).

11. Je, mtoto au kichanga kinaweza kumwamini Kristo kama Mwana wa Mungu, kikatubia dhambi zake zilizopita na kikakiri jina la Kristo? NDIYO/HAPANA.

12. Kulingana na mafundisho ya Agano Jipya, Je, ni suala la kimaandiko kuwabatiza watoto au vichanga? NDIYO/HAPANA

MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MASUALA YA MAAMUZI

- A. Kama “ulibatizwa” wakati ukiwa mtoto, Je, huo ni “ubatizo” kulingana na maandiko? NDIYO/HAPANA
- B. Kama “ulibatizwa” wakati ukiwa mtoto, Je, unapaswa kufanya nini kuhusiana na suala hilo?
- C. Je, wenye dhambi (ambao bado hawajabatizwa) wanapaswa wabatizwe? NDIYO/HAPANA
- D. Je, wewe ni mwenye dhambi? NDIYO/HAPANA
- E. Je, unaamini kwamba damu ya Yesu inaweza kukuokoa? NDIYO/HAPANA

MASUALA YA MAZUNGUMZO

- A. Sababu pekee itakayomsababisha mtoto au kichanga kihitaji ubatizo ni kama mtoto huyo ana dhambi ambazo zingehitajika kusamehewa. Kulingana na Biblia, Je, watoto hutenda “dhambi?” Ni kwa nini ndiyo au hapana?
- B. Je, kulingana na maandiko, watoto ni wahusika sahihi wa ubatizo? Ni kwa nini ndiyo au hapana?



Sura ya 6

JE, WEWE UMESHABATIZWA KULINGANA NA MAANDIKO?

Sasa, hebu tuliangalie swali letu kuu. Tunapofanya hivyo, hebu tulifanye liwe swali binafsi kwa kukuzungumzia wewe, Mungu na ubatizo: “Je, wewe umeshabatizwa kulingana na maandiko?”

Kuamua ama ubatizwe au la ni uamuzi wa muhimu sana. Kwa hakika ni uamuzi wa muhimu sana mtu anaoweza kufanya. Kama hujawahi kubatizwa, basi kulingana na Biblia wewe bado upo katika dhambi zako, kwa sababu faida ya damu ya Bwana iokoayo hutolewa tu katika njia ya Mungu aliyoipanga ya ubatizo. Basi, kama hujawahi kubatizwa kulingana na Biblia wewe bado hujaokolewa, nawe haupo katika ufalme wa Mungu:

Yesu akajibu, “Amin, amini, nawaambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu” (Yohana 3:5).


...Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aminiye na kubatizwa atao-koka (Marko 16:15-16).

Mwanzoni mwa somo hili, uliombwa kujibu maswali kadhaa, la kwanza ambalo lilikuwa linauliza, Je, wewe umeokolewa au la. Je, umeokolewa? Je, upo katika uhusiano sahihi na Mungu? Je, umeshawahi kufanya vitu ambavyo ulitambua kuwa si sahihi? Je, ulemewa na hatia? Je, dhambi imekuwa ni mzigo ambao hauwezi kuendelea kuvumilia kabisa?

Je, wewe kwa hakika ni mwenye dhambi aliyepotea na kutengwa na Mungu? Au, Je, kuna uwezekano wa wewe kutokuwa na hakika kuhusu uhusiano wako na Mungu? Je, usingelipenda kuwa na uhakika? Je, hupendi kuwa na uhakika, na kufahamu kwamba umeokolewa?

Kama umetengwa na Mungu, tafadhali tambua kwamba damu ya thamani ya Kristo inaweza kuwahesabia haki wenyewe dhambi (Warumi 5:9). Inaweza kuisafisha dhamiri yako (Waebrania 10:22). Inaweza kuondoa dhambi zako (Ufunuo 1:5). Inaweza kukuletea ukombozi wa kweli kwenye moyo wako ambao umeshikwa mateka na Shetani (Waefeso 1:7).

Hata hivyo, ili uweze kupata msamaha wa dhambi kutoka kwa Mungu, ni lazima uyatii mapenzi yake kwa kubatizwa. Kwa hakika, tunakutia moyo na kukusihi kulifanya hilo wakati huu. Wasiliana na mtu aliyekupatia kitabu hiki cha Tafuta Kweli, na pawepo na mtu wa kukubatiza katika Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zako. Unapokuwa umebatizwa, ndipo unapoweza kuifahamu amani ipitayo akili zote (Wafilipi 4:7). Unaweza ukatambua kwamba upo kwenye familia ya Mungu, kanisa.



Unapoitii kweli kwa kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zako, unaweza ukafahamu kwamba nafsi yako imetakaswa (1 Petro 1:22). Kulingana na Wakolosai 1:22-23, kama unadumu katika imani – kwa kujengwa na kuwa imara katika Injili ya Kristo – utakapofika wakati wa kuondoka katika maisha haya, unaweza kutarajia rehema za Mungu na kutarajia Kristo kukutambulisha mbele ya kiti cha enzi kama mtu asiye na hila wala mawaa.

Uamuzi huu ni wa muhimu kuliko yote katika maisha yako. Lakini lenye umuhimu sawa na hilo – kama unaamini kwamba tayari umeshaokolewa – ni uamuzi wa ama kile ulichokifanya ili uokolewe kinaendana na mapenzi ya Mungu au la. Je, ulizitii amri za Mungu, au amri za wanadamu? Je, majibu yako kwa maswali tuliyoyauliza hapo awali katika somo hili yanalingana na yale yanayopatikana katika neno la Mungu?

Kwa mfano, Je ulifundishwa kwamba, ili ufanyike kuwa mkristo, unapaswa kumwamini Yesu tu na kumwomba aingie moyoni mwako? Je, ulifundishwa kwamba ili uweze kuokoka, unapaswa kuongozwa sala ya toba? Au je, ulifanyika kuwa mkristo kwa kumwamini Yesu, kulikiri jina lake, kuzitubia dhambi zako na kubatizwa?

Kama ulibatizwa, Je, ulibatizwa kwa kunyunyuziwa, kumwagiwa au kuzamishwa majini? Je, ulibatizwa ukiwa mtoto

Kuhusu Ubatizo

mchanga au mtu mzima? Ubatizo wa kweli kama unavyozungumziwa na Mungu ni kuzamishwa/kutoswa majini, na unahitaji imani na toba. Kama tulivyoona, ubatizo ni kwa ajili ya kumuunganisha mwenye dhambi na kifo cha Kristo ili aweze kuoshwa dhambi. Je, hii ndiyo sababu iliyokufanya wewe ubatizwe? Je, ulibatizwa ili uokoke? Au ulibatizwa huku ukiamini kwamba tayari ulikuwa umeshaokoka? Kulingana na Biblia, ubatizo ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Hivyo basi, kama ulifundishwa kwamba ulishaokolewa kabla ya ubatizo, Je, ulibatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi?

Kama majibu yako hayalingani na ukweli tuliouona kwenye Biblia, tunakutia moyo uirekebishe hali yako sasa. Kubatizwa kwa sababu sahihi, na katika njia sahihi, na kulingana na ukweli wa Injili ni jambo la muhimu kabisa.

Hili ni sawa na lile lililotokea katika mji wa Efeso, wakati mtume Paulo alipokutana na baadhi ya wanafunzi ambao hawakubatizwa kwa sababu sahihi. Hadithi hii imeandikwa katika sura ya kumi na tisa ya kitabu cha Matendo, na inaeleza kwamba kuna baadhi ambao walikuwa wanafanya vitu vinavyofanana na aina ya ukristo (na wale ambao hata wamebatizwa). Hata hivyo, baada ya kujadiliana kwa kirefu na Paulo, akagundua kwamba ubatizo wao haukufanywa kulingana na mapenzi ya Mungu. Na ndipo katika hatua ile Paulo akayasahihisha mawazo yao potofu kuhusu ubatizo wao. Waliitikia kwa kubatizwa tena. Hata hivyo wakati huu ubatizo wao ulifanyika katika jina la Yesu Kristo. Ubatizo wao wa kwanza bila shaka ulifanyika kwa lengo zuri tu, lakini haukuwa sawa sawa na ukweli wa Injili.

Je, ni wangapi leo ambao wamebatizwa kwa lengo zuri tu, lakini bado hawajafanya sawa sawa na kweli? Kwa mfano, kama ubatizo wako haukufanyika kwa kutoswa/kuzamishwa majini, au kwa ajili ya ondoleo la dhambi, Je, kwa uaminifu kabisa unaweza kusema kwamba umebatizwa kulingana na kielelezo cha Mungu kinachoonekana katika neno lake?

Kumbuka kwamba utahukumikiwa kupitia neno la Mungu. Je, unaweza kusema – bila shaka – kwamba ubatizo wako ulifanyika sawa kabisa na ule unaoelezewa na Biblia?

Kwa mara nyingine tena, kielelezo hicho kinamhitaji mwenye dhambi afuate hatua za wokovu, ambazo zinahusisha...

- **Kusikia Injili (Yohana 6:45, Warumi 10:17)**
- **Kuamini Injili (Marko 16:16, Yohana 8:24)**
- **Kutubu dhambi (Luka 13:3)**
- **Kukiri kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu (Mathayo 10:32-33; Warumi 10:10, Mdo. 8:37)**
- **Kutoswa/kuzamishwa (Kubatizwa) kwa ajili ya ondoleo la dhambi (Mdo. 2:38, 22:16; 1 Petro 3:21)**
- **Kuishi maisha ya uaminifu mpaka kufa (Ufunuo 2:10).**

Kama huna uhakika kabisa wa ama ulizifuata hatua hizi ipaswavyo au la, tafadhali basi usitoe nafasi ya kuikosa mbingu. Tafadhali utii ukweli leo. Kumbuka kwamba ukweli na ni ukweli pekee ndio utakao kuweka huru (Yohana 8:32).

SEHEMU YA MARUDIO: JE, UMEBATIZWA KULINGANA NA MAANDIKO?

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana hapo juu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na Marko 16:15-16, Yesu alisema, “Enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa _____ kiumbe. Aminiye na _____ ataokoka.”
2. Damu ya thamani ya Yesu _____ wenye dhambi, husafisha _____ zako, huondoa na huleta _____ safi.
3. Unapobatizwa, unaweza ukaifahamu amani ipitayo akili zote. Unaweza ukajua kwamba uko ndani ya _____ wa _____, kanisa.
4. Kulingana na mstari hapo chini, unapoutii ukweli kwa kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi, unaweza ukafahamu kwamba roho yako _____.

Sura ya 6

Mkiisha kuzitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo (1 Petro 1:22).

5. Kulingana na mstari hapo chini, kama watu wamebatizwa katika njia isiyo sahihi, Je, wanapaswa kubatizwa katika njia sahihi? NDIYO/HAPANA

Ikawa, Apolo alipokuwa Korintho, Paulo, akiisha kupita kati ya nchi za juu, akafika Efeso; akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko; akawauliza, "Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?" Wakamjibu, La, "hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia." Akawauliza, "Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani?" Wakasema, "kwa ubatizo wa Yohana." Paulo akasema, "Yohana alibatiza kwa ubatizo wa toba, akiwaambia watu wamwamini yeye atakayekuja nyuma yake, yaani, Yesu." Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu (Mdo 19:1-5).

6. Kielelezo cha Agano Jipya ambacho mwenye dhambi anapaswa kukifuata ili aweze kuokolewa kinahusisha yafuatayo:

- a. _____ Injili (angalia mstari hapo chini)

Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo (Warumi 10:17)

- b. _____ Injili (Marko 16:16)

- c. _____ dhambi (angalia mstari hapo chini)

Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu (Mdo. 17:30).

- d. _____ kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu (angalia mstari hapo chini).

Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni (Matthayo 10:32).

- e. _____ kwa ajili ya ondoleo la dhambi (angalia mstari hapo chini).

Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake (Mdo. 22:16).

- f. Kuwa _____ mpaka kufa (angalia mstari hapo chini).

Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyu ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima (Ufunuo 2:10).

7. Kulingana na mstari hapo chini, ukweli tu kama unavyopatikana katika maneno ya Yesu ndio utakaotuweka _____.

Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, "Nanyi mkikaa katika neno langu, mme-kuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru" (Yohana 8:31-32).

MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUJIFUNZIA yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

Kuhusu Ubatizo

MASUALA YA MAAMUZI

Mwanzoni mwa sura hii ya Tafuta Kweli kuhusu Ubatizo, uliombwa ujibu maswali kadhaa ya muhimu kuhusu wokovu. Hebu rudi nyuma na uyaangalie majibu yako na uyalinganishe na kile ulichojifunza katika somo hili, halafu ujibu maswali yafuatayo:

- A. Je, kwa sasa wewe upo katika uhusiano wa kuokolewa na Mungu? NDIYO/HAPANA
 - B. Je, unaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu? NDIYO/HAPANA
 - C. Kama tulivyoona, Yesu anaamuru toba. Je, upo tayari kufanya mabadiliko katika maisha yako ambayo Yesu ameyaamuru na kumuishia Mungu? NDIYO/HAPANA
 - D. Kulingana na Agano Jipya, kama hujabatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi katika jina la Yesu Kristo, Je, umeokoka? NDIYO/HAPANA
 - E. Kulingana na Agano Jipya, kama hujabatizwa katika njia sahihi, na sababu sahihi, Je, umeokoka? NDIYO/HAPANA
 - F. Kulingana na mstari hapo chini, Je, unampenda Yesu? NDIYO/HAPANA
- Mkinipenda, mtazishika amri zangu (Yohana 14:15).*
- G. Je, unataka kumtii Yesu? NDIYO/HAPANA
 - H. Je, ni wakati gani unataka kumtii Yesu? _____
 - I. Kutokana na kwamba Yesu anakutaka ubatizwe, na sasa unaelewa umuhimu wa kubatizwa wakati huu, Je, siitampendeza Mungu kwa wewe kubatizwa sasa hivi? NDIYO/HAPANA
 - J. Je, leo utanza kukataa majina mengine yote ya kidini na kuanza kujitambulisha kama mkristo tu? NDIYO/HAPANA
 - K. Angalia mistari hapo chini. Baada ya ubatizo wako, Je, utakuwa mwaminifu katika kuhudhuria ibada za kanisa la Bwana? NDIYO/HAPANA

Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia (Waebrania 10:24-25).

MASUALA YA MAZUNGUMZO

- A. Je, inatosha kuwa na “nia njema” wakati mtu anapobatizwa?
- B. Je, ni uamuzi gani mmoja wa muhimu sana ambao mtu anaweza akaufanya katika maisha yake?
- C. Je, makundi yote ya kidini yanafundisha kwamba ubatizo ni wa lazima ili mtu aweze kupata wokovu? Je, ni kwa nini ndivyo au sivyoyote?
- D. Je, ni mafundisho gani ya uongo au mapokeo ya wanadamu ambayo yapo, yanayoupuuzia umuhimu wa ubatizo wa maji? Je, ni kwa jinsi gani maandiko yanavyolipinga hili fundisho la uongo?



Sura ya 6

HITIMISHO

Rafiki, Je, umeitii kweli, au Je, umezitii amri za wanadamu? Mtume Petro anawakumbusha wasomaji wake kwamba walipoitii kweli, roho zao zilitakasika. Kama ukizitii amri au mapokeo ya wanadamu katika kutaka kufanyika kuwa mkristo, basi hujautii ukweli.

Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo (1 Petro 1:22).

Roho iliyotakaswa hutoka katika kuutii ukweli pekee. Ukweli unaotoka kwa Yesu, kama unavyofunuliwa katika Mathayo 7:21-23, ni kwamba, si kila mtu anayeliitia jina la Bwana ataokoka. Badala yake, ni wale “wayafanyayo mapenzi ya Baba” ndiyo wataokoka.

Je, wewe umeyatenda mapenzi ya Baba? Je, umebatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zako katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu (Mathayo 28:19) ili ufanyike kuwa mshiriki wa kanisa la Yesu Kristo? Kama sivyo, usichelewe. Nenda katafute kanisa la Kristo, na umuombe mmoja wa washiriki wake akubatize kwa ajili ya ondoleo la dhambi zako. Baada ya ubatizo wako, uanze kuabudu kulingana na ukweli wa Injili. Ujiite mkristo – na si zaidi.

Yatoe maisha yako moja kwa moja kwa Bwana na kanisa lake. Utafute kwanza ufalme wa Mungu, na kamwe usiache kukutanika na kanisa. Na hatimaye wakati wote uyakumbuke maneno haya toka kwa Yesu:

Basi Yesu akawaambia Wayahudi waliomwamiini, “Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru” (Yohana 8:31-32).

Huu ndiyo wakati muafaka. Leo ndiyo siku ya wokiovu. Huu ndiyo wakati wa kuiamini na kuitii kweli. Sasa kwa kuwa unaifahamu kweli, Je, utaitii wakati huu? Kesho inaweza isifike. Yesu alisema, “Mkinipenda, mtazishika amri zangu” (Yohana 14:15). Kama kweli unampenda Yesu, basi utautii ukweli kuhusu Muumba, ukweli kuhusu mamlaka katika dini, ukweli kuhusu kanisa, ukweli kuhusu nyumba ya Mungu na ukweli kuhusu ubatizo.

Je, utajibu nini? Je, utaiamini na kuitii kweli? Umilele wako utaamuliwa na kile utakachoifanyia kweli. Sasa hili ni juu yako. Tunatumaini na kuomba kwamba wewe uishi kulingana na kweli.

MARUDIO YA SURA

Majibu ya maswali yafuatayo yanapatikana ndani ya sura hii.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Katika Agano Jipya, _____ ili-kuwa ni sehemu ya muhimu sana ya mpango wa Mungu wa kuokoa roho.
2. Je, kumnyunyizia au kumwagia mtu maji kama aina fulani ya ubatizo ni sehemu ya ukristo wa kweli? NDIYO/HAPANA
3. Kulingana na Warumi 6:17-18, wenye dhambi ambao walikuwa watumwa wa dhambi hawakuyatii mafundisho kuhusu kifo, maziko na ufufuo wa Kristo, badala yake walitii _____ ya mafundisho/elimu ili wafanyike kuwa watumwa wa haki.
4. _____ ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na pia njia ambayo mtu hufanyika kuwa mtumwa wa haki, mwana wa Mungu, na _____.
5. Je, watoto wadogo au vichanga wanapaswa kubatizwa? NDIYO/HAPANA
6. Kulingana na Marko 16:16 na Mdo. 2:38, Je, mtu anapaswa afanye nini kabla hajabatizwa? _____ na _____.
7. Kulingana na Luka 9:23, Yesu alisema, “Mtu yeyote akitaka kunifuata, _____ mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, _____.”

Kuhusu Ubatizo

MASWALI YA KUTILIA MKAZO

1. Kulingana na Yohana 8:31-32, Yesu alisema, "Mkikaa katika _____ langu, mme-kuwa _____ wangu kweli kweli; na _____ itawaweka huru."
2. Kulingana na Yohana 3:20-21, Yesu alisema kwamba "bali yeye _____ huja kwenye nuru."
3. Kulingana na Ufunuo 2:10 na Wakolosai 1:22-23, mtu anapaswa awe mwaminifu "mpaka _____" ili hatimaye aweze kuishi mbinguni.

MAJIBU kwa ajili ya MASWALI YA KUJIF-UNZIA na MASWALI YA KUTILIA MKAZO yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.

MAMBO UNAYOPASWA KUFHAMU

- Katika Agano la Kale na Agano Jipya, Mungu alitumia maji na damu katika mchakato wa kumtakasa na kumsafisha mwenye dhambi.
- Kuzaliwa mara ya pili kunahitaji ubatizo wa kutosa/kuzamisha.
- Ubatizo ni muhimu kwa ajili ya wokovu.
- Tendo la ubatizo linaenda sambamba na suala la kuitii Injili.
- Wale wasioitii Injili wataangamizwa milele.
- Dhambi hairithiwi, bali ni tendo lifanywalo makusudi kupitia mapenzi ya mtu.
- Watoto hawazaliwi katika dhambi na kwa njia hiyo hawahitaji kubatizwa – wako salama.
- Ili kubatizwa kulingana na maandiko mtu anapaswa kusikia Injili, kuamini, kutubu na kukiri.
- Ubatizo kwa ajili ya ondoleo la dhambi humuigiza mwenye dhambi katika mwili wa Kristo.
- Wale ambao ni sehemu ya mwili wa Kristo wanatambulika kama Wakristo.
- Ili kubaki kuwa mkristo wa kweli, mtu anapaswa adumu katika maneno ya Kristo.

KUCHIMBA ZAIDI

Somo hapo chini limekusudiwa kwa wale watu ambao wangependa kujifunza somo hili zaidi. Kuna maelezo ambayo kimsingi hayakujadiliwa ndani ya somo.



UMUHIMU WA KUUTHI UJUMBE WA MUNGU

Wala hawatamfundisha kila mtu jirani yake, na kila mtu ndugu yake, wakisema, Mjue BWANA; kwa maana watanijua wote, tangu mtu aliye mdogo miongoni mwao hata aliye mkubwa miongoni mwao, asema BWANA; maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena (Yeremia 31:34).

Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho (Yohana 12:48).

Mkinipenda, Mtazishika amri zangu (Yohana 14:15).

Ninyi mmekuwa marafiki zangu, mkitenda niwaamuruyo (Yohana 15:14).

Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuuzi, bali kwetu sisi tunaokolewa ni nguvu ya Mungu. Kwa kuwa imeandikwa, Nitaiharibu hekima yao wenye hekima, na akili zao wenye akili nitazikataa. Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mlete hoja wa zamani hizi? Je! Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu? Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa (1 Wakorintho 1:18-21).

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

1. Kulingana na Yeremia 31:34, Je, moja kati ya baraka za kumtii Mungu ni kusamehewa dhambi zetu? NDIYO/HAPANA
2. Kulingana na 1 Wakorintho 1:18-21, Je, baadhi ya watu wanauchukulia ujumbe wa Mungu kama "upuuzi?" NDIYO/HAPANA
3. Kulingana na Yohana 12:48, Je, Ujumbe wa Mungu ni upuuzi?
4. Je, Yesu alisema katika Yohana 14:15 na Yohana 15:14 kwamba kama tunampenda, tutamtii yeye? NDIYO/HAPANA

Sura ya 6



UMUHIMU WA DAMU YA KRISTO

Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi (Mathayo 26:28).

Wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu; ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake, ili aonyeshe hiki yake, kwa sababu ya kuziachilia katika ustahimili wa Mungu dhambi zote zilizotangulia kufanywa, apate kuonyesha haki yake wakati huu, ili awe mwenye haki na mwenye kumhesabu haki yeye amwaminiye Yesu (Warumi 3:24-26).

Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake (Warumi 6:3-5).

Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawa sawa na wingi wa neema yake (Waefeso 1:7).

Wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele. Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyonyunyiziwa wenye uchafu hutakasa hata kuusafisha mwili; basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai? (Waebrania 9:12-14).

Nao waimba wimbo mpya wakisema, “wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa” (Ufunuo 5:9).

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

- Je, Mathayo 26:28 na Waefeso 1:7 zinafundisha kwamba Kristo aliimwaga damu yake ili tupate ondoleo (msamaha) la dhambi? NDIYO/HAPANA.
- Je, Warumi 3:24-26 inafundisha kwamba ili sisi tupate msamaha wa dhambi kupitia damu ya Kristo, tunapaswa kumwamini Kristo (Hiyo ni kwamba ni lazima tumtii yeye)? NDIYO/HAPANA

7. Damu ya Yesu iokoayo roho ilimwagika katika mauti yake. Je, Warumi 6:3-5 inafundisha kwamba ubatizo unatuingiza katika mauti ya Yesu, mahali pale pale ambapo damu hiyo ilimwagika? NDIYO/HAPANA

8. Je, Waebrania 9:12-14 inafundisha kwamba tunaweza kutakaswa kwa damu ya mafahali na mbuzi? NDIYO/HAPANA

9. Je, Ufunuo 5:9 inafundisha kwamba Kristo alitukomboa kwa damu yake? NDIYO/HAPANA



UMUHIMU WA UBATIZO

Waliposikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, “Tutendeje, ndugu zetu?” Petro akawaambia, “Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mta-pokea kipawa cha Roho Mtakatifu” (Mdo. 2:37-38).

Kisha akawaleta nje akasema, Bwana zangu, yanipasa ni fanye nini nipate kuokoka? Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako. Wakamwambia neno la Bwana, yeye na watu wote walio-mo nyumbani mwake. Akawakaribisha saa ile ile ya usiku, akawaosha mapigo yao, kisha akabatizwa, yeye na watu wake wote wakati uo huo (Mdo. 16:30-33).

Basi sasa unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake (Mdo. 22:16).

Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo (Wagalatia 3:27).

Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja (Waefeso 4:4-5).

Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno (Waefeso 5:25-26).

Katika yeye mmetahiriwa kwa tohara isiyofanyika kwa mikono, kwa kuuvua mwili wa nyama, kwa tohara ya Kristo. Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu (Wakolosai 2:11-12).

Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa; si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake,

Kuhusu Ubatizo

kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu; ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu; ili tuhesabiwe haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu (Tito 3:4-7).

Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo (1 Petro 3:21).

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

10. Wakati hadhira ya Petro ilipouliza wanapaswa wataendeje katika Mdo 2:37, Petro akawajibu katika mstari unaofuata kwamba wanapaswa _____ na _____.
11. Katika Mdo. 16:30, askari wa kifilipi aliuliza, “Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?” katika Mdo.16:33, yeye na familia yake _____ wakati huo huo.
12. Kulingana na Wagalatia 3:27, tunapobatizwa _____ Kristo, _____ Kristo.
13. Kulingana na maelezo ya Paulo katika Waefeso 4:4, Je, leo kuna ubatizo wa aina ngapi? _____
14. Katika Waefeso 5:25-26, kishazi “kulisafisha kwa maji” kinazungumzia tendo gani? _____
15. Kulingana na Wakolosai 2:12, tunapobatizwa, “tunazikwa pamoja na Kristo katika ubatizo.” Je, tunaweza “kuzikwa” katika tamaduni ya “kumwagia” au “kunyunyiza” ambayo imekuwa ni mbadala wa kuzamisha mwili wote? NDIYO/HAPANA
16. Kulingana na Tito 3:4-5, Mungu “alituokoa kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya.” Kishazi “kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya” kinazungumzia tendo gani? _____
17. Je, Petro alisema ni nini “unaotuo kwa sasa” (1 Petro 3:21)? _____.



UMUHIMU WA “MATENDO YA MUNGU” (KAMA YANAVYO TOFAUTISHWA NA “MATENDO YA HAKI” YALIYOBUNIWA NA WANADAMU)

Mungu akaona matendo yao, yakuwa wameiacha njia yao mbaya. Basi Mungu akaghairi neno lile baya, ambalo alisema atawatenda; asilitende (Yona 3:10).

Maana kila mtu atendaye mabaya huichukia nuru, wala haji kwenye nuru, matendo yake yasije yakakemewa. Bali yeye aitendaye kweli huja kwenye nuru, ili matendo yake yaonekane wazi ya kuwa yametendwa katika Mungu (Yohana 3:20-21).

Kwa sababu hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria; kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria (Warumi 3:20).

Hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahehesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki (Wagalatia 2:16).

Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambyo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo (Waefeso 2:8-10).

Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa; si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu; ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu; ili tukihehesabiwe haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu (Tito 3:4-7).

Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake (Yakobo 2:24).

VITU VYA KUFIKIRI... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

18. Je, Yona 3:10 inafundisha kwamba Mungu huona matendo yetu mema, na kwamba hayo matendo mema hushawishi maamuzi yake kuhusu sisi? NDIYO/HAPANA
19. Je, Yohana 3:20-21 inafundisha kwamba “matendo

Sura ya 6

yetu yaonekane wazi ya kuwa yametendwa katika Mungu?” NDIYO/HAPANA

20. Kulingana na Warumi 3:20, Je, tunaweza kuziokoa nafsi zetu kwa kutenda “matendo ya sheria?” NDIYO/HAPANA
21. Je, Wagalatia 2:16 inasema kwamba tunaokolewa “kwa matendo ya sheria?” NDIYO/HAPANA
22. Je, Waefeso 2:9 inafundisha kwamba tunaokolewa kwa matendo? NDIYO/HAPANA
23. Je, Waefeso 2:10 inafundisha kwamba kuna matendo ambayo Mungu anatutaka tuenende nayo (tuyafanye)? NDIYO/HAPANA
24. Je, Tito 3:4-5 inafundisha kwamba tunaokolewa “kwa matendo ya haki tuliyoyatenda?” NDIYO/HAPANA
25. Je, Yakobo 2:24 inafundisha kwamba “mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake?” NDIYO/HAPANA
26. Kama Biblia inafundisha kwamba matendo hayatuokoi, lakini pia inafundisha kwamba matendo hutuokoa sisi, Je, hilo linatunesha kwamba kuna aina mbili tofauti za matendo zinazozungumziwa? NDIYO/HAPANA
27. Je, ni kweli kusema kamba aina moja ya matendo – “matendo ya haki tuliyoyatenda” – hayawezi kutuokoa sisi? NDIYO/HAPANA
28. Je, ni kweli kusema kwamba aina moja ya matendo – “matendo ya Mungu” (hayo ni matendo ambayo Mungu ametuamuru tuyatende) – yanaweza kutuokoa sisi? NDIYO/HAPANA



BARAKA ZA KUBATIZWA

Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya, akisema, Jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi. Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaozeka watu wapata elfu tatu.... Wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa (Mdo. 2:40-41,47).

Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama

Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima (Warumi 6:3-4).

Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo (Waefeso 1:3).

Kwa ajili ya hilo nastahimili mambo yote, kwa ajili ya wateule, ili wao nao wapate wokovu ule ulio katika Kristo Yesu, pamoja na utukufu wa milele (2 Timotheo 2:10).

MAMBO YA KUFIKIRIA ... WAKATI WA KUCHIMBA ZAIDI

29. Je, Mdo. 2:40-41,47 inafundisha kwamba Mungu aliwazidisha wale waliobatizwa kwa “wale waliookolewa” (kanisa)? NDIYO/HAPANA
30. Kulingana na Waefeso 1:3, Je, “baraka zote za rohoni” zinapatikana wapi? _____
31. Kulingana na 2 Timotheo 2:10, Je, wokovu unapatikana wapi? _____
32. Kama mtu hayupo ndani ya Kristo, Je, anaweza akapata baraka ye yote ya rohoni au wokovu? NDIYO/HAPANA
33. Kulingana na Warumi 6:3-4, Je, ni tendo gani limuingizalo mtu “ndani ya Kristo?” _____
34. Angalia kwa makini: Je, umebatizwa katika njia ambayo Biblia inafundisha ili uingizwe ndani ya Kristo na uwe na uwezo wa kuzifikia baraka za rohoni na wokovu? Kama sivyo, kwa nini?

MAJIBU kwa ajili ya **MASWALI YA CHIMBA ZAIDI** yanapatikana katika sehemu ya nyuma ya kitabu.



SURA YA 1: TAFUTA UKWELI KUHUSU UKWELI

1. 153,000
2. WENGI
3. a. HAPANA; b. NDIYO; c. mapenzi ya Baba yangu
4. NDIYO
5. ukweli
6. tabia zisizo za haki, matendo ya uongo ya kidini, tamaduni
7. a. Yesu; b. HAPANA
8. NDIYO
9. NDIYO
10. kweli
11. si sahihi
12. HAPANA



SURA YA 2: TAFUTA UKWELI KUHUSU MUUMBAJI

JE, ASILI INATUELEZA NINI KUHUSU MUNGU?

1. asili
2. udhuru
3. mbunifu mwenye akili
4. msanifu mwenye ujuzi
5. mti, asili
6. HAPANA
7. HAPANA
8. HAPANA

JE, TUNAWEZA KUFAHAMU NIA YA MUNGU?

1. HAPANA
2. HAPANA
3. andiko
4. NDIYO
5. Biblia
6. pumzi ya Mungu
7. Roho Mtakatifu
8. HAPANA

JE, BIBLIA INATUELEZA NINI KUHUSU MUNGU?

1. habari njema
2. NDIYO
3. HAPANA
4. tubu
5. mbali
6. upendo
7. tubu
8. NDIYO
9. HAPANA
10. NDIYO
11. HAPANA
12. NDIYO

MARUDIO YA SURA

Maswali ya kujifunza

1. NDIYO
2. Mungu
3. Hukumu
4. NDIYO

Maswali ya kutilia mkazo

1. HAPANA
2. HAPANA
3. NDIYO

CHIMBA ZAIDI ...

1. NDIYO
2. NDIYO
3. Mungu
4. ulimwengu, kila kitu
5. vitu vyote
6. NDIYO
7. NDIYO
8. moyo
9. vitu vyote

10. habari
11. kila kitu
12. alisema, aliamuru
13. vitu vyote
14. HAPANA
15. Muweza
16. haiwezi kuwa
17. kimbia
18. NDIYO
19. HAPANA
20. HAPANA
21. Huruma
22. NDIYO
23. zawadi njema, zawadi kamili
24. NDIYO
25. Upendo



SURA YA 3: TAFUTA UKWELI KUHUSU MAMLAKA KWENYE DINI

JE, MAMLAKA NI NINI?

1. tunayapata wapi
2. NDIYO
3. amri, uamuzi
4. NDIYO
5. HAPANA
6. NDIYO

JE, NI NINI AU NI NANI AMBAYE NDIYE MAMLAKA KATIKA DINI?

1. NDIYO
2. NDIYO
3. NDIYO
4. NDIYO
5. Baba (Mungu)
6. kanisa

JE, HAYA MAMLAKA
YALIDHIHIRISHWA KWA NJIA
GANI?

1. HAPANA
2. Mwana wake
3. NDIYO
4. NDIYO
5. imeandikwa
6. Roho Mtakatifu
7. sheria, Kristo
8. kitabu cha mwongozo
9. NDIYO
10. Kristo (Yesu)
11. NDIYO
12. roho, uzima

JE, KUNA KIWANGO ZAIDI YA
KIMOJA CHA MAMLAKA LEO?

1. NDIYO
2. NDIYO
3. HAPANA
4. uzima, utauwa
5. HAPANA
6. yote
7. HAPANA
8. alaaniwe
9. mara moja

JE, KUNA TOFAUTI GANI KATI
YA AGANO LA KALE NA AGANO
JIPYA?

1. NDIYO
2. kujifunza kwetu
3. timilizwa
4. agano jipya
5. linatoweka
6. sheria, lazimisha
7. kiongozi
8. NDIYO
9. NDIYO
10. NDIYO
11. NDIYO
12. itunze Sabato
13. mamlaka, imeandikwa

MARUDIO YA SURA

Maswali ya Kujifunza

1. yote

2. imeandikwa
3. uzima, utauwa

Maswali ya kutilia mkazo

1. HAPANA
2. HAPANA
3. neno

CHIMBA ZAIDI ...

1. kweli
2. ulimi
3. nuru, ufahamu
4. NDIYO
5. HAPANA
6. kweli
7. NDIYO
8. uongo
9. walinena, wakiongozwa
10. NDIYO
11. HAPANA
12. Mauti
13. HAPANA
14. HAPANA
15. NDIYO
16. waliyachunguza maandiko kila siku
17. ulimwengu, Mungu
18. NDIYO
19. Mungu, Yesu Kristo
20. wenye hekima, wapumbavu
21. NDIYO
22. ukweli
23. huru
24. NDIYO



SURA YA 4: TATUFA UKWELI KUHUSU KANISA

JE, KANISA NI NINI?

1. walioitwa
2. NDIYO

3. NDIYO
4. NDIYO
5. NDIYO
6. mkabatizwe, ondoleo la dhambi
7. waliookolewa
8. waliookolewa
9. NDIYO
10. nyumba ya Mungu, kanisa
11. NDIYO
12. mawe yaliyohai
13. a. Yesu; b. Yesu; c. sikia, amini, tubu, kiri, batizwa

JE, KANISA NI LA LAZIMA NA
MUHIMU?

1. HAPANA
2. NDIYO
3. kanisa, kusudi la milele
4. HAPANA
5. NDIYO
6. Ufalme (kanisa)
7. NDIYO
8. mwili wake
9. NDIYO
10. HAPANA
11. kanisa moja
12. HAPANA

JE, NI LAZIMA KANISA LIWE NA
UMOJA?

1. HAPANA
2. HAPANA
3. migawanyiko, iunganishwe pamoja
4. NDIYO
5. hapana jina jingine
6. moja
7. NDIYO
8. NDIYO
9. NDIYO

MARUDIO YA SURA

Maswali ya Kujifunza

1. Langu
2. waliookolewa
3. HAPANA



Maswali ya kutilia mkazo

1. HAPANA
2. Moja
3. a. la popote (Waefeso 5:25); b. maalumu (kama katika mkutaniko, Waebrania 2:12)

CHIMBA ZAIDI

1. Yesu
2. Yesu
3. NDIYO
4. kanisa
5. NDIYO
6. Lilichaguliwa toka mwanzo, limedhihirishwa
7. Yesu
8. pumzika
9. NDIYO
10. HAPANA
11. Wakristo
12. kifo, uzima wa milele
13. Kristo (Yesu)
14. HAPANA
15. taji ya uzima



SURA YA 5: TAFUTA UKWELI KUHUSU NYUMBA YA MUNGU

JE, NI NANI AMEIJENGA
NYUMBA YA MUNGU?

1. kanisa
2. NDIYO
3. a. Yesu; b. Yesu
4. kichwa, yote
5. yote, mbinguni, duniani
6. NDIYO
7. HAPANA
8. NDIYO
9. NDIYO

JE, SIFA ZA KIPEKEE ZA
NYUMBA YA MUNGU NI ZIPI?

1. milele
2. a. NDIYO; b. HAPANA; c. NDIYO
3. a. wazee/maaskofu; b. NDIYO; c. NDIYO; d. NDIYO; e. HAPANA
4. NDIYO
5. HAPANA
6. NDIYO
7. a. neno la Mungu (Biblia); b. NDIYO
8. NDIYO
9. omba
10. lilinenwa (lililubiriwa, lilitangazwa)
11. toa (changia)
12. mega mkate
13. imba
14. HAPANA
15. Muziki
16. NDIYO
17. NDIYO

JE, LEO, TUNaweza
KUIANZISHA NYUMBA YA
MUNGU?

1. NDIYO
2. mapokeo
3. tii
4. kuwa na urafiki
5. NDIYO
6. ongeza, ondoa

MARUDIO YA SURA

Maswali ya Kujifunza

1. kweli
2. hekalu
3. mkristo

Maswali ya Kutilia makazo

1. Kristo (Yesu)
2. Sifa
3. NDIYO

KUCHIMBA ZAIDI

1. HAPANA
2. NDIYO
3. ufalme wa Mungu
4. ufalme (kanisa)
5. NDIYO

6. HAPANA

7. Wakristo
8. NDIYO
9. NDIYO
10. watakatifu
11. NDIYO
12. NDIYO
13. NDIYO
14. NDIYO
15. NDIYO
16. NDIYO
17. NDIYO
18. roho, kweli
19. NDIYO
20. NDIYO
21. katika, nje ya
22. NDIYO
23. endelea kwa bidii
24. NDIYO
25. kufanikiwa
26. anayetoa kwa moyo wa ukujufu
27. HAPANA
28. mauti ya Bwana
29. kupambanua
30. moyo
31. kwa wingi, kwa uchache
32. NDIYO
33. kifo, uzima
34. amani, kujengwa
35. NDIYO
36. NDIYO
37. kuu
38. HAPANA
39. Mungu (Baba)
40. NDIYO
41. kwenda na kutoka
42. maneno
43. fundisho
44. okoa
45. kujivuna, si kitu
46. mafundisho yenye uzima
47. uaminifu, uchaji, kutokuharibika, maneno yenye uzima
48. HAPANA
49. moja
50. Kristo Yesu

51. NDIYO
52. urithi wa milele
53. Yesu Kristo
54. Dhambi



SURA YA 6: TAFUTA UKWELI KUHUSU UBATIZO

JE, UBATIZO NI NINI?

1. Kusafishwa
2. kuteremka katika
3. NDIYO
4. NDIYO
5. HAPANA
6. HAPANA
7. zamisha
8. sehemu za kubatizia

JE, DHUMUNI LA UBATIZO NI NINI?

1. maji
2. waliokoka, ubatizo
3. damu
4. maji
5. damu
6. mnahesabiwa haki
7. huna hatia
8. damu, maji, kuhesabiwa haki
9. imani pekee
10. inafanya
11. tii
12. injili ya Kristo
13. NDIYO
14. Mungu, itii injili
15. HAPANA
16. alibatizwa
17. ondoleo (msamaha)
18. maji

19. ubatizo
20. unaokoa
21. NDIYO
22. alibatizwa
23. mwili

JE, NI NANI ANAYEPASWA KUBATIZWA?

1. aaminiye, kubatizwa
2. NDIYO
3. Mwana
4. Kusikia
5. kutubu
6. HAPANA
7. dhambi
8. kukiri
9. NDIYO
10. HAPANA
11. HAPANA
12. HAPANA

JE, UMESHAWAHI KUBATIZWA KULINGANA NA MAANDIKO?

1. kila, kubatizwa
2. kuhesabiwa haki, moyo, ukombozi
3. familia, Mungu (au mwili, Kristo; au ufalme, Mungu)
4. kusafishwa
5. NDIYO
6. a. kusikia; b. kuamini; c. kutubu; d. kukiri; e. kutoswa/kubatizwa; f. kwa uaminifu.
7. Huru

MARUDIO YA SURA

Maswali ya Kujifunza

1. maji
2. HAPANA
3. namna (kielelezo)
4. Ubatizo, Mkristo
5. HAPANA
6. amini, tubu
7. kana, fuata

Maswali ya Kutilia mkazo

1. neno, wanafunzi, kweli, kweli
2. hutenda kweli
3. kifo

CHIMBA ZAIDI

1. NDIYO
2. NDIYO
3. HAPANA
4. NDIYO
5. NDIYO
6. NDIYO
7. NDIYO
8. HAPANA
9. HAPANA
10. tubuni, mkabatizwe
11. mkabatizwe
12. katika, mvaa
13. moja
14. ubatizo
15. HAPANA
16. ubatizo
17. ubatizo
18. NDIYO
19. NDIYO
20. HAPANA
21. HAPANA
22. HAPANA
23. NDIYO
24. HAPANA
25. NDIYO
26. NDIYO
27. NDIYO
28. NDIYO
29. NDIYO
30. katika Kristo
31. katika Kristo Yesu
32. HAPANA
33. ubatizo

VIPINDI VYA BIBLIA



Mwanzo 1:1,26

KIPINDI CHA MABABA

Adamu

- Kipindi cha mababa kilianza katika bustani ya Edeni na kuendelea kuwepo sambamba na kipindi cha Musa.

Mungu alizungumza na mababa Waebrania 1:1

EDENI



GHARIKA



KUTOKA



Dola ya Ashuru



Dola ya Babeli



Dola ya Uajemi



Dola ya Yunani



Dola ya Rumi

WAEBRANIA

KIPINDI CHA MUSA

Huduma ya Kristo
Mathayo 5:17

Kuvuka Bahari ya Shamu
Kutoka 20

- Kipindi cha Musa kilianza milima Sinai na kuendelea kuwepo sambamba na kipindi cha Mababa Mungu alizungumza kupitia Musa Waebrania 9:18-20

AMRI KUMI

SHERIA

UFALME ULIOGA WANYIKA



Kalvari
Waebrania 9:15-17

Je, ni lini kipindi cha Ukristo kitakoma?
"Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna ajiuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake."
Mathayo 24:36

KIPINDI CHA UKRISTO

Kristo

Kanisa la Kristo
ndiyo ufalme

Mungu anazungumza
kupitia Neno

KORNELIO
Mdo 10:1-48



PETRO SIKU
YA PENTEKOSTE

Biblia:

"Mbingu na nchi zitapita,
lakini maneno yangu hayatapita kamwe."
Luka 21:33
Mathayo 24:35



Mdo 2

Mataifa yote
Danieli 7:14 Wagalatia 3:28





Je, tunakwenda wapi tunapokufa?

Ulimwengu
(Mahali pa kuishi)

Sheol au Kuzimu
(Mahali pa wafu)

Mbinguni

“Njoni”

“Njoni”
Njoni, mliobarikiwa
...urithini ufalme
(Mathayo 25:34)

“Ondokeni”

“Ondokeni”...katika
moto wa milele
(Mathayo 25:41)

Jehannamu

Mauti

Waliookolewa

Mlango mwebamba

Paradiso

Kumewekwa Shimo Kubwa

Walipopotea

Mlango mpana

Mateso

Mauti

Ufufuo

Hukumu

Siku ya

Kuzawadiwa

Kuhukumiwa

“Ondokeni”

WALIOOKOLEWA: Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa (Mab 2:47)
WALIOPOTEA: Wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu (2 Wathesalonike 1:7-8)

MAUTI: Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu (Waebrania 9:27)

MLANGO MPANA: Mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi walingiao kwa mlango huo (Mathayo 7:13)

MLANGO MWEBAMBA: Mlango ni mwebamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao wajiano ni wachache (Mathayo 7:14)

PARADISO: Uta kuwa pamoja nami peponi. (Luka 23:43)

MATESO: Kuzimu alipokuwa katika mateso (Luka 16:23)

UFUFUO: Ufufuo wa wafu (1 Wakorintho 15:42-44)

SIKU YA HUKUMU: Na kama vile watu walivyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu (Waebrania 9:27)

MBINGUNI: Urithi uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu (1 Petro 1:4).

JEHANAMU: Mungu ana uwezo wa kuangamiza mwili na roho pia katika jehannamu (Mathayo 10:28).

SHIMO KUBWA: Kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa (Luka 16:26)